BUNGE LA TANZANIA

———

MAJADILIANO YA BUNGE

———

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Thelathini na Tisa - Tarehe 5 Agosti, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo zimewasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):

Hati ya Matumizi ya Ziada bila Idhini ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2000/2001 *(Statement of Excess Vote for the Year 2000/2001).*

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 2 na Na. 4 ya Mwaka 2002/2003 *(Statements of Reallocation Warrant No. 2 and No. 4 of 2000/2001).*

MASWALI NA MAJIBU

Na. 379

Maombi ya Mashamba Yaliyomilikiwa na Chavda

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa katika mkutano wa wadau wa Mkonge uliofanyika Tanga mwaka 2001 chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, wadau hao kwa niaba ya wananchi walipendekeza na kuomba mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na Chavda katika Wilaya ya Muheza na Korogwe yafutiwe Hati Miliki na kugawanywa kwa wananchi:-

(a) Je, mapendekezo hayo sasa yamefikia wapi?

(b) Kwa kuwa Benki ya *CRDB (1996) Limited* ndiyo iliyoweka dhamana ya mkopo kwa baadhi ya mashamba hayo makubwa; je, hati miliki za mashamba hayo zimebadilishwa na kuwa katika jina la *CRDB (1996) Limited?*

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani za kumpata Chavda ili alipe fedha hizo zilizodhaminiwa na *CRDB (1996) Limited?*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kufuta hati miliki ya mashamba makubwa na kuyagawa kwa wananchi yalikwisha anza kutekelezwa kabla ya zoezi la kubinafsishwa kwa mashamba ya Mkonge. Serikali ilishatoa na kuwagawia wananchi waliokuwa wanazunguka mashamba haya jumla ya hekta 38,666. Kati ya Wilaya zilizonufaika na mgao huo kutokana na kumegwa kwa mashamba makubwa ni Wilaya ya Kilosa hekta 6,944 kutoka kwenye mashamba ya Mbugani, Magole na Ulaya, Manispaa ya Tanga hekta 761 kutoka kwenye mashamba ya Kange/Mgwisha; Wilaya ya Muheza hekta 530 kutoka kwenye shamba la Sagula na Wilaya ya Korogwe hekta 15,266 kutoka kwenye mashamba ya Magoma, Magunga, Ngombezi na Gomba.

Zoezi hili halikufanikiwa kwani kinyume na matarajio, maeneo yaliyogawiwa wakulima wadogo wadogo hayajaendelezwa ipasavyo, hivyo Serikali ikalazimika kuagiza kuwa utaratibu wa kuyagawa mashamba makubwa usitishwe. Aidha, Mkoani Tanga kuna maeneo mengi na makubwa ya ardhi ambayo hayajaendelezwa na yanafaa kugawiwa wananchi ili mashamba makubwa yatumike kuendeleza zao la Mkonge.

(b) Mheshimiwa Spika, Hati Miliki za mashamba hayo hazijabadilishwa majina na kuwa za benki ya *CRDB (1996) Limited* isipokuwa zilisajiliwa kwa Msajili wa Hati kuthibitisha kwamba mashamba hayo yalitolewa kama dhamana *(mortgage)* katika benki ya *CRDB (1996) Limited.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua hujuma zilizofanywa na Chavda, imempiga marufuku kuingia nchini Tanzania na imekamata mali zake zilizohusika na ukopaji wa mamilioni ya fedha ambazo zitauzwa na kama hazitatosha kufidia madeni yake, mali nyinginezo ambazo hazikuhusika na mkopo huu zitakamatwa na kuuzwa.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini ningeomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa sababu hadi sasa hivi Chavda bado hajapatikana. Ni kwa nini Serikali isitumie utaratibu wa Kimataifa wa kumkamata Chavda na kumrudisha hapa nchini ili aweze kulipa madeni haya ya Taifa?

Pili, iwapo hati zile hazijabadilishwa maana umiliki wa mashamba bado una utata. Aidha, bado uko kwa Chavda au uko kwa Benki ya *CRDB*. Je, Serikali haioni ni vema sasa hati hizo zikajulikana umiliki wake sahihi uko kwa nani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kumkamata Chavda unafanywa na taratibu za kiserikali kwa maana iko chini ya sheria na dola na nina hakika kwamba kwa sababu yuko nje ya nchi lazima Serikali itakuwa inafanya jitihada za kuwasiliana na vyombo vya Kimataifa *(Interpol)* ili kuweza kumkamata Bwana Chavda.

Pili, hati bado hazijabadilishwa ni kweli lakini katika suala hili kwa sababu ilikuwa limeshafikia Mahakamani ubadilishaji wa hati hizi kutoka *CRDB* kwa mmiliki mwingine bila shaka utasubiri mpaka hatima ya kupatikana kwa Bwana Chavda ikamilike.

MHE. JOEL N. BENDERA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Chavda toka ameondoka ameacha mashamba haya mengi tu katika Mkoa wa Tanga, shamba la Hale Mwakinyumbi na Kwashemshi ni mashamba ambayo Mheshimiwa Herbert Mntangi, ameyatamka na kuna wananchi wengi ambao wapo kule amewaacha wanaishi katika mazingira ambayo hakuna mashamba wala hakuna Mkonge na wala hawalipwi chochote na huyu Chavda hatarudi na wananchi wale wako pale. Je, kwa kuzingatia kwamba *CRDB* ni Serikali na wananchi wale wanateseka na wameshaanza kulima mashamba haya. Je, Serikali haioni busara kuwaachia wananchi wale walioko katika maeneo yale wakaendelea kulima ili waweze kuishi na kujiendeleza katika maisha yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni suala la msingi sana kuwaachia maeneo haya wakulima wayalime ili kujipatia riziki na maisha yao na ndiyo maana katika maeneo haya wakulima wengi wameambiwa wanaweza wakayatumia

kwa kupanda mazao ambayo si ya kudumu kwa hivi sasa kwa sababu mashamba hayo bado yana mgogoro. Lakini vile vile tayari maeneo mengine kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi yamekwishagawanywa kwa wananchi na nina hakika kabisa kwamba Halmashauri ya Korogwe ilipewa jukumu la kugawa maeneo hayo wakati wakisaidiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi wa Wizara hii kwamba inaonyesha kwamba Chavda amepewa kibali cha muda kuishi nchini. Sasa nimepata taarifa kutoka Serikalini kwamba hayupo nchini. Sasa tupate taarifa ya kweli. Hivi Chavda yupo nchini ama hayupo nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, taarifa nilizopewa mimi ni kwamba Chavda yuko nje. Lakini kama yeye ana habari kwamba ana kibali cha muda tutakutana naye, yeye na mimi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kupata ufafanuzi zaidi.

Na. 380

Kupambana na Umaskini

MHE. LEONARD N. DEREFA aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali ilitangaza kuwa kutakuwa na fedha zitakazotokana na msamaha wa madeni ambazo zitatumika katika mpango wa kupambana na umaskini:-

Je, Mkoa wa Shinyanga umepangiwa fedha kiasi gani katika mpango huo wa kupambana na umaskini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi chache maskini kuingia katika mpango wa msamaha wa madeni kutokana na mpango wa *Highly Indebted Poor Countries (HIPC).*

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kuingia katika mpango huu, kulitokana na utekelezaji mzuri wa Sera za kiuchumi unaoendelea hivi sasa na kukamilishwa kwa mkakati wa kupunguza umaskini wenye kuzingatia matakwa na mahitaji ya wananchi walio wengi, yaliyopatikana kwa njia shirikishi hapo mwaka 2000. Msamaha huu wa madeni umeiongezea Serikali uwezo zaidi wa kupambana na umaskini na hivyo kuongeza Bajeti yake inayoelekezwa katika juhudi za kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, tangu kipindi hicho Serikali imekuwa ikielekeza fedha hizo katika huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji, barabara na kilimo, kwa maeneo ya mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotokana na misamaha ya madeni hayo si fedha za ziada kutoka nje, bali hizi ni fedha zinazotokana na juhudi zetu Kitaifa kupitia mauzo nje na makusanyo ya kodi na huingizwa moja kwa moja katika Hazina ya Taifa kama vyanzo vingine vya mapato na kupangiwa matumizi kufuatana na taratibu na vipaumbele tulivyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na utaratibu wa mgawanyo niliioueleza hapo juu siyo rahisi kuainisha kiasi cha fedha kilichoelekezwa Mkoani Shinyanga kutokana na msamaha wa madeni pekee. Lakini inawezekana kabisa kuainisha ongezeko la Bajeti katika Mkoa wa Shinyanga tangu Serikali iingie katika mpango wa *HIPC*. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2000/2001 Mkoa wa Shinyanga ulipatiwa shilingi 11,266,962,082/=, mwaka 2001/2002 shilingi 12,111,758,100/= na mwaka 2002/2003 shilingi 16,079,440,500/=. Ongezeko la shughuli mbalimbali zinazoendelea mkoani Shinyanga katika nyanja za elimu, afya, maji na barabara zinatokana na mpango huo.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa iko Mikoa na Wilaya zinazorundikiwa miradi mingi sana ya Kitaifa kama

vile *TASAF, HIPC* na miradi mingine mingi ya Kitaifa kwa kisingizio kwamba hizo ni Wilaya maskini au *pilot areas* au wafadhili wamependelea huko na kwa kuwa ziko Mikoa na Wilaya ambazo hazipati kwamba wao ni matajiri, kitu ambacho siyo kweli, je, Serikali iko tayari kupokea lawama na aibu na malalamiko kwa Mikoa ambayo haipati mgao huo? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Spika, sikubaliani naye anaposema kwamba baadhi ya mipango hii haitekelezwi katika Mikoa mingine. Nimesema ongezeko la fedha la zaidi ya shilingi bilioni 3 katika kipindi cha miaka miwili ni dalili ya wazi kwamba Serikali inasambaza mapato yake katika maeneo mbalimbali. Kuhusiana na baadhi ya Mikoa kuanzishiwa miradi kutokana na kuwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, yapo madai hata hapa Bungeni kwamba Mikoa iliyo nyuma iwe na upendeleo fulani na ndiyo jambo ambalo linatazamwa na Serikali na kwa hiyo, kwa mfano miradi ya *TASAF* hapa hapa tumetoa Semina na vile vile hotuba ya Ofisi ya Rais pamoja na Makamu wa Rais, tumesema *TASAF* hivi sasa wanajiandaa kwa mwaka huu kusambaa nchi nzima baada ya kufanya mazoezi sehemu zingine.

Kwa hiyo, hata hiyo mikoa anayosemea Mheshimiwa James Musalika, itafaidika na mradi huo na mwisho kutokana na maelezo yangu, Serikali haina sababu ya kukubali kwamba kuna aibu. Aibu ya namna gani wakati maendeleo yanaonekana sehemu zote? Juzi Mheshimiwa Rais, amefungua daraja la Mto Rufiji linaloitwa Daraja la Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, babarabara sehemu zote zinajengwa, shule na hospitali. Sasa aibu hii inatokana na nini? *(Kicheko/Makofi)*

Na. 381

Tofauti za Umaskini wa Vijijini na Mijini

MHE. KHALID S. SURU aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikifanya bidii za kuondoa umaskini miongoni mwa wananchi wake na hususan wale wanaoishi vijijini na baadhi ya miji midogo ya Kata na Tarafa na kwa kuwa yako mafanikio yanayoonekana katika suala la kuondoa umaskini wa huduma mbalimbali kama elimu, maji na afya katika maeneo mbalimbali nchini na kwa kuwa inaonyesha hatujafanikiwa kwa kiasi cha kuridhisha kuondoa umaskini wa kipato miongoni mwa wananchi hasa wale wanaojihusisha na uzalishaji mali kupitia kilimo na ufugaji huko mashambani na kwa kuwa wananchi wa kawaida kule vijijini wanaona umaskini wa kipato unaendelea kustawi miongoni m wao kwa sababu ya zana duni za kuzalisha mali, ukosefu wa barabara za kupitika wakati wote, kuyumba kwa masoko, kukosa misaada na mikopo na kukosekana kwa mazingira mazuri ya kuwezesha kutumia nguvu kazi ya vijana wetu katika uzalishaji mali wa kisasa unaowavutia kukaa na kuishi vijijini:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza na kufafanua tofauti za umaskini wa vijijini na mijini kwa kutaja takwimu zake na kama ni kweli kwamba umaskini wa kipato miongoni mwa wananchi bado ni tatizo linalostahili kupewa uzito na je, Serikali inaweza kutaja baadhi ya mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Kata za Mnenia, Kisese, Kikore, Changaa, Thawi, Suruke na Kikilo wana mabonde mazuri ya Mto Bubu ya kilimo cha umwagiliaji, lakini wanashindwa kupanua kilimo hicho kwa kukosa barabara ya kutolea nje mazao yao, je, Serikali inaweza kuchangia japo kidogo gharama za barabara hizo mbili kwa faida ya Taifa?

(c) Je, kwa nini tusianzishe programu ya matumizi bora ya nguvu kazi ya vijana kwa kuwapa zana na teknolojia muafaka ili kuondosha umaskini haraka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumjibu swali hilo ningependa nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ipo tofauti kubwa sana ya umaskini kati ya mijini na vijijini. Kulingana na tafiti mbalimbali zilizofanywa hapa nchini kama *survey* ya mapato na matumizi ya Kaya ya mwaka 1991/1992 na ile ya mwaka 2000/2001; umaskini wa kipato ni mkubwa zaidi vijijini kuliko mijini. Tafiti hizi pia zimeonyesha kwa ujumla kwamba kaya za vijijini ni maskini zaidi kuliko kaya kama hizo za mjini. Taarifa hizi zinaonyesha kwamba maendeleo yametokea zaidi katika maeneo ya mjini, hususan Dar es Salaam, wakati maeneo ya vijijini ni madogo sana maendeleo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, kama ifuatavyo:-

(a) Tofauti moja ni ile ya upatikanaji wa maji. Watu katika maeneo ya mjini wanapata maji ya kunywa salama zaidi kuliko watu wa vijijini. Kiasi cha asilimia 53 ya kaya za vijijini zinategemea maji yasiyo salama, wakati ambapo asilimia 86 ya kaya za Dar es Salaam na asilimia 76 katika maeneo mengine ya mjini zinapata maji ya bomba. Kaya za vijijini pia zinalazimika kutembea mwendo mrefu kupata maji, ni asilimia 49 tu ya kaya zilizo ndani ya kilometa moja ikilinganishwa na asilimia 85 na asilimia 73 ya kaya za Dar es Salaam na maeneo mengine ya mjini.

Mheshimiwa Spika, tofauti zingine zipo katika hali ya kipato. Utafiti wa mwaka 2000/2001 unaonyesha kwamba zipo dalili za kupanda kwa kipato cha kaya ambayo inadhihirishwa na ongezeko la matumizi ya kaya. Baada ya kutilia maanani mfumuko wa bei, matumizi ya kaya yamepanda zaidi mijini. Dar es Salaam imeonyesha kupanda na kuongezeka kwa pato la kaya kwa asilimia 47 wakati maeneo ya vijijini pato limepanda kwa asilimia 11 tu.

Aidha, viwango vya umaskini vina uhusiano mkubwa na elimu ya mkuu wa kaya. Kiasi cha asilimia 51 ya watu ni maskini iwapo mkuu wa kaya hana elimu ikilinganishwa na asilimia 12 pale ambapo Mkuu wa Kaya ana elimu zaidi ya kiwango cha elimu ya msingi.

(b) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, haina dhamana ya usimamizi na ujenzi wa barabara moja kwa moja, badala yake Wizara zenye dhamana hii ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ujenzi. Ofisi ya Makamu wa Rais kazi yake ni kuratibu shughuli za kuondoa umaskini, hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais itawasiliana na Wizara husika kuhusu ombi hili la Mheshimiwa Mbunge.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuanzishwa kwa programu ya matumizi bora ya nguvu kazi ya vijana kwa kuwapa zana na teknolojia muafaka ili kuondoa umaskini haraka. Aidha, Serikali inahimiza Halmashauri za Wilaya na taasisi za kijamii zianze kuwawezesha vijana ili wajiletee maendeleo na kupunguza umaskini uliokithiri hususan vijijini.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Kuondoa Umaskini kwa majibu yake mazuri katika swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umaskini wa kipato ndiyo adui mkubwa anayeangamiza wananchi kule vijijini na kwamba adui huyu ili aweze kuangamizwa vizuri lazima tutumie nguvu kazi ya vijana. Lakini vijana hawa wanashindwa kwa sababu hawana uwezo, nyenzo hakuna. Je, Serikali itaanzisha mitambo midogo midogo ile ya *solar* kule vijijini ili kupunguza kazi za shuruba ili vijana wetu waweze kuzalisha mali zaidi na kuondoa umaskini?

Pili, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma ni moja ya ile mikoa ambayo ni maskini na pia Wilaya ya Kondoa ni moja ya zile Wilaya ambazo ni maskini zaidi katika nchi yetu. Je, Waziri atakubaliana na mimi

maombi kwamba ajitahidi kutupatia Wahisani ama Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutuongezea nguvu ili tuweze kufanya kazi ya kuondoa umaskini kule Kondoa? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Spika, umaskini wa kipato ndiyo unaonekana zaidi kwa sababu ndiyo unaomfanya mwananchi akose kwa mfano milo mitatu, akose nyumba bora, akose kuwaendeleza vijana wake shule na kadhalika. Ndiyo maana katika mkakati wa kuondoa umaskini tunazingatia kuimarisha miundombinu ambayo itamwezesha mwananchi kuzalisha na kupata masoko kwa urahisi zaidi kwa sababu kuna barabara safi, anatibiwa na kuondolewa matatizo mengine.

Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuongeza kasi katika kumwezesha kutengeneza mazingira ya kumwezesha mwananchi aondokane na umaskini wa kipato na ndiyo maana pia mfumko wa bei ukidhibitiwa unasaidia kumwezesha mwananchi kuwa na uwezo wa kujinunulia vitu vyake vizuri zaidi kuliko pengine ingekuwa vinginevyo.

Kuhusu kueneza nishati kama ya *solar* vijijini. Nakubaliana naye na sina shaka Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na kueneza umeme wa kawaida hilo nalo lipo pale ambapo pana uwezekano inasambazwa ingawa mpaka sasa kuna tatizo la bei kuwa kubwa katika hili la *Solar panel.*

Mheshimiwa Spika, mwisho la pili kuhusiana na Wahisani mkakati wa Serikali Wizara husika Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango ndiyo nguvu zinavyoelekezwa katika vipaumbele vyetu kwamba pale ambapo Mikoa imebainika iko nyuma kuliko mingine tunatilia nguvu zaidi. Siyo tu Wafadhili, lakini hata katika mgao wa fedha na hapa tuliwahi kukubaliana kwenye vikao vyetu hivi hivi kwamba nguvu ya Serikali iongezwe ili ionekane wazi ile mikoa iliyo nyuma kweli inapewa uwezo wa kujiondoa kwenye matatizo ya lindi ya umaskini. Tutazingatia ushauri wake.

Na. 382

Barabara ya Nyasa-Gare-Magamba

MHE. HENRY D. SHEKIFFU aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Nyasa-Gare-Magamba inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS;* na kwa kuwa barabara hiyo inalo eneo chepechepe kati ya Nyasa, Kongei na Gare; na kwa kuwa ni kipindi kirefu barabara hiyo haijapata matengenezo ya kuridhisha hususan katika eneo hilo chepechepe:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura za kurekebisha barabara hiyo hasa maeneo hayo korofi kabla ya kuanza kunyesha mvua za masika ili iweze kupitika wakati wote na wananchi waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi bila bughudha.

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyasa-Gare-Magamba yenye urefu wa kilometa 17.4 ni barabara ya mkoa ambayo inahudumiwa na Wizara yangu kwa kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Tanga.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya kawaida kati ya eneo la Nyasa-Gare lenye urefu wa kilometa 7 ambalo lilikuwa kwenye hali mbaya zaidi ukilinganisha na sehemu nyingine za barabara hii. Eneo hili pia lina wakati wengi zaidi na huduma nyingi za kijamii. Matengenezo yaliyofanyuika ni kuchonga barabara, kukata mifereji, kufyeka majani na kuweka changarawe sehemu korofi kwa gharama ya shilingi milioni 8.

Aidha, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2003/2004, imetenga jumla ya shilingi milioni 10 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ambayo yakikamilika barabara hii itapitika bila shida.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa matengenezo ya barabara hii hasa haya maeneo ambayo ni chepechepe ni kidogo sana. Kwa hiyo, matengenezo yanayofanyika ni kama kuahirisha tatizo tu. Kwa nini Serikali haitengi fedha za kutosha kukabili tatizo hili na barabara ipitike kwa wakati wote?

Pili, kwa kuwa mwaka huu Serikali imetamka kwamba ziko fedha za *STABEX* na kwa kuwa eneo hili ni eneo linalolimwa kahawa na wanaishi wananchi wengi wanaolima Kahawa. Je, Serikali itatamka wazi kwamba barabara hii itatengenezwa kwa fedha za *STABEX? (Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha inayotengwa kwa barabara hizi za Mikoa siyo tu kati ya Nyasa-Gare mpaka Magamba lakini kwa barabara zote za Mikoa nchini ni ndogo na hii inatokana na sungura wenyewe tuliyenaye.

Kwa hiyo, tunagawana kidogo kidogo ili kila mkoa uweze kupata sehemu katika barabara ya mkoa. Lakini ile sehemu ambayo inakuwa ngumu zaidi kama sehemu ya Kongei mpaka Gare tunahakikisha inatengenezwa ili walau barabara iweze kupitika. Kwa hiyo, ni tatizo hatuna uwezo wa fedha ndiyo tunafanya kutenga fedha kiasi hicho kinachoonekana.

(b) Hili suala la *STABEX,* si suala la Wizara ya Ujenzi peke yake linahitaji kushirikiana na Wizara zinazohusika kama vile Fedha, Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko na kadhalika. Kwa hiyo, tutamwakilishia Waziri, ombi lake Mheshimiwa Henry Shekiffu, ili awasiliane na Wizara zinazohusika na litakalowezekana litafanyika, lisilowezekana Mheshimiwa Mbunge atajulishwa.

Na. 383

***TANROADS* kuwa Msimamizi wa Barabara zote nchini**

MHE. ROBERT K. MASHALA (k.n.y. MHE. EMMANUEL E. KIPOLE) aliuliza:-

Kwa kuwa wakala wa barabara *(TANROADS)* wameonyesha uwezo mkubwa wa kusimamia matengenezo ya barabara Mikoani na barabara hizo zimeonyesha tofauti kubwa dhidi yake na zile zinazosimamiwa na Halmashauri:-

Je, isingekuwa vyema sasa jukumu la kusimamia barabara zote nchini likawa chini ya hao wakala wa barabara?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Emmanuel Kipole, kwa sifa alizozitoa kwa *TANROADS* kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa kusimamia matengenezo ya barabara mikoani. Lengo kuu la Serikali kufanya mabadiliko *(reforms)* katika utartibu wake wa utendaji kazi ni kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi. Tunaendelea kuimarisha wakala wa barabara kwa mtazamo huu.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* ilianzishwa mwaka 2000 chini ya sheria Na. 30 ya Wakala ya mwaka 1997 na sheria ya *Road Tolls (Ammendment)* Na. 2 ya mwaka 1998. Madhumuni makuu ya *TANROADS* ni kusimamia matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa *TANROADS* imeonyesha uwezo wa kusimamia matengenezo ya barabara kuu na zile za mikoa, bado inahitaji kujenga uwezo zaidi *(Capacity Building)* ili iweze kufanya majukumu iliyokabidhiwa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo haitakuwa vizuri kuiongezea *TANROADS* majukumu mengine ya kusimamia matengenezo ya barabara za vijijini na mijini wakati yale iliyokabidhiwa haijaweza kuyamudu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa ushauri kuwa tuendelee kuimarisha uwezo wa Halmashauri zetu ili ziweze kusimamia kazi za ujenzi hasa barabara. Naamini mgawanyo wa kazi baina ya Wizara ya Ujenzi na TAMISEMI, bado ni sahihi ila tatizo ni uwezo mdogo wa Halmashauri zetu.

MHE. ROBERT K. MASHALA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri zetu nyingi hazina uwezo wa kukabiliana na matatizo haya ya matengenezo ya barabara ya mara kwa mara. Je, Serikali inaziwezesha vipi Halmashauri hizi ili ziwe na uwezo wa kutengeneza barabara hizo? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI): Mheshimiwa Spika, uwezo wa Serikali unaoziwezesha Halmashauri kuweza kumudu utengenezaji wa barabara ni kuwapatia ma-*Engineer* wa Ujenzi, hatutarajii kwamba Halmashauri yenyewe ndiyo itengeneze barabara zile, kama tunavyofahamu zote Halmashauri hutumia wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, uwezo mkubwa tunaouzungumzia hapa ni wa kuwa waadilifu katika kusimamia hao makandarasi ili tuhakikishe kwamba kazi wanayopewa wanaifanya kwa ukamilifu. Siyo uwezo wa mwenyewe *Engineer* wa Wilaya kwenda kutengeneza. Lakini uwezo wa kuwasimamia Makandarasi wetu kuwa waaminifu na waadilifu. *(Makofi)*

Na. 384

Mawasiliano ya Simu Mnazi

MHE. CHARLES H. KAGONJI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imejitahidi kwa kiwango kikubwa kujibu hoja za Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2000 hasa katika eneo la mawasiliano kwa njia ya simu; na kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Mlalo wanaipongeza Serikali yao mara kwa mara kwa kazi nzuri ya kueneza simu katika Jimbo hilo:-

(a) Je, ni lini huduma hiyo itafikishwa Makao Makuu ya Tarafa ya Umba pale Mnazi hasa ikizingatiwa kwamba mawasiliano ya simu yamefika pale Mtae kilomita tisa tu kutoka Mnazi?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba Mnazi na Tarafa ya Umba kwa ujumla ina mpaka mrefu sana na nchi jirani ya Kenya, hivyo kuhitaji mawasiliano ya simu ili kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayotokea mipakani?

(c) Je, Serikali inao mpango wowote wa kuyashawishi Mashirika ya Simu za Mikononi kufikisha huduma zake Jimboni Mlalo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango kabambe wa uboreshaji wa huduma ya mawasiliano ya simu Vijijini *(Rural Automation Plan),* Makao Makuu ya Tarafa ya Umba Mnazi yatapatiwa huduma ya mawasiliano ya simu kupitia mtambo unaotumia teknolojia ya kisasa ya Simu Bila Waya *(SIWAYA).* Ukaguzi *(Survey)* na maandalizi yote yamekamilika lakini utekelezaji wake umesimama kidogo mpaka hapo wanahisa (Serikali na Mwekezaji) watakapofikia muafaka kuhusu ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba Mnazi na Tarafa ya Umba kwa ujumla ina mpaka na nchi jirani na ndiyo sababu inajitahidi ili kukamilisha zoezi la kuweka simu kwenye maeneo hayo. Aidha, Serikali inawasiliana na mashirika ya simu za mikononi ili yaweze kufikisha huduma za simu maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Katika juhudi za kufanikisha huduma za simu za mkononi katika maeneo mbalimbali nchini, Serikali inakamilisha juhudi za kumpata mshauri *(consultant)* atakayetafiti na kutoa mapendekezo ya mikakati ya uanzishaji wa mfuko maalum wa maendeleo ya huduma za mawasiliano ya simu Vijijini.

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Serikali kwa kutupatia fedha ya ujenzi wa daraja la Mkundi pamoja na kukarabati barabara ya Mkomazi, Mnazi mpaka Mng'aro. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hii kwa majibu mazuri ya matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mkutano uliopita Wizara hii ikijibu swali langu moja iliwaahidi wananchi wa pale Mwangoi, pale Viti, pale Gologolo na Manolo pamoja na Rangwi kwamba watawekewa simu za vibandani; na kwa kuwa nilipotoka nyumbani bado kazi hii ilikuwa haijaanza; je, Serikali inataka kuwapa matumaini gani wananchi wa maeneo hayo kwamba kazi hiyo itaanza lini ili wapate kufaidika? Nashukuru.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Kagonji, atakubaliana nami kwamba baada ya kufanya ziara kule Lushoto ambayo namshukuru yeye na pia napenda kuwashukuru wananchi wa Lushoto kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kunipokea na kunitembeza maeneo yote, zipo huduma mbalimbali ambazo zilikuwa ziko ndani ya uwezo wetu ambazo tumezifanya na katika maeneo yake kuna maeneo karibu sita ambayo tumepeleka huduma za simu za vibandani karibu na wananchi ambako wanazihitaji zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutofika hapo, tutaendelea kupeleka huduma hizo katika maeneo yaliyobakia. *(Makofi)*

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Mkoa wa Kagera karibu Wilaya zote zimekwishapata simu za mkononi isipokuwa Wilaya ya Biharamulo; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawahakikishiaje wananchi wa Wilaya ya Biharamulo kupata simu za mkononi kabla ya mwezi wa Agosti! Aah, mwezi Septemba? *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAWASIILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu nyingi tu za maeneo ya Kagera zimepata mawasiliano ya simu za mikononi. Lakini napenda nisite kuchukua ahadi ya mwezi huu wa Agosti kwamba zitapelekwa simu za mikononi kule Biharamulo. Ninachoweza kuahidi, ni kuendelea kuwasiliana na wenzetu wa simu za mikononi ili waone umuhimu wa kupeleka simu katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 385

Huduma ya Simu Iguguno, Kinampanda na Shelui

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kuweka simu kwenye Miji midogo ya Iguguno, Kinampanda na Shelui katika mwaka wa fedha wa 2000/2001; na kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali Bungeni mwaka 2000 ilieleza kwamba mradi huo ungechelewa kwa sababu ya makabidhiano kati ya Mwekezaji mpya na Menejimenti iliyokuwepo; na vile vile shirika lilifanya utafiti kwa ajili ya kuweka simu Nkungi, Nduguti na Ibanga:-

(a) Je, ndiyo kusema kwamba makabidhiano hayo mpaka leo hayajaisha ili wananchi wa maeneo niliyoyataja waweze kupatiwa huduma hiyo kwani wamesubiri kwa muda mrefu?

(b) Kwa kuwa sasa hivi njia rahisi ya kuweka simu ni kuweka mitambo ya simu za mikononi kama vile *Vodacom, Celtel* na kadhalika; na kwa kuwa mitambo yake inao uwezo mkubwa wa kupeleka mawasiliano umbali mkubwa; je, Serikali itasaidiaje upatikanaji wa mawasiliano hayo ambapo kwa sasa kuna wateja zaidi ya 25,000 wanaohitaji huduma hiyo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati kwa *TTCL* kuweka mtambo wa kisasa Kiomboi ili simu ziweze kufanya kazi kwa saa 24 kila siku?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* imeidhinisha matumizi yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 17 kwa ajili ya mpango wa maendeleo wa miezi sita kati ya Machi/Agosti 2003. Awamu ya pili ya mpango huo inahusisha dola za Kimarekani milioni 63. Katika awamu hii ya mpango wetu wa maendeleo, Miji midogo ya Kinampanda, Iguguno na Shelui itahusika. Hivi sasa, mipango inaandaliwa ya kupeleka mitambo ya kisasa ya mawasiliano kwenye sehemu hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Vodacom* ina mpango wa kusambaza mtandao wake wa simu kwa Wilaya zote nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Iramba. Hata hivyo, kupatikana kwa njia za mawasiliano *(Transmission Links)* kutatokana na kujenga njia zake zenyewe au kukodisha kutoka Kampuni ya *TTCL*. Kwa hiyo, uwezekano upo wa kujenga mitambo kutoka Nzega (ambapo mitambo yao ipo tayari) kupitia Igunga na kwenda Iramba. *Vodacom* imepanga kufanya tathmini ya soko mwaka 2004. Aidha, Kampuni ya *Celtel* ilishafanya tathmini ya soko mwezi Aprili, 2003 na hivi sasa matokeo yanafanyiwa kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, mtambo wa kisasa wenye kutoa njia 300 utawekwa hapo Kiomboi mwishoni mwa mwaka 2003.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa teknolojia ya sasa imebadilika kabisa na kwamba unapofunga hiyo mitambo mikubwa inayosemwa ni kupoteza fedha za wananchi maana siku hizi simu za mkononi ndiyo zina *replace* hiyo mitambo mikubwa wanayoifunga; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba itakuwa ni hasara kwa wananchi kuendelea kutoa fedha kwa njia ya kodi na kuongeza kununua mitambo hiyo ambayo imepitwa na wakati?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba teknolojia ya mawasiliano ya simu kila siku inabadilika na kila siku inaboreka. Lakini ninachotofautiana na yeye ni kwamba kila teknolojia ina umuhimu wake katika dunia hii ya sasa ya mawasiliano ya simu. Kwa kutumia *Celtel* au simu za mikononi ni kweli unaweza kuwasiliana popote na ni rahisi zaidi lakini pia simu za *TTCL* zina umuhimu wake na bado nafasi itolewe ili simu za *TTCL* ziweze kutoa huduma hizo. Kwa kufanya hivyo, hatutumii hela za wananchi vibaya. *(Makofi)*

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Kampuni ya *Vodacom* ina mpango wa kueneza simu katika Wilaya zote; je, mpango huo utaanza lini na utamalizika lini; na kwa nini *Vodacom* mpaka sasa hivi wanashindwa kupeleka simu Kisarawe ambayo ni kilomita sita tu kutoka mpakani na Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli katika jibu langu la msingi nimesema kwamba *Vodacom* ina mpango wa kusambaza simu Vijijini. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *Vodacom* kwanza ilichofanya ni kuhakikisha wanapeleka simu Makao Makuu yote na sasa wamefika katika Mikoa yote, wakimaliza hapo wanaanza katika Vijiji. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kisarawe nao watapata mawasiliano ya huduma za simu za *Vodacom. (Makofi)*

SPIKA: Kanuni zinaruhusu maswali matatu, sasa jinsia. *(Kicheko)*

MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda kuuliza swali moja ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anayo taarifa ya kwamba katika mkakati wake wa kuboresha mawasiliano kwa njia za kisasa, sisi kutoka Nansio mpaka Mrutunguru, tumelanguliwa kwa sababu tumeletewa mtambo ambao ni *absolute* haufanyi kazi na ni wa waya za kuunganisha ambao umepitwa na wakati?

SPIKA: Ni swali jipya sijui kama una maelezo? Mheshimiwa Naibu Waziri hana jibu, ni swali jipya. Kwa hiyo, tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Na. 386

Mpira wa Miguu wa Waheshimiwa Wabunge na Mabalozi

MHE. THOMAS NGAWAIYA aliuliza:-

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania walicheza Mpira wa Miguu na Waheshimiwa Mabalozi:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilipatikana kutokana na mchezo huo?

(b) Je, ni nani anayehusika kufuatilia matumizi ya fedha hizo kuhakikisha kuwa zinatumika ilivyokusudiwa; na kwamba tumejifunza nini kutokana na pambano hilo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi 13,714,900/= zilipatikana kutokana na mchezo kati ya Mabalozi na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, fedha hizo zilikusanywa na kutunzwa kwenye *Account* Maalum iliyofunguliwa na Balozi wa Uingereza Mheshimiwa Richard Clarke. Fedha hizo zimetumika kugharamia ununuzi wa tiketi za kusafiria kwa Timu yetu ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu kwa michezo ya *Special Olympic,* mashindano yaliyofanyika Ireland mwezi Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, tumejifunza mambo mengi sana kutokana na mchezo huo wa Mabalozi na Waheshimiwa Wabunge. Baadhi yake ni pamoja na:-

(i) Mchezo huo uliongeza mshikamano wa sisi Wabunge kwa upande mmoja na Wabunge na Mabalozi kwa upande mwingine. *(Makofi)*

(ii) Mchezo huo ulithibitisha kwamba michezo inajenga umoja, kudumisha amani, upendo na ushirikiano miongoni mwa Mataifa na jamii hata pale penye uhasama, ukinzani na upinzani. *(Makofi)*

(iii) Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mabalozi wapo tayari kutumia nguvu, muda na nafasi zao kufanya shughuli mbalimbali za kuchangia huduma mbalimbali za maendeleo ya jamii.

(iv) Wananchi wakiandaliwa vizuri na kuwekewa mipango mizuri wapo tayari kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo yao.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imeonyesha mafanikio katika mchezo huo wa Wabunge na Mabalozi; je, Serikali ina mpango gani wa kuleta michezo ya namna hiyo ili tuweze kuwasaidia wenzetu ambao ni walemavu au maskini zaidi?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Vyama vya Michezo kama *FAT* vina Sheria ambazo zinasaidia udikteta, vyama hivyo ni kama vile kuna Vyama vya Ushirika hata Vyama vingine vya Siasa vina udikteta ambao hairuhusu Serikali kuingilia humo ndani na wakati huo huo inaleta madhara kwa wananchi na Serikali kwa ujumla; je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza labda *Regulatory Board* au kupitia upya Sheria hizo za Vyama hivyo ili kuondoa tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa kugundua kwamba katika mchezo ule kulikuwa na mafanikio makubwa, sio tu ya kuingiza pesa za kuwasaidia hawa watu wenye ulemavu lakini vile vile pesa zile zilichangia watu hao wenye ulemavu kutuletea jumla ya medali 18, nne zikiwa za dhahabu, 11 za fedha, tatu za shaba na kuchukua nafasi ya pili duniani kati ya washiriki 7,000 kutoka nchi 160 na nchi za Afrika zilizoshiriki zikiwa ni 24. Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Katiba ama Kanuni zenye mwekeleo wa udikteta ndani ya michezo. Serikali sasa hivi inaandaa kutengeneza Sheria ya Maendeleo ya Michezo ambayo itaipa nguvu sheria ya BMT badala ya sasa ambapo sheria ya BMT ina meno ya nailoni. Napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria hiyo itakapoletwa Bungeni basi tuichangie vizuri, tuipitishe ili meno haya ya *nylon* yageuke kuwa meno ya kweli kweli. *(Makofi)*

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulicheza mechi hii ikaleta mafanikio na faraja kubwa na kulitangaza Bunge kuwa linaweza likachangia. Lakini wakati huo huo tulipata taabu sana katika mambo haya ya maandalizi na motisha ilikuwa ni ndogo sana; je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaonaje Bunge hivi sasa liweze kujiandaa kuipatia Timu ya Bunge kwenda mahala kama ni motisha ili kuhakikisha kuwa tunaweza tukachangia katika sehemu nyingine? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli siyo tu motisha lakini itakuwa ni kuwaandaa vizuri Waheshimiwa Wabunge kwa kuwatafutia safari ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuthibitishie Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, kwamba ombi hili nitalifikisha kwa Mheshimiwa Spika mwenye timu yake na nitalifikisha kwa Mheshimiwa Waziri

Mkuu ambaye ndiye mlezi wa timu hiyo. Nitafanya kazi hiyo leo mara baada ya Kikao hiki cha Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Na maombi hayo yakifikishwa yatafanyiwa kazi mara moja. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 387

Kukua kwa Ukusanyaji Mapato

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imejitahidi sana kukusanya mapato hata kurudisha hadhi ya Serikali inavyotakiwa kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma:-

(a) Je, mkulima anafaidikaje na Pato hilo la Serikali?

(b) Je, Serikali inaligawaje Pato lake hilo kwa jamii ya Watanzania kwa uwiano wa Taifa zima?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kumekuwepo na ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato katika Serikali ya Awamu ya Tatu. Hii imetokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara ya Fedha kupitia Mamlaka ya Mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha sera na mfumo wa kodi, utawala wa kodi, uwazi na uwajibikaji na kuboresha mbinu za kuziba mianya ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo katika Pato la Taifa, imekuwa ikitoa kipaumbele katika mgao wa fedha kwa sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Serikali iliongeza mgao wa fedha kwa sekta ya kilimo kwa kiasi cha shilingi bilioni 40.022, ikiwa ni ongezeko la asilimia 57.8. Mgao halisi wa fedha ulikuwa ni shilingi bilioni 70.5 ukilinganisha na shilingi bilioni 30.478 mwaka 2001/2002.

(b) Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mapato kumeiwezesha Serikali kuboresha huduma za jamii na za kiuchumi kama vile elimu hasa ya msingi, afya, barabara, maji, vita dhidi ya Ukimwi na utawala bora. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa maeneo yote hayo niliyoyataja yana mchango mkubwa katika sekta ya kilimo, hivyo basi uboreshaji wa huduma za jamii na uchumi, hasa Vijijini unachochea kwa namna moja au nyingine katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa mkulima katika uzalishaji wa mazao. Hizo ni baadhi tu ya faida nyingi azipatazo mkulima kutokana na ongezeko la Pato la Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya mgao wa mapato yake kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele katika kukabiliana na umaskini na pia katika maeneo yanayochochea ukuaji wa Pato la Taifa na hatimaye kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi walio wengi. Kwa hivi sasa mgao wa mapato ya Serikali hutegemea uchambuzi wa wadau mbalimbali. Wadau hao hutoa mchango wao kwa kupitia Kamati za Kisekta *(Sector Working Groups)* chini ya Mpango wa *Public Expenditure Review (PER).* Washiriki wa Kamati za Kisekta ni pamoja na Wizara husika, wahisani, Mashirika ya Fedha ya Kimataifa pamoja na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali yaani *NGOs*. Upana huu wa washiriki huhakikisha kwamba maslahi ya Wizara/Sekta na Mikoa yanazingatiwa katika ugawaji wa Pato la Taifa.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha zetu za maendeleo zinapotolewa hutofautiana sana Mkoa hadi Mkoa; na hii inaonyesha wazi kwamba ukiangalia mahesabu hayo unatia mashaka kwamba kuna baadhi ya Mikoa hupendelewa kwa mfano mwaka huu wapo waliopewa shilingi bilioni tano, shilingi bilioni tatu, wengine wakapewa shilingi milioni nne na wengine shilingi milioni mia tatu; je, ugawaji huu unatumia vigezo gani ili kuondoa mashaka yanayotolewa na watu hawa wanaosimamia, ili tuweze kugawana pato sawa sawa kwa kila mmoja? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimesema kwamba kwa hivi sasa mgao wa mapato ya Serikali hutegemea uchambuzi wa wadau mbalimbali. Wadau hao hutoa mchango wao kupitia Kamati za Kisekta chini ya Mpango wa *Public Expenditure Review*. Washiriki wa Kamati za Kisekta ni pamoja na Wizara husika ama Mikoa husika, wahisani, mashirika ya fedha ya Kimataifa pamoja na *NGOs*. Kwa hiyo, upana huu wa washiriki uhakikishe kwamba maslahi ya Wizara, Sekta ama Mikoa inazingatiwa katika ugawaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini mfano mzuri wa kuonyesha usawa katika ugawaji wa mapato ya Taifa ni kama ilivyofanyika katika Sekta mbili yaani Elimu na Afya. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba, mgao wa fedha katika Sekta ya Elimu umekuwa wa usawa kuzingatia mahitaji ya elimu katika Mikoa na Wilaya mbalimbali. Kwa mfano, katika mwaka 2002 Mkoa wa Shinyanga ulikuwa wa kwanza katika kupata fedha za elimu kiasi cha shilingi bilioni 2.2, hakuna Mkoa mwingine uliopata fedha kiasi hiki. Hii inaonyesha mahitaji makubwa ya elimu katika Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, katika afya Mkoa wa Shinyanga ulikuwa wa pili baada ya Mkoa wa Mbeya kwa kupata shilingi 874,819,700/=.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mgao wa Pato la Taifa haupendelei na unazingatia kwa kweli mahitaji katika sekta mbalimbali hasa sekta zinazopewa kipaumbele katika kuondoa umaskini.

Na. 388

Karafuu Zilizoingizwa kwa Njia ya Panya

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD (k.n.y MHE. HAROUB SAID MASOUD) aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wa *TRA* nchini siku hadi siku wanajipatia sifa kem kem kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo kupitia madukani na kuwapiga faini wafanyabiashara wanaokutwa na bidhaa ambazo zinatuhumiwa kuingizwa nchini kwa njia ya panya:-

(a) Je, katika pekuzi hizo *TRA* imewahi hata siku moja kukuta karafuu ambazo zimeingizwa kwa njia za panya kutoka Zanzibar?

(b) Je, kama jawabu ni ndiyo, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wafanyabiashara hao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, zao la Karafuu linalimwa katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Zao hili pia limeanza kupata umaarufu katika Mkoa wa Tanga hasa sehemu za Maramba.

Mheshimiwa Spika, zao la karafuu ni zao sawa na mazao mengine ya biashara yanayolimwa na kuuzwa nje ya nchi *(Traditional Cash Crops)* ambayo hayatozwi kodi ya mazao ya nje *(Export Tax)*. Kwa vile zao hili linalimwa hapa Tanzania Bara na pia kuingizwa nchini toka Zanzibar likiwa ghafi *(unprocessed),* halitozwi kodi ya aina yoyote. Hata hivyo, karafuu iliyosindikwa *(processed)* inalipiwa kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kama yalivyo mazao mengine yaliyosindikwa yanayouzwa ndani ya nchi. Kwa vile hakuna kizuizi wala ushuru wa forodha kwenye Karafuu inayoingizwa Tanzania Bara toka Zanzibar, wafanyabiashara hawaingizi Karafuu kwa njia za panya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyotangalia kuyatoa, Serikali haina habari kama Mamlaka ya Mapato *(TRA)* haijawahi kufanya pekuzi na kukuta karafuu ambazo zimeingia kwa njia za panya na kwa mantiki hiyo hakuna takwimu zozote kufuatana na uuzaji wa karafuu. Aidha, hakuna wafanyabiashara waliokamatwa au hatua zilizokwisha chukuliwa dhidi ya wafanyabiashara wa karafuu wanaopitia njia za panya.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jirani zetu wa Kenya wanajisifu sana kwa kuuza Karafuu nyingi nje wakati wao hawazalishi Karafuu; je, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inatusaidia vipi katika kudhibiti hizi njia za panya zinazokwenda Kenya? *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la magendo ya Karafuu limejadiliwa mara nyingi sana kwenye Vikao vya Baraza la Mawaziri la Afrika ya Mashariki na kuna maelewano kwamba Serikali ya Kenya itajitahidi kushirikiana na Serikali ya Tanzania ili kuona namna ya kudhibiti magendo ya Karafuu kutoka Zanzibar kupitia Baharini kwenda Kenya. Kwa hiyo, kuna makubaliano hayo na tumaini langu ni kwamba hatua kwa hatua tutaweza kudhibiti magendo hayo ya karafuu. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wake vile vile umekwisha.

Kabla hatujaendelea kuna matangazo ya Vikao vya leo, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wake wakutane Saa 7.00 mchana ukumbi Na. 84. Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anaomba Wajumbe wake wakutane leo Saa 5.00 asubuhi hii chumba Na. 56. Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Kwaangw', naye anaomba Wajumbe wake wakutane Saa 5.00 asubuhi hii chumba Na. 58. Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, anaomba Wajumbe wake wakutane Saa 7.00 mchana chumba Na. 81. Mwisho, Kamati ya Kanuni za Bunge, Mwenyekiti wake anaitisha Kikao Saa 5.00 asubuhi hii. Mwisho wa vikao.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye *Order Paper* kuna Muswada wa Fedha *(Finance Bill).* Huu tumeugawa mara mbili, mara ya kwanza kabisa halafu baada ya Muswada kwenda kwenye Kamati na kujadiliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yamefanyika mabadiliko makubwa.

Kwa hiyo, Muswada ukachapishwa upya pamoja na hayo mabadiliko, nao tumeishaugawa, tuligawa kwenye *pigeonhole* lakini kama kuna Mheshimiwa Mbunge hana nakala yake zinapatikana nakala za ziada hapa mezani.

Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper*.

MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2003 *(The Appropriation Bill, 2003)*

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja tisini na nane, milioni mia sita na tano mia tano na sabini

na sita elfu na mia tisa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itakayotelekezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo sasa usomwe mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004, nilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja tisini na nane, milioni mia sita na tano mia tano na sabini na sita elfu na mia tisa kwa mwaka 2003/2004 kwa Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni mia nane na saba, milioni mia nne na arobaini elfu, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni moja, milioni mia tatu tisini na moja, mia moja na sitina na tano elfu na jumla shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja tisini na nane, milioni mia sita na tano, mia tano na sabini na sita elfu na mia tisa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekwishajadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha Makadirio ya Wizara zao. Madhumuni wa Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Serikali ya mwaka 2003/2004 ya jumla ya shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja tisini na nane, milioni mia sita na tano, mia tano na sabini na sita elfu na mia tisa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na ya Miradi ya Maendeleo yaliyokubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, waliochambua Muswada huu atoe maoni ya Kamati. Aah, samahani, hii ni *Appropriation Bill.*

Waheshimiwa Wabunge Muswada wa *Appropriation* haupiti kwenye zile hatua nyingine za Miswada ya kawaida. Unajadiliwa moja kwa moja na wala hautakwenda kwenye Kamati ya Bunge Zima. Sasa Muswada umeongwa mkono, namwita Mheshimiwa Paschal Degera, aah, sio huu alioomba kuchangia, hakuna aliyeomba kuchangia Muswada huu na hakuna anayesimama kutaka kuuchangia basi mtoa hoja huna jambo la kujibu. Kwa hiyo, nitawahoji kama mnakubali Muswada usomwe Mara ya Pili.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2003 *(The Appropriation Bill, 2003)*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja tisini na nane, milioni mia sita na tano, mia tano na sabini na sita elfu na mia tisa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itakayotelekezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Fedha kwa Mwaka 2000/2001

(The Supplementary Appropriation for the Financial Year 2000/2001) Bill 2003

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa kuhalalisha Matumizi ya Ziada ya jumla ya shilingi bilioni nne, kumi na tisa milioni, mia moja themanini elfu, mia moja arobaini na tano kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaliyofanyika mwaka wa fedha 2000/2001 kwa ajili hiyo sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kudhibiti matumizi katika vyombo vyake na matokeo ya hatua hizo yameanza kudhihirika kwa kupungua viwango vya matumizi zaidi nje ya Bajeti. Hata hivyo, kwa mwaka 2000/2001 kama Waheshimiwa Wabunge watakavyoona kwenye hati husika, matumizi ya ziada yamesababishwa hasa na kasoro za kihasibu ambazo zimerekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi imechambua kwa undani Matumizi haya ya Ziada. Madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu kuhalalisha Matumizi zaidi ya shilingi bilioni nne, kumi na tisa milioni, mia moja themanini elfu, mia moja arobaini na tano kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mwaka wa fedha 2000/2001.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naomba kuelekezwa kuhusu utaratibu, niliona kuna maoni ya Kamati halafu Kambi ya Upinzani.

SPIKA: Utaratibu wa *Supplementary Appropriation* ni sawasawa na ule wa *Appropriation,* Muswada hauendi kwenye Kamati wala haupitii kwenye Kamati ya Bunge Zima, iko kwenye Kanuni lakini nadhani mnaamini maneno yangu. Lakini kama unataka kuchangia kama mchangiaji wa kawaida endelea tu. *(Kicheko)*

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako tu ni kwamba Kamati ya Fedha na Uchumi, ilijadili Muswada huu na tulitegemea Kamati italeta maoni yake lakini kwa sababu tunakuheshimu maamuzi yako....

SPIKA: Nadhani ulipelekwa kwenye Kamati kwa makosa tu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Basi nasema tunaheshimu maamuzi yako, naomba kusema mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwamba kuna *Access Vote* inayohitajika karibu ya shilingi bilioni nne sehemu kubwa hasa ni kwa ajili ya ni *Vote 34,* Mambo ya Nje peke yake imechukua kama shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, ukichukua matumizi Wizara hii kwa mwaka wa 2000/2001 Addis-Ababa peke yake ilikuwa imetengewa kama shilingi 242,000,000/= lakini ukitazama *Access Vote* inakuja shilingi 242,000,000/= vile vile. Sasa unaona kuna matumizi ya siyo *Access Vote* kwa maana ya matumizi ya dharura yaliyotokea lakini ni matumizi ya mwaka mzima yameombwa tena kama *Access Vote.*

Mheshimiwa Spika, hili linatupa wasiwasi kwamba je, Bajeti ilifanywa sawasawa kiasi cha kwamba *Access Vote* isiweze kukabiliana na *actual* Bajeti. Wasiwasi mmoja tulionao ni kwamba inaelekea ama pesa zinazopelekwa *Foreign Affairs* haziwasilishwi kwenye Ubalozi kama inavyotakiwa na kwa maana hiyo Balozi zinapata pesa kasoro katika kipindi cha mwaka na hatimaye wana accumulate matatizo na baadaye kuiomba Wizara iwasilishe maombi ya ziada.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Kwanza, ufanyike utafiti wa kina juu ya matumizi ya Balozi zetu. Inaelekea kuna ubadhilifu mkubwa sana wa matumizi katika Balozi zetu. Kwa mfano Ubalozi wa Bonn uliomba pesa kwa ajili ya kununua gari lakini fedha hizo wakazitumia kwa shughuli nyingine bila ya idhini ya Bunge lako Tukufu baadaye wakaendelea tena kuomba pesa kwa ajili ya kununua gari. Sasa huu utaratibu ambao mtu anaweza kufanya *re-allocation* anavyotaka yeye na utaratibu wa kupelekewa fedha za matumizi mengine zikatumika kwa ajili ya matumizi mengine nafikiri sio utaratibu sahihi ulioidhinishwa na Bunge hili. Bunge lako linapitisha Matumizi vifungu kwa vifungu tungetegemea na wengine wangetumia fedha hizo kwa mafungu hayo hayo bila kubadilisha au kubadilisha baada ya kupata idhini ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, inaelekea utaratibu huu wa kupitisha fedha *Foreign Affairs* Balozi zinapata matatizo. Kwa hiyo, kama vile tulivyoshauri Uhamiaji kuwa na Fungu lake peke yake na kwa kuwa kila Balozi zimetengewa bajeti yake maalum tunashauri kwamba fedha zao zitoke moja kwa moja na mafungu yao yaende kwa Balozi zinazohusika kusiwe na upungufu katikati, kusiwe na mtu katikati anawapunguzia matumizi yao. Nafikiri hili nalo litatuondolea matatizo na tutaweza kuzibana Balozi zetu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, ni ubadhilifu katika Balozi zenyewe. Kunahitajika kuwekwa mipaka juu ya *authority* inayoruhusu matumizi katika Ofisi za Balozi. Inaelekea hakuna *authority* maalum Balozi anavyoamua ndivyo Mhasibu Mkuu aliyeko pale anafuata na hii kuna hatari. Inawezekana kuna shughuli fulani inataka kufanyika basi Balozi akatoa tu amri. Nafikiri *Financial Regulations* kwenye Balozi lazima ziheshimike sana vinginevyo matumizi ya ovyo ovyo na ununuaji wa vifaa hasa samani ambazo hazilingani na hadhi za Kibalozi yanatokea na hasa kwenye nyumba za watumishi wa Ubalozi.

Kwa hiyo, nashauri kuwe na *standardization* ya vifaa vinavyotumika katika Balozi zetu ili utaratibu wa Serikali wa kununua vifaa uwe unaeleweka sio uende kwenye Ubalozi huu unakuta kitu tofauti na sehemu nyingine. Nalo hilo linachangia sana katika ubadhilifu wa matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu wanasema maji yaliyokwishamwagika hayazoleki, Bunge lako Tukufu halipendi sana kuwa na *Access Vote* kwa kiasi hiki kwanza tunasikitika kwa nini Wizara imechelewa sana mpaka inaileta leo 2003. Tunahitaji kupata mapendekezo ya *Access Vote* yakitokea kwenye Kamati za Bunge kwa wakati unaofaa na jambo hilo lifanyike kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Spika, kukaa muda mrefu kama huu mpaka leo 2003 ndio tunaletewa sio utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kusema kwamba nakubali na naunga mkono Muswada huu kwamba tuidhinishe hayo matumizi yaliyokwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda nisaidiwe kidogo kuelewa nifutiwe ujinga kwenye masuala haya, kwanza hapa tunaambiwa tunatakiwa tu-*appropriate* tena pesa ambazo kwa kweli zilishatumika sasa sijui kama *technically* ni kitu ambacho kinawezekana, mimi sio Mhasibu na anasema kwamba *appropriation* yenyewe iwe kwenye *Act* ile ya mwaka 2000/2001.

Mimi nafikiria sijui wataalam watasemaje, si vema tukafanya *amendment* ya ile *Bill* ya wakati ule kwa sababu kama tunakuwa *confined* kwamba hii iende pamoja na ile na kwa kweli ku-*appropriate* kitu ambacho tayari kilishatumika *I think* sio matumizi mazuri ya uelewa ambao mimi nafikiri nilitakiwa

niamini kwamba nauelewa. Nilikuwa nafikiri kama Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia kwamba ni bora ile *Bill* ambayo ili-*appropriate* pesa katika mwaka ule wa pesa ikafanyiwa *amendment.*

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuwa nataka nisaidiwe kwa kweli ni muda mrefu umepita tangu mwaka 2003 tumekwishaingia kwenye mwaka 2003/2004 ni *two years now* kwa nini? Maana yake pale Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha hoja hii amesema kwa mapungufu yaliyotokana na Wahasibu wa Serikali. Hii inaonyesha tuna matatizo makubwa sana kama kitu cha namna hiyo kwanza kinaweza kikachelewa namna hii halafu kinatokea ati tu kwa sababu kulikuwa na matatizo ya Wahasibu wenyewe.

Mimi nilitaka niamini kwamba kulikuwa na matatizo yaliyo-*prompt* hizi pesa zitumike na sio matatizo ya Wahasibu, kama nilielewa vizuri. Sasa hebu naomba nisaidiwe hizi pesa ziliombwa kwa sababu matatizo yalizuka nje ya wakati ambao Bajeti ilikuwa inatengenezwa au ni kweli kabisa ni uzembe wa Wahasibu na inawezekana huu uzembe ulisababishwa na Wahasibu wenyewe baada ya kuwa Wizara zimewakilisha mahitaji yao vizuri. Hilo nalo nafikiri ni la msingi sana tulielewe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nipate tu jibu la nadharia kwa sababu ninachokisema hapa sasa pia ni cha nadharia. Kwa mfano, pesa hizi zimekwishatumika nafikiri wanaweza kuonyesha *evidence* ya matumizi hayo, lakini sasa wanaomba tuidhinishe kwamba wao wametoa pesa hizo huko. Kwa mfano, nilishasema mwanzo kabisa naunga mkono, nataka nielewe tukikataa itakuwaje? Hilo naona ni la msingi sana kwa sababu unaweza uka-*sanction* vitu ambavyo baadaye vikaja vikakuweka kwenye matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hii nataka niunganishe na *Clause* Na.4 katika *Bill* hii ambayo inasema Waziri *may at any time or times not latter than* mwisho wa mwaka ule wa pesa kwa maana hii ni mwaka 2001 aazime pesa, napenda nifahamu kwa sababu hapa imesema tu kijumla, hivi kuna *limits I would like* kwa mfano *to believe* kwamba hii pesa bilioni nne ni *percent* fulani ya Bajeti ambayo tulikuwa tumepanga wakati ule.

Sasa nafahamu mnapobajeti huwa mnabajeti kwa mfano, *you have your figure 100%* halafu unakaa nyuma tena unasema *assume* una *10% less,* nafikiri ndio mnavyofanya hivyo maana yake utaalam wa *budgeting* na mimi ninaanza kuupata. Mimi ni *Engineer.* Sasa hii *10% less budgeting* naamini *this four billion I am not sure* na *figure* ya Bajeti ya mwaka ule *less than ten percent* ya Bajeti ile ya mwaka ule, *I believe so,* sina uhakika.

Sasa nataka niseme *if budget* ina-*allow* unaweza kuwa na *10% less scenario* na ukaona jinsi ambavyo unaweza kuogolea kwenye maji haya kwa nini hamku-*resort* kwenye hiyo *scenario* ya kwamba *now* kwa sababu tumekuwa na *excessive need* ya pesa tubadilishe kwa sababu tuna ile *scenario* ya pili tuende kwenye *scenario* ya *10% less* ili tuweze kuishi na ile ile Bajeti. Nataka nisisitize tena tusijifunze kukabidhi madeni haya kwa wajukuu zetu sio kitu kizuri. Nilitaka kama Mheshimiwa Waziri atakuwa na nafasi anisaidie hizi pesa basi zilikwenda kufanya nini? Mimi sitaki kuingilia sana huko lakini nataka niamini kwamba kulikuwa na sababu ya msingi sana ya kufanya urudi tena kwenda kuchokonoa bajeti ambayo ulishaipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri maswali yangu yameeleweka na kwa nia njema tu naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuelewa na nafikiri wengi tutafurahi kupata taarifa hiyo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. NJELU E.M. KASAKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba tuidhinishe alichoomba zaidi ya shilingi bilioni nne kwa kweli kwa sasa hatuna uchaguzi itabidi tuidhinishe kwa sababu fedha zilishatumika. Lakini katika maoni yangu nafikiri utaratibu huu wa kutumia fedha za Serikali bila idhini ya Bunge ungeachwa kwa sababu Bunge linakutana hapa mara nne kwa mwaka hakuna sababu yoyote ya Serikali kutoliarifu Bunge kwamba kuna matumizi ya dharura. Ingekuwa ni jambo jema kwa Serikali kama kuna jambo la dharura wametumia fedha kikao cha Bunge kinachofuata basi kinajulishwa

kuwa fedha zimetumika lakini kungoja miaka miwili, mitatu hakuna sababu ya msingi na tunaona kwa kweli ni kukiuka kanuni pamoja na Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, fedha hizi nyingi zilikwenda kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwenye *Vote* za Kibalozi na imeelezwa kwamba hali ya Balozi zetu ni mbaya kwa hiyo ilibidi fedha zipatikane zikatumike huko. Nakubaliana na umuhimu wa kuwapelekea Mabalozi wetu fedha ili Ofisi zao na mazingira yao wanaomoishi na wanamofanyia kazi yaweze kuwa mazuri. Lakini inajulikana wazi kwamba hali mbaya ya Balozi zetu sio jambo geni wala sio jambo la dhararu, inajulikana kabisa kwamba Balozi zetu zimo katika hali mbaya, hawana majengo mazuri, hata nyumba za kuishi Mabalozi wenyewe sio nzuri na baadhi ya Balozi zetu hata magari ya kutumia hawana.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanajulikana na tunatazamia yangekuwa yameingizwa kwenye Bajeti ya kawaida na ikapitishwa ndani ya Bunge hili. Lakini kuja na matumizi ya dhararu kwa madai kwamba ilibidi tupeleke kwenye Balozi zetu bila kuliarifu Bunge tunafikiri sio jambo la busara na tunafikiria kwamba utaratibu wa kuliarifu Bunge au kuliomba Bunge liidhinishe uwe unatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, fedha ambazo zilitumiwa na Mikoa kwa hii hali ambayo inaitwa ni ya dharura tulipokuwa tunaangalia tuligundua kwamba katika Mkoa mmojawapo walitumia fedha kununua *uniform* za wafanyakazi. Sasa *uniform* za wafanyakazi haliwezi kuwa jambo la dharura hata siku moja. Kwa hiyo, tunafikiri hizi fedha za ziada utaratibu ungeachwa wawe wanakuja hapa kuomba idhini ya Bunge na kama ni jambo la dhararu sana tunafikiri kwamba Kamati ya Fedha na Uchumi iitwe iarifiwe kwamba kuna matumizi ya dhararu na kama fedha italazimika zitoke kabla basi iarifiwe kwamba wiki au mwezi uliopita tulitoa fedha kiasi fulani kwa dharura hii na hii na sisi tutaliarifu Bunge kupitia Kamati yake ya Kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, tuna utaratibu wa *Cash Budget* ambao umeanza muda mrefu uliopita, ina maana kwamba unatumia kile ulichonacho sasa unapokuja na *access* ya *four billion* katika matumizi ya *Cash Budget* na wakati ule ule tumearifiwa baadhi ya miradi haikupata fedha kwa sababu fedha zilizokusanywa hazikutosha hizi za *access* ya *four billion* zilitoka wapi? Hayo ni baadhi ya mambo tungetazamia Serikali itueleze kwamba pamoja na kwamba hatukuweza kuzipatia fedha Idara fulani fulani lakini *access cash* ilipatikana kutoka maeneo haya na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa ambao umeuanzisha wa hizi *Portfolio Committees* umerahisisha mambo kwa Serikali kuzitumia Kamati hizo wakati wote wanapokuwa na mahitaji. Hawahitaji kusubiri mpaka Bunge litakapokutana au mpaka Mkaguzi Mkuu wa Serikali atakapokuja kukagua. Kwa sababu tulicholetewa sasa inasema kwamba Mkaguzi alishakagua lakini matumizi haya kupata kibali cha Bunge hawahitaji Mkaguzi Mkuu wa Serikali akague kwanza mahesabu hayo ndipo waweze kuja kwenye Bunge wanaweza kuja hata kabla ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali hajafanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa leo kwa kweli hatuwezi kulikataa ombi la Mheshimiwa Waziri tunalikubali na tutamruhusu atumie fedha hizi, naomba Bunge likubali lakini kwa siku zijazo utaratibu huu ambao tunauzungumza hapa sasa tutaomba uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nina mambo machache tu katika huu utaratibu ambao tumeuzoea wa muda mrefu. Wakati uliponiteua katika *Public Accounts Committee* nilipoanza kuwa Mbunge katika miaka ya 1990, *Access Vote* zilikuwa nyingi sana *Accounting Officers* walitumia ovyo ovyo wakati ule watu walikuwa wanapewa fedha na wanatumia wanavyotaka.

Nimeshukuru sana katika *experience* za *Access Vote* ukilinganisha kuanzia miaka ya 1989 mpaka 2000 kwa kweli hii *four billion* ni karibu *one third* ambapo Serikali imefuta kiwango kimoja kibovu cha matumizi na kuendelea kuwa *as a good quality control.* Kwa hiyo, napongeza Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kwa kuweka hatua hizi za *Cash Budget* ambayo inapunguza kiwango cha *Access Vote.*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia mafanikio haya ya *Cash Budget* na nilionana na *Controller and Auditor General* nje huko nilipotoka hapa nikamuuliza kwa nini imetokea *Access Vote* ya *four billion* pamoja na kwamba ni ndogo ninaisifu Serikali na kwa utaratibu wa *Cash Budget* unatumia ulichonacho mkononi, mdomoni na unachokiona machoni na taratibu ni kwamba unakusanya halafu unaanza kutoa mgao. Akaniambia *Access Vote* imetokea katika Ofisi za Ubalozi.

Mheshimiwa Spika, nikamwuliza Ofisi za Ubalozi wanazipata wapi wanakopa au wanapewa na wafadhili halafu Serikali yetu inalipa? Akasema hapana wale wanatumia yale maduhuli ambayo wanayapokea kule wakiyapokea wanasema kwamba tumepokea kwa mfano milioni mia nane wanasema jamani tumekwama huku kwa hiyo, katika hizi tunatumia milioni mia nne, tuwaambia tumieni halafu tutawapelekeeni. Nikamwuliza sasa hesabu zinakosana wapi katika mtandano wa sasa hivi, unaweza kuijua dunia kwa kutumia ncha ya vidole vyako chini ya teknolojia mpya ya utandawazi, website ama katika Hazina hatuzitumii hizi?

Mheshimiwa Spika, mimi nilisimama tu kuwaambia watu wa Hazina wazinduke kama mlivyozinduka katika utaratibu tuliopitisha Bajeti yetu zinduka, uchumi uko ndani ya ncha ya vidole vyetu sasa hivi sio lazima uende kule wakuandikie makaratasi wakuletee dakika moja tu unajua *www.tanzania.com* unapata kila kitu pale. Kwa utaratibu huu nilitegemea kwamba huenda tungeletewa *Access Vote* za mwaka 2000/2001, 2001/2002, 2002/2003 au kwa kanuni inasema kwa kikao kimoja ni lazima kutoa *Access Vote* moja tu? Kwa sababu hii imepita kwenye arobaini hata hitma imepita nadhani hii ni kijungu, watu wanakwenda kuzuru kwenye makaburi vitu vimeshatumika *(Access Vote)* tayari kwa sababu sasa hivi ni miaka minne kwa hiyo kumwambia mtu msiba huu kwa kweli mtu hashtuki Mwenyezi Mungu alishaweka fedha hizi mahali pema peponi na zilishazikwa, kijungu kilishasomwa, ni karibu miaka minne. Kwa hiyo, naomba Wizara tuzinduke na utaratibu huu kwamba tutoe *Access Vote* kwa kipindi muafaka ili kusudi ili kutoa ushauri vizuri. Hii kitaalam ni *posthumous,* ni taratibu ya kufukua maiti iliyozikwa 2000/2001.

Mhehsimiwa Spika, *otherwise* nashukuru sana kwa utaratibu huu ambao Mabalozi kwa mfano, aidha, zimeuliza kitu kimoja kwenye utaratibu, kama Mabalozi walikuwa na matatizo kama haya, kwa nini katika *Vote 34* tulipitisha kifungu kwa kifungu. Mwaka 2001/2002, tulikadiria bilioni 20 lakini mwaka 2002/2003 tulikadiria bilioni 37, *which means* tuligundua matatizo yao. Lakini mwaka huu tulitoa bilioni 32. Kwa hiyo, tumepunguza bilioni karibu tano. Kama tatizo hili linatokea kwenye ofisi za Mabalozi kwa nini tumepunguza au idadi ya Mabalozi wamepungua?

Sasa kama hesabu ile na matumizi vile vile Mabalozi wakiiona kwa kuwa mazoea wataendelea kutumia ile vile vile, *other wise Controler and Auditor General* alifanya kazi nzuri kutuelimisha vipengele kwa vipengele. Sasa inabidi kifungu kwa kifungu.Wale wanatumia kipengele kwa kipengele wakati Bunge linapitisha kifungu kwa kifungu.

Kwa hiyo, tunaomba utaratibu huu uwe *up to date* badala ya kulilia historia ya miaka minne sasa tuletewe *Cash Budget Vote* kwa wakati ambapo ni muafaka ili tuweze kuelewa. Najua hili huwezi kulitabiri kwamba wapewe *vote* kiasi gani, lakini mambo mengine siyo ya dharura ni mambo ya matumizi ya kawaida kuna *stationary* na vitu vingine. Kwa hiyo, nadhani itazidi kupungua kadri Wizara ya Fedha itakapozinduka. Nimesema zinduka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Fedha imezinduka kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Semindu Pawa. Tumezinduka kwa njia mbili. Moja, tumeleta *Public Finance Act, 2001.* Sheria ile imeanza kutumika na jinsi muda utakavyokwenda mambo haya yaliyojitokeza mwaka 2000 hayatatokea tena na yakitokea itakuwa ni kwa bahati mbaya sana. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara ya Fedha imezinduka kwa kutambua kwamba katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje yapo matatizo makubwa sana ya ufinyu wa fedha. Ndiyo maana kutokana na kuzinduka huko mwaka huu wa Bajeti hii ya 2003/2004 tumeiweka Wizara hii kwenye kundi maalum la

kushughulikiwa kibajeti. Wizara ya Mambo ya Nje ipo kwenye kundi moja na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ulinzi. Ni Wizara zinazoitwa Wizara za NU na Wizara za NU mwaka huu kama vile mlivyogundua na Waziri mwenyewe wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, amesema hapa alipokuwa akiwasilisha hotuba, Wizara hizi zimepewa upendeleo maalum kwa Bajeti hii. Mwisho wa mwaka jana na mapema mwaka huu nilipeleka timu maalum Ulaya na Amerika kutoka Wizara ya Fedha kwenda kujithibitishia yenyewe timu hiyo, kulikoni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, huko kwenye Balozi. Mhasibu Mkuu wa Serikali mwenyewe aliongoza timu hiyo. Mhasibu Mkuu siyo Mkaguzi Mkuu akifuatana na Maofisa wa Ukaguzi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Hazina kwenyewe kujionea wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mambo waliyojinea kutokana na upungufu huo wa fedha wa miaka mingi ni kama alivyosema Mheshimiwa Njelu Kasaka, kuna Balozi yaani matatizo yale hayafai kusema hapa. Niaminini tu ninavyosema, ni kweli matatizo yale hayafai kusema hapa kwa sababu siyo vizuri yaingie kwenye *Hansard.* Lakini naweza nikasema tu kwamba kwa Kiingereza ungeweza kusema hali ya Balozi zetu ni *pathetic* yaani ya kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekwishakubaliana na Waziri wa Mambo ya Nje na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa kwamba Wizara hii itaendelea kupewa upendeleo maalum kidogo kidogo mpaka iweze kunyanyua kiwango chake, hadhi yake kufikia kiwango na hadhi inayokubalika Kimataifa na kwenye Bajeti ya mwaka huu tumeanza na tutaendelea hivyo. Kwa hiyo, nakubali lazima tuzinduke na ndivyo tulivyoanza kuzinduka.

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika Wizara hiyo ni kuangalia upya kada ya Waweka Hesabu (Wahasibu) kwenye Balozi hizo. Wakati tulipopunguza wafanyakazi kwenye Serikali walipunguzwa Wahasibu wa Balozi zetu nje, kwa hiyo Balozi zikabaki na Wahasibu ambao hawakuwa wamesomea sawasawa. Ni karani wa aina fulani ndiye huyo Mhasibu, ndiye huyo wa *Passport, Visa* na mambo mengine ya utawala.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje tumekubaliana hatua kwa hatua kurejesha tena Wahasibu kwenye Balozi zetu ili wawepo watu ambao wanafahamu wanachofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo niseme tu kwamba hesabu hizi kweli ni za 2001/2002 na zimechelewa. Lazima kama mtu ninayependa Utawala Bora kwenye eneo hili niombe radhi kwamba hali hii siyo nzuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii hairidhishi kwamba mambo ya 2000 yanakuja hapa leo. Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri kwamba hata kama inatokea dharura ya namna gani ni vizuri hiyo dharura isemwe hapa wakati tunaitekeleza au mara baada ya kutekeleza ili angalau Wabunge wajue kinachoendelea kwamba kuna mdudu ameingia kwenye mambo yetu tunamshughulikia lakini anaweza akavuka viwango vya Wizara fulani. Jambo hilo ni zuri na wala halina gharama nitalizingatia kwa siku zijazo na nadhani mwaka huu nitaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zilizogawanywa kwenye Balozi zetu kama alivyosema Mheshimiwa Semindu Pawa, ni kweli ni fedha ambazo hazikutoka Dar es Salaam kwenda kule ni fedha ambazo walikuwa nazo wao wenyewe, fedha zilizotokana na *visa* na mauzo ya *passport* na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, kwa namna yao wakaomba kwa sababu matumizi yao yalikuwa makubwa, wakaomba Hazina na Wizara Mama, Wizara zao ziwaruhusu kutumia fedha hizo kwa maeneo hayo yaliyoainishwa. Utaona kwenye kila Balozi kuna maeneo hayo.

Kwa hiyo, tukasema kwa kuwa fedha zilikuwa huko basi tuwaruhusu watumie. Lakini kama mnavyoelewa hata eneo hilo pia tuliliwekea uamuzi hapa kwenye Bajeti ya mwaka jana kuangalia Uhasibu wake wa visa hizo utakuwa namna gani na ni jambo ambalo tumekwishaanza kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwenye hilo la Mabalozi niseme tu kwamba tunayo ratiba sasa, tunashughulikia mambo *one after another,* kimoja kwa wakati. La kwanza, ni kushughulikia majengo ya

ofisi za Balozi zetu na nyumba ya Balozi. Baadaye tutaendelea kwenye nyumba za watumishi wengine na lengo la Serikali ifike siku nyumba zilizoko Balozini nje ziwe ni mali ya Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu kidogo kwamba Tanzania ambayo ni nchi iliyopata uhuru siku nyingi haina nyumba nyingi nje lakini ukiangalia nchi kama Uganda Idd Amin, alinunua nyumba nyingi sana nje. Hivi leo kwa mfano, Ubalozi wetu wa Paris unapanga nyumba ya Uganda iliyonunuliwa na Idd Amin na kadhalika. Kwa hiyo, jambo hili linatugharimu fedha na tunaona kwamba ni muhimu tuanze hatua kwa hatua kuwa na nyumba zetu. Kwa hiyo, sasa hivi tuna nyumba Addis Ababa, Berlin na zile za Bonn tutaendelea kuzitumia kwa namna ambayo itahudumia hizi. Tuna ratiba ya kuwa na nyumba Abuja, tayari tuna nyumba Rome.

Mimi nahesabu zile ambazo zimenunuliwa kipindi changu tu. Rome, Addis Ababa, Berlin kuonyesha mzinduko mkubwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo ratiba na tunaendelea kushughulikia kwa utaratibu huo kadri fedha zitakabvyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya ya huku Mikoani kwa kweli nakubali kwamba kitu kama *uniform* kingeweza kikaelezwa vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa hapa na kwa kweli nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwamba mambo mengine haya ya humu humu ndani tungeweza tukayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuna lingine la ubadhirifu na kadhalika. Ubadhirifu unatokea pale ambapo hata Mhasibu hajui anachofanya na pengine usimamizi kutoka Makao Makuu siyo mzuri. Hili wazo la kwamba tuangalie uwezekano wa Balozi kutengewa *Vote* zao moja kwa moja kutoka Hazina, wapewe fedha zao moja kwa moja ni jambo ambalo tunashauriana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuona namna ya kulitekeleza kwa ufanisi lakini tunafikiri kwamba ni wazo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Dr. James Msekela, nadhani ni kwamba kwa kweli tunazungumza historia lakini cha maana tujifunze kutokana na historia, tumejifunza nini na tuliyojifunza ni hayo ambayo nimekwishaeleza na ndiyo maana lile swali kama tungekataa ingekuwaje. Ingekuwa balaa kwa namna fulani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ingebidi Waziri wa Fedha atumie muda mrefu zaidi kwa sababu yeye ndiye ambaye angeulizwa ilikuwaje na kadhalika. Lakini kwa kweli tugange ya mbele haya ya nyuma ndivyo yalivyotokea na maelezo ndiyo hayo kadri tulivyokuta huko lakini tugange ya mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2000/2001*(The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2000/2001) Bill, 2003)*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuhalalisha Matumizi ya Ziada ya shilingi 4,019,180,145/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya mwaka 2000/2001 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003
(The Finance Bill, 2003)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Kabla sijamwita mtoa hoja, nitoe maelezo kwamba hatukukadiria sawasawa jinsi shughuli za leo zitakavyokwenda Bungeni, inaelekea tutamaliza mapema kabla ya mwisho wa siku ya leo kwa *Order Paper* ilivyo sasa hivi.

Sasa baada ya kupokea maombi ya kuchangia Muswada uliosomwa sasa hivi na kuona kwamba ni machache, Katibu anaandaa *Order Paper* ya nyongeza ili ituwezeshe kushughulikia baadhi ya Maazimio yanayotakiwa kuridhiwa kipindi cha mchana.

Kwa hiyo, mimi nilitaka kutoa taarifa hiyo, lakini kabla sijamwita mtoa hoja namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aje anipokee ili mimi niende kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003 *(The Finance Act, 2003)* sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa wakati wa kuchambua Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yao nimeithamini na nimeizingatia wakati wa kurekebisha Muswada huu. Aidha, nawashukuru wadau na washauri mbalimbali katika sekta ya fedha na vile vile Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao kwa nyakati tofauti wamesaidia kutoa ushauri na mapendekezo yao kwa lengo la kuuboresha Muswada huu.

Mwisho napenda nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Andrew Chenge, pamoja na wataalam wake kwa kusaidia kuandaa Muswada wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ulio mbele yenu ni hitimisho la hotuba yangu ya bajeti ambayo pamoja na mambo mengine niliainisha azma ya Serikali ya kufanya marekebisho katika baadhi ya sheria, mfumo wa kodi, adha mbalimbali na vile vile kuchukua hatua nyingine zenye lengo la kuongeza mapato. Ili utekelezaji wa hatua hizi uweze kupata nguvu za kisheria umeandaliwa Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003 ambao naamini Waheshimiwa Wabunge hasa Kamati ya Fedha na Uchumi wamepata fursa ya kuupitia baada ya kufanyiwa marekebisho na kuchapishwa upya kama Kamati hiyo ilivyokuwa imeelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kufanyia marekebisho sheria 17 zinazohusu fedha na kodi kwa lengo la kuweka viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali. Sheria hizo ni sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege ya Mwaka 1992, Sheria ya Leseni za Biashara ya Mwaka 1992, Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Mwaka 1976, Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 1970, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa sura 332, Sheria ya Uuzaji Nje Bidhaa ya Mwaka 1974, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya Mwaka 2003, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 1973, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Sheria ya Usimamizi wa Mafuta ya Petroli ya Mwaka 1981, Sheria ya Ushuru wa Bandari ya Mwaka 1973, Sheria ya Ushuru wa *Stamp* ya Mwaka 1972, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya Mwaka 1995, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 1967, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Sheria ya Halmashauri za Wilaya ya Mwaka 1982 na mwisho Sheria ya Halmashauri za Miji ya Mwaka 1982.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Muswada huu umezingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa mjadala wa hotuba ya Bajeti. Kwa mfano, wakati nilipokuwa najibu hoja za Waheshimiwwa Wabunge walizotoa wakati wa kuchangia mjadala wa bajeti nilibainisha kwamba Ushuru wa Forodha kwa dawa za mbu za kuchoma utabaki asilimia 10 kama ulivyokuwa hapo awali.

Pili, utaratibu wa sheria utafanywa ili viwanda vyetu vinavyotengeneza vyandarua vilindwe. Tatu, idadi ya dawa za binadamu zinazopunguziwa kodi zitaongezwa. Nne, ushuru kwenye matumizi ya simu za mikononi utabaki kama ulivyo yaani asilimia tano na mwisho *subcontractors* wa uchimbaji wa madini wataendelea kulipia kodi ya *VAT*. Maeneo haya pamoja na mengineyo yameainishwa katika Muswada huu.

Aidha, msamaha wa kodi kwenye dawa zinazosambazwa na Wakala wa *Medical Stores Department* Vijijini za chanjo na za misaada kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya zitaundiwa *General Notice (GN)* yaani Tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo basi napenda sasa nieleze kwa muhtasari maudhui ya Muswada wenyewe sehemu kwa sehemu. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu 16. Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya utangulizi kama vile jina la Muswada na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inapendekeza kufanyia marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege ya Mwaka 1992. Katika marekebisho haya inapendekezwa kumpa uwezo Kamishna wa Kodi kukusanya ushuru kutoka kwa Wakala kwa kutumia utaratibu wa kunadi mali za Wakala pale Wakala mhusika anaposhindwa kuwasilisha ushuru aliokusanya kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu mpya una lengo la kupambana na Mawakala wa usafirishaji wa ndege ambao si waaminifu na ambao wamekuwa wakibana makusanyo ya ushuru wa tiketi za wasafiri na hivyo kuinyima Serikali mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu marekebisho katika sheria ya Leseni za Biashara ya Mwaka 1972, ambapo inapendekezwa kuondoa leseni za michezo ya kubahatisha chini ya sheria hii kwa vile kuanzia tarehe 1 Julai, 2003 biashara zote za michezo ya kubahatisha zitapatiwa leseni chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Mwaka 1976 kwa kurekebisha viwango vya ushuru wa forodha kwa baadhi ya bidhaa na malighafi zinazoagizwa kutoka nje. Malighafi na bidhaa hizo ni pamoja na nguo za pamba, mafuta ya kula, vipuri vya magari na kadhalika. Mapendekezo haya yote yana lengo la kuweka ushindani ulio wa haki kati ya bidhaa zinazoagizwa nje na zile zinazotengenezwa hapa nchini na pia kuondoa ushuru katika bidhaa na malighafi za uzalishaji. Katika eneo hili naomba nitoe msisitizo kuhusu mafuta ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitoe pongezi kwa yale makampuni ambayo yameleta hapa mitambo ya kisasa kabisa ya kusindika mbegu za mafuta ya kula kama vile mawese, karanga, ufuta, pamba na alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuingizwa kwa mitambo hiyo kumeongeza mahitaji ya mazao ya mbegu za mafuta na vile vile kumechangia katika kuwapunguzia wakulima usumbufu wa kutafuta soko kwa mazao hayo. Kwa maana hiyo basi, napenda kurudia tena nia ya Serikali ya kuhimiza wakulima kuwa na mashamba makubwa ya mbegu za mafuta kwa sababu soko la mazao hayo sasa ni la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba wenye viwanda vya kisasa vya mafuta watachukua hatua za kujitegemea kwa malighafi. Si busara kutegemea Serikali kuchukua hatua zaidi katika eneo hili nje ya kupunguza uingizaji kutoka nje wa mafuta na sabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 1970, Sura ya 27. Katika marekebisho hayo inapendekezwa kwanza

kuongeza utaratibu na hatua mbalimbali za kuchukuliwa endapo yatatokea makosa ya kughushi nyaraka za kodi kwa upande wa forodha.

Pili, kuweka utaratibu madhubuti wa kushughulikia mizigo inayohifadhiwa katika maghala ya forodha na tatu, kuweka utaratibu wa usafirishaji wa bidhaa kutoka bandarini kwenda nje ya nchi kwa kutumia barabara.

Nne, kumwezesha Kamishna wa Forodha kutoa leseni kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa zinazosimamiwa na Idara ya Forodha. Utaratibu huu una lengo la kuleta mfanano na utaratibu unaokubalika katika nchi wanachama wa *SADC*. Tano, kuwezesha mashauri yote yanayohusu Forodha kusikilizwa kwa mujibu wa sheria ya *Tax Appeals* ya Mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 332. Katika eneo hili inapendekezwa kufanya marekebisho makuu matatu kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuongeza kiwango cha faini ambacho kitalipwa na mtu yeyote atakayechelewa kuleta makadirio ya ushuru na pia kuainisha taratibu za kuchukuliwa kwa wale watakaoshindwa kulipa kodi au watakaokaidi.

Pili, kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi, mvinyo, vinywaji vikali, sigara na tumbaku ili vilingane na hali ya mfumuko wa bei. Aidha, inapendekezwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye gesi ya kupikia. Lengo la hatua hii ni kulinda mazingira yetu kwa kujenga tabia ya kutumia gesi katika kupikia badala ya kuni ama mkaa.

Tatu, inapendekezwa kutozwa ushuru wa bidhaa kwa mifuko laini ya plastiki. Lengo la hatua hii ni kupunguza madhara kwa afya na mazingira. Aidha, Serikali itaendelea kuhimiza matumizi ya mifuko ya plastiki isiyonyofoka au mifuko ya karatasi ili iweze kutumika mara nyingi pasipo kutupwa ovyo.

Kama kuna kiwanda kinachotengeneza mifuko ya aina hii nacho pia kitaathirika na ushuru huu. Ili kukabiliana na tatizo hili ni vema viwanda vya aina hiyo vikatafuta mitambo ama teknolojia muafaka ili kupunguza madhara yatokanayo na mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba inafanyia marekebisho Sheria ya Uuzaji Nje Bidhaa ya Mwaka 1974. Rekebisho lililopo ni lile la kuweka ushuru wa asilimia 20 kwenye ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuhimiza usindikaji wa ngozi ghafi hapa nchini ili nchi inufaike zaidi kwa kuongeza ajira na mapato kwa Serikali badala ya kuendelea kuuza nje ngozi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane inafanyia marekebisho sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya Mwaka 2003. Marekebisho hayo yanakusudia kukabidhi madaraka ya kutoa leseni na kukusanya ada za michezo kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawezesha Bodi hiyo kutoa leseni za biashara hii na pia kukusanya ada za michezo ya kubahatisha badala ya utaratibu wa sasa ambapo kazi hii ilikuwa inafanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mujibu wa sheria ya Leseni za Biashara ya Mwaka 1972. Hii ni kutekeleza vizuri madaraka ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ambayo Bunge lilianzisha mwezi Februari, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekebisho lingine linahusu kuipa uwezo Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kurithi mali na madeni yaliyokuwa Shirika la Bahati Nasibu la Taifa na pia kurekebisha viwango vitakavyotozwa na Bodi katika michezo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa inakusudia kurekebisha sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 1973. Pamoja na azma ya Serikali ya kuifuta sheria ya sasa ya Kodi ya Mapato na kuiandika upya bado upo umuhimu wa kurekebisha maeneo kadhaa ili Bajeti ya mwaka huu itekelezeke kuanzia 1 Julai, 2003.

Marekebisho yanayokusudiwa ni pamoja na kurekebisha kifungu 34(2b) ili kuweka utaratibu wa kulipa kodi ya asilimia mbili kwa kila malipo yanayozidi shilingi laki moja yanayofanywa kutokana na malipo ya ada, huduma au ununuzi wa bidhaa. Rekebisho lingine ni kupunguza Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)* katika mauzo ya samaki kutoka kwa wavuvi. Lengo la hatua hii ni kuondoa adha katika sekta ya uvuvi na pia kupunguza tatizo la magendo ambapo wavuvi hupeleka samaki nje ya nchi ambapo bei ni nzuri kuliko ilivyo kwao. Vile vile inapendekezwa kurekebishwa jedwali la tatu la sheria hii ili kurekebisha viwango vya Kodi ya Makubaliano *(Presumtive Tax).*

Lengo la marekebisho haya ni kuondoa kero kwa wafanyabiashara na wanaviwanda wadogo ambao hutozwa kodi ya shilingi 50,000/= kwa mauzo ya shilingi milioni 3/= kwa mwaka, ili sasa walipe kodi ya shilingi 20,000/= kwa mauzo hayo hadi kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi inapendekeza kurekebisha sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Rekebisho la kwanza linapendekeza kupunguza utitiri wa karibu aina 60 za kodi na ada mbalimbali zinazotozwa na Serikali za Mitaa ambazo ni bughudha na kero kwa wananchi na kubakiza kodi za aina 6 tu zenye manufaa kwa wananchi kwa jumla. Kodi zinazofutwa ni pamoja na zile ambazo zimeelekezwa kwa watu maskini, kama vile ushuru wa kuingiza nafaka, mboga na matunda katika masoko. Hatua hii itaondoa adha na kero kubwa wanayoipata wakulima na wachukuzi wadogo wanaokwenda kwenye masoko au magulio na mboga mboga zao au mbuzi wawili au watatu wakitarajia kuuza bidhaa hizo ili fedha watakayopata kwa siku hiyo wanunulie bidhaa au chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni ule wa mama wa Kijijini anayejilimia mbogamboga zake au anafuga kuku wa kienyeji na siku ya gulio anapeleka bidhaa zake katika gulio au soko ili auze apate fedha ya kujikimu yeye na familia yake tu. Huyu siyo mfanyabiashara kama wale wanaouza ili wapate faida. Aina hii ya mama kama huyu pamoja na watu wa aina hii hawatalipa ushuru wa kuingiza bidhaa zao huko kwenye gulio au sokoni kama vile mboga au matunda katika maeneo ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwakatisha tamaa walipa kodi hususan wale wa kipato cha chini utitiri wa kodi hizi umedhoofisha jitihada za wananchi za kupunguza umaskini na hivyo kukwamisha ukuaji wa uchumi wetu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali sasa imekamilisha orodha ya kodi, ushuru na ada ambazo zinafutwa na ambazo ni marufuku kukusanywa tena na Halmashauri yoyote kama ilivyokuwa hapo awali. Kodi hizo ambazo zinafutwa ni zifuatazo:-

Kodi ya Maendeleo, ada ya kuchuna wanyama, kukusanya mchanga na uuzaji wa asali, ada ya ramani za majengo *(Architectural Fees),* ukaguzi wa majengo, ukaguzi wa biashara na majengo ya biashara, ukaguzi wa afya katika majengo, ukaguzi wa nyumba, ukaguzi wa nyama na ukaguzi wa Mipangomiji. Ada ya mizani na ukaguzi wa hali ya usafi katika maeneo ya biashara, ada ya kuhifadhi mafuta chini ya Ardhi *(Underground Storage),* ada ya kusafirisha mizigo, ada ya zahanati au *clinic* kwa kiwango kinachosizidi asilimia 20 ya ada inayokusanywa chini ya sheria iliyohusika. Leseni kwa baiskeli, mikokoteni na cherehani, ada ya kibali cha kukausha damu, ada ya kibali cha kufanya burudani, leseni ya uchukuzi, leseni ya useremala na biashara ya magogo, kibali cha kuweka mifugo katika Miji, kibali cha kuendeleza ujuzi, yaani *Human Sources Development Permit,* leseni ya kufunga ndoa na michango ya fadhila nyinginezo yaani *other donations,* ada za huduma za kukodisha gari la Halmashauri la kubebea wagonjwa, huduma ya kuzimamoto, ada ya kibali cha mazishi, ada ya hati ya kumiliki ardhi, ada ya kutumia huduma za jamii, ada ya chanjo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni ada ya uthamini yaani *valuation,* ada ya mauzo ya vitambulisho, ada ya kuteremsha mizigo katika masoko, ada ya usafirishaji wa mazao, ada ya mitihani, ada ya kulipia hati iliyopotea, ada ya kuandikisha upya hati ya kodi, ada ya uhamisho wa mtoto shuleni, ada nyinginezo zinazohusu maombi mbalimbali ama uandikishwaji na mwisho ada ya kuandikishwa kulipa kodi yaani *Tax Registration Fee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeamua kuhusu ushuru na kodi ambazo zitaendelea kutozwa na Halmashauri kwa kiwango na utaratibu utakaoainishwa katika Sheria zao ndogo ndogo zitakazotungwa. Hizi ziko katika maeneo makuu sita kama ifuatavyo.

Eneo la kwanza, ni ushuru wa mazao na ushuru wa mazao ya misitu *(Crops cess and forest produce cess).* Ushuru huu unaotozwa katika Sekta ya Kilimo na Misitu hautazidi asilimia 5 ya bei ya kuuzia. Naomba nirudie tena rai ya agizo hili la Serikali la siku nyingi kuwa kodi au ushuru unaotozwa katika Sekta ya Kilimo na Misitu usizidi asilimia 5 ya bei ya kuuzia yaani *Farm gate price* na kitu kinachotozwa kodi kisitozwe zaidi ya mara moja. Kwa mfano, kama korosho imeshatozwa ushuru yaani *cess,* huko ilipotokea isitozwe tena kodi nyingine inaposafirishwa kwani *Export Tax* katika mazao ilikwishafutwa au kama maharage yamekwishalipiwa ushuru yaani *cess* huko yaliyokotokea yasitozwe tena ushuru au aina nyingine yoyote ya kodi yanapoingizwa na kuuzwa sokoni. Kwa upande wa mazao ya misitu Halmashauri zinatoza ushuru kwenye magogo, mbao, mkaa, kuni, fito milunda, pamoja na nguzo. Bidhaa zitokanazo na mbao kama vile samani hazitatozwa ushuru na Halmashauri. *(Makofi)*

Eneo la pili, linahusu ada mbalimbali kama vile za mifugo iliyokwishapata mnunuzi mnadani. Mifugo iliyokwishakupata mnunuzi mnadani siyo ile iliyoko kwenye eneo la mnada, ile iliyokwishakupata mnunuzi. Uzoaji majitaka na kuzibuaji mifereji, ada za machinjio na huduma ya uchinjaji, ada ya huduma ya usambazaji wa maji, kama huduma hiyo itafanywa na Halmashauri, mauzo ya miche inayosimamiwa na Halmashauri, huduma za afya, ada za kuogeshea ng'ombe katika josho, huduma zitolewazo na Halmashauri za kupandikiza mbegu, mitamba na kadhalika.

Eneo la tatu, ni ada za leseni na vibali. Katika Fungu hili ada zitakazotozwa na Halmashauri ni pamoja na kibali cha ujenzi na udhamini, ada ya uvuvi wa kibiashara, ada ya leseni ya biashara, ada ya uuzaji wa vileo, umiliki wa bunduki za jadi yaani gobori, ada ya kuvuna bidhaa za misitu kama vile mbao na kadhalika.

Leseni ya chombo cha uvuvi, matangazo mbalimbali, uchukuzi wa vitu kwa ajili ya ujenzi kama vile mawe, mchanga, kokoto na kadhalika, umiliki wa *Taxi,* ada za magari ya usafirishaji zinazotozwa chini ya sheria ya *SUMATRA* ya mwaka 2001, ada za zabuni za Halmashauri, uegeshaji magari Mijini na katika vituo vya kati vya mabasi yaani *Central Bus Stand Fees* na ada ya uwindaji kwa kiwango kisichozidi asilimia 20, umiliki wa maduka ya madawa.

Zahanati na Vituo vya Afya kwa kiwango kisichozidi asilimia 20 ya ada inayokusanywa kwa mujibu wa sheria, ada ya udhamini yaani *valuation,* ada ya kumiliki magari ya mizunguko katika miji na ada za kuweka uzio wakati wa ujenzi au ukarabati wa nyumbani yaani *scaffolding fees.*

Eneo la nne, aina ya nne ya ushuru ambao utakusanywa na Halmashauri ni ule unaohusu utoaji wa huduma yaani *Services Levy,* kodi ya majengo, ushuru wa gulio la samaki yaani *fish landing and auction levy* na ushuru wa nyumba ya kulala wageni.

Eneo la tano, aina ya tano ya kodi, zitakazotozwa na Halmashauri ni zile zinazohusiana na mauzo au ukodishaji wa mali au bidhaa za Halmashauri. Kodi hizi ni pamoja na kodi ya nyumba, kodi ya vibanda vya kuuzia bidhaa soko, magulio na minada, ukodishaji wa magari, mitambo au mali nyingine za Halmashauri, kodi ya ardhi na riba ya benki itokanayo na fedha za Halmashauri.

Eneo la sita na la mwisho, ni lile linalohusu mapato kutokana na faini na adhabu. Halmashauri zitaendelea kutunga sheria ndogo ndogo yaani *bylaws* ambazo mwananchi akienda kinyume atatakiwa kulipa faini kama itakavyoainishwa katika sheria ndogo hizo.

Aidha, Halmashauri pia itakusanya nusu ya faini zote anazotozwa mtu pale mali yake inapotaifishwa kwa amri ya Mahakama katika Halmashauri hiyo na pia Halmashauri zitatoza faini kwa mifugo inayozurura ovyo. Orodha zinazokatazwa na zinazoruhusiwa zitafanunuliwa zaidi na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Waraka maalum kwa Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ieleweke kuwa si kila kilicho kwenye orodha inayokubalika kinatakiwa kitekelezwa. Narudia si kila kilicho kwenye orodha inayokubalika kinatakiwa kitekelezwe. Kila Halmashauri itatoza ushuru na ada kulingana na mazingira yake na kwa taratibu za kawaida. Ni kosa kutotii ile orodha iliyokatazwa kwa mtendaji yeyote au Halmashauri yoyote. Ni kosa kwa mtendaji yeyote au Halmashauri yoyote kutotii ile orodha iliyokatazwa. Nashauri kila Mheshimiwa

Mbunge, ahifadhi orodha za Kiingereza zilizo kwenye Muswada huu kwani zitawasaidia sana kuelezea wananchi kwenye Majimbo yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na moja inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Udhibiti wa Petroli ya mwaka 1981. Katika eneo hili inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 4 cha Sheria hii ili kuainisha utaratibu wa kuweka mita maalum ya *flow meters* ambazo zitasaidia katika kudhibiti uingizwaji na usafirishaji wa mafuta ya petroli ili kuziba mianya ya rushwa na pia kulinda mapato ya Serikali. Kwa kuanzia mita hizo zitawekwa katika Bandari ya Dar es Salaam chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Makampuni yoyote yatakayoagiza mafuta kutoka nje yatatakiwa kupitishia mafuta yao katika mita hizo kabla hajaingizwa katika maghala yaani *storage tanks* ya kuhifadhia mafuta yao. Taratibu za awali za kufunga mita hizo tayari zimekwishaanza na inatarajiwa kwamba hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba, 2003 mita hizo zitaanza kutumika rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na mbili, inafanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bandari ya mwaka 1973. Lengo la marekebisho hayo ni kumpa uwezo Kamishna wa kukusanya ushuru kutoka kwa Wakala kwa utaratibu ambao utatumiwa pia na Kamishna wa Kodi katika kukusanya Ushuru wa Viwanja vya Ndege kama nilivyokwisha kuelezea hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na tatu, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1972. Katika eneo hili inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 51 katika jedwali la sheria hii ili kutoa haki katika ulipaji ushuru wa stempu katika Sekta ya Uvuvi kama ilivyo katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na nne, inakusudia kufanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya mwaka 1995. Katika sehemu hii inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 15 cha Sheria hii ili kumwezesha Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuwapa uwezo Maofisa wa Idara ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendesha na kusimamia mashitaka yatakayofunguliwa na Mamlaka au dhidi ya Mamlaka katika Mahakama, Bodi au Mabaraza ya Kodi au chombo chochote kinachosimamia utoaji wa haki katika suala ya kodi inayohusu Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwneyekiti, lengo la marekebisho hayo ni kuharakisha husikilizwaji wa mashauri yanayohusu kodi, na vilevile kurahisisha utaratibu wa kuwapatia uwezo Maofisa hawa wa Kodi wa kusikiliza mashauri na kwenda Mahakamani. Kabla ya marekebisho haya Kamishna Mkuu alikuwa anatakiwa awakasimu uwezo huu Maofisa hawa kwa kutoa Tangazo katika Gazeti la Serikali. Kwa vile taratibu zilizotakiwa kufuatwa hadi kutolewa Tangazo la aina hiyo zinachukua muda mrefu na mashauri mengi sana yalikuwa yanachelewa kusikilizwa na hivyo kuleta kero na usumbufu kwa mlipa kodi aliyewasilisha malalamiko yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na tano, inakusudia kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 1997. Katika eneo hili marekebisho yafuatayo yanapendekezwa. Kwanza, kuanza kuboresha utaratibu wa usimamiaji na ukusanyaji wa kodi chini ya sheria hii kama vile kuteua wadhamini.

Pili, kufuta unafuu wa *VAT* kwa magari yanayoagizwa au kununuliwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na ambayo siyo ya kidini yaani *Non Religious NGOs,* ili kubana mianya ukwepaji kodi. Kwa yale Mashirika ya Kidini, kusamehewa kodi kwa magari yenye *engine* zisizozidi *CC 3,000* bila kuathiri malori, mabasi na vyombo vya usafiri vya namna hiyo.

Tatu, kurekebisha jedwali la tatu la sheria hii ili kuwezesha magari ya kubebea wagonjwa yaani *Ambulances* kusamehewa *VAT* kwa kuwa ni sehemu ya vifaa vya afya na tiba ambavyo husamehewa kodi kwa kawaida.

Nne, inapendekezwa pia kuhamisha vifungashio vya maziwa kutoka jedwali la pili kwenda la tatu, ili kupunguza gharama ya vifungashio hivyo pamoja na bei ya maziwa yenyewe na pia kuongeza katika jedwali hili msamaha kwa vifaa vya uchimbaji wa maji vitakavyoingizwa na makampuni ya

uchimbaji maji na pia msamaha wa bidhaa za kutengenezea dawa za binadamu yatakayoagizwa na Makampuni ya kutengeneza dawa hizo.

Tano, kufuta kipengele cha kumi na moja cha jedwali la tatu la sheria hii kinatoa unafuu wa *VAT* kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, unafuu huo sasa unatolewa chini ya kipengele cha 9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na sita, inapendekeza kurekebisha sheria ya usimamizi ya fedha za umma ya mwaka 2001. Marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuboresha zaidi sheria hii na pia kuondoa dosari chache zilizojitokeza katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi na saba na ya kumi na nane ambayo ndiyo ya mwisho zinapendekeza kuzifanyia marekebisho sheria mbili za Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji zote za mwaka 1982.

Katika marekebisho hayo inapendekezwa kuwepo kwa mashauriano kabla ya kanuni hazijatungwa chini ya sheria hizi. Mashauriano hayo na makubaliano ni lazima yawe katika maandishi kuonyesha kwamba yamefanyika kati ya Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Halmashauri za Wilaya na Miji na Waziri mwenye dhamana ya Sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge mabadiliko ninayopendekeza hayaingizi jambo lolote jipya bali ni utekelezaji tu wa mapendekezo ya Serikali ambayo yamekubaliwa na Bunge wakati wa mjadala wa hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. LEPHY B. GEMBE (k.n.y. MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, juu ya Muswada wa Fedha kwa mwaka 2003 kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilipitia na kujadili makusudio ya kufanyia marekebisho sheria mbalimbali zinazohusu fedha na kodi kwa kina. Kwa madhumuni ya kuboresha sheria hizo na kujiridhisha kuwa aina zote za kodi zilizofutwa na zilizoongezwa zinakuwepo katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote Kamati inaipongeza Serikali katika kuandaa miongozo kwa Halmashauri za Wilaya na Miji katika kupunguza kero na malalamiko kutoka kwa wananchi wa kawaida, wafanyabiashara wa ndani na wawekezaji kutoka nje ya nchi kuhusu misururu mirefu ya kodi na ada zinazotozwa na Serikali za Mitaa Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirejea katika Taarifa ya utekelezaji wa sera ya Bajeti ya mwaka 2002/2003 pamekuwepo mafanikio ya kutia moyo katika kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini kutokana na mabadiliko ya mifumo ya kodi na usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yanayofikia takriban shilingi bilioni 100 kwa mwezi. Ili kuongeza ufanisi zaidi katika ukusanyaji wa kodi na kujenga mazingira mazuri ya kukua kwa uchumi ni vyema kuimarisha vianzio vya kodi zote. Kuendelea kudhibiti misamaha ya kodi, kudhibiti ukwepaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje na kuboresha mifumo yote ya kodi na kujenga mazingira yatakayowavutia wadau mbalimbali kujisikia kuwajibika kulipa kodi kwa hiari kutokana na shughuli wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu baada ya kupitia Muswada wa Fedha wa mwaka 2003 ilijitosheleza na kuridhika na hatua mbalimbali ambazo Wizara inazichukua katika kuboresha mfumo wa kodi kwa kuzifanyia marekebisho Sheria mbalimbali za kodi. Aidha, pamoja na kuupitisha Muswada huu,

Kamati ilihoji na kushauri katika maeneo yafuatayo. Ni athari gani Halmashauri za Wilaya itazipata kutokana na kufutwa kwa kodi mbalimbali ambazo ndizo zilizokuwa ni chanzo cha mapato ya kuendesha shughuli za Halmashauri hizo pamoja na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri taratibu za kufidia upatikanaji wa mapato ziharakishwe ili wananchi wasiathirike kimaendeleo. Vilevile katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa wanafanya utaratibu wa kukutana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ilisisitiza utaratibu huo hufanyike haraka iwezekanavyo. Kuhusu kuwepo ongezeko la utitiri wa minara ya simu. Kamati imeafiki kwani hali hiyo inaleta ushindani wa kibiashara kwamba wenye minara hiyo walipie kodi ya viwanja wanamojenga minara kwa Halmashauri za Wilaya.

Aidha, baada ya Kamati kukutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambaye aliijulisha Kamati kuwa Baraza la Mawaziri limepitisha Azimio kuwa wawekezaji wa simu za mikononi wasilipie minara hiyo kwa sababu wapo katika programu ya kujenga minara hiyo mpaka Vijijini. Kamati ilikubali maamuzi hayo, lakini pia imeishauri Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itoe programu ya utekelezaji wa kufikisha minara hiyo Vijijini. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitisha Muswada wa Fedha wa mwaka 2003 na kushauri kuwa Muswada huo mara utakapopitishwa na Bunge utekelezaji wake uanze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Muswada wa Sheria ya Fedha 2003 *(The Finance Bill, 2003)* kwa mujibu wa Kanuni 43(5)(b)(c) Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kambi ya Upinzani imeridhia Bajeti yote, tunaomba kwanza kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tunaunga mkono Muswada huu mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya *Finance Bill,* kifungu cha sita, kinapendekeza marekebisho ya kumpa madaraka Mheshimiwa Waziri kupunguza au kubadilisha kodi, pia kinampa Mheshimiwa Waziri uwezo wa kuweka muda maalum kwa msamaha uliotolewa kuweza kutumika. Bila shaka hili suala limekuwa likileta matatizo kwani wengine wanatumia madaraka vibaya na hii imetoa mwanya kwa Mheshimiwa Waziri kuweza kupendelea baadhi ya wafanyabiashara au kuikosesha Serikali fedha nyingi. Kwa mfano, *TBL* iliwahi kusamehewa bilioni 9 kwa sababu Sheria ilimruhusu Mheshimiwa Waziri kufanya hivyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba Bunge kwa kupitia Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi ndiyo ihusike na suala la kusamehe au kupunguza au kudhibiti kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho pia yanapendekeza kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye gesi ya kupikia. Lengo la hatua hii nikusaidia kuhifadhi mazingira na hasa ikizingatiwa kwamba wananchi walio wengi hutumia nishati ya kuni na mkaa kwa matumizi ya kupikia au kujengea. Kambi ya Upinzani inaupongeza uamuzi huo wa Serikali tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani bado upungufu huu upo kwani umeme ndiyo unaotumika zaidi Vijijini kuliko gesi. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba ni vizuri Serikali ikafikiria ni namna gani inaweza kupunguza viwango vya umeme kwani ndiyo sehemu kubwa inayotumika Vijijini kuliko Mijini. Gesi inatumika zaidi Mijini na siyo Vijijini na kwa hiyo, haiwezi kuwasaidia wananchi walio Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa kuondoa zile kodi zinazowakera wananchi kama vile ambavyo ilikuwa ni kelele za Wapinzani na Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani ya Bunge. Tunaiomba Serikali ijitahidi kuziba pengo pale ambapo itaona kwamba Halmashauri fulani imeshindwa kutekeleza Miradi yake kutokana na kukosa kodi hiyo kwa wakati. Hivyo, tunaishauri Serikali iharakishe utaratibu wa kuangalia ni Halmashauri gani ambazo kwa kuondolewa kodi zile ambazo walikuwa wakitoza, Miradi yao haiwezi kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaishauri Serikali iharakishe kuzipelekea Halmashauri fedha zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada huu, na naanza kusema kwamba naunga mkono Muswada huu mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu na mimi nichangie machache na nianze na kodi ya Ushuru wa Forodha. Hatuwezi tukalalamikia kila kodi kwa sababu uwezo wa Serikali sasa kuweza kusaidia miradi katika maeneo mbalimbali, tunafahamu kwamba unatokana na ukusanyaji wa kodi na bila kodi hakuna kitakachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kusema kwamba Serikali ingejaribu kuwavutia wafanyabiashara wawe karibu wasiogope Ushuru wa Forodha kana kwamba ni maadui. Kwa sababu mimi nipo pale Namanga tuna Forodha pale, kwa hiyo kodi zinalipwa pale. Lakini wakati mwingine wafanyabiashara wanaogopa mpaka wanakwepa sehemu hiyo. Mimi ningependa Maofisa wa kodi wafanye urafiki na kuwavutia na kuwaelimisha ili waweze kulipa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni bidhaa zinazokamatwa. Ningeiomba Serikali iangalie hizo bidhaa zinazokamatwa, wakati mwingine hazihifadhiwi kikamilifu. Hasa wakati ambapo mfanyabiashara anapokomboa mali yake inakuwa ni mali ambayo haifai kabisa, kwa sababu inakuwa haikuhifadhiwa kwa njia iliyo nzuri. Wakati mwingine mashauri yenyewe hayamaliziki upesi. Kwa hiyo, haya mashauri yanachukua muda. Mhusika anagharamia mpaka wakati mwingine anaicha mali yake iende. Kwa hiyo ningeomba hayo mashauri yawe yanamalizika upesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu Halmashauri zetu. Kwanza tunaishukuru sana Serikali kwa kuondoa kodi zote zenye kero. Tunaishukuru sana Serikali. Lakini baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi wa kodi ambazo zimefutwa, unaangalia kwamba hivi Halmashauri zingine zitakusanya nini. Kwa sababu hizi kodi nyingine za majengo, kodi za vibanda, kodi za

magulio unakuta katika Halmashauri zingine hizo kodi ni chache sana, na ni kama hazipo. Kodi za mazao, kama mazao ya misitu, kuna Halmashauri zingine hata misitu hawana. Kwa hiyo hizo kodi hazipo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kusema kwamba Serikali hili iliangaliwe kwa haraka sana, kwa sababu kuna Halmashauri zingine ambazo wataweza kuwafukuza wafanyakazi kwa sababu hawataweza kuwalipa.

Mimi nikikumbuka katika Halmashauri yangu ya Monduli, baada ya kuondoa hizo kodi zote na kujaribu kuangalia ni kodi zipi zimebaki, na nikijaribu kuwahesabu wafanyakazi ambao wanalipwa na Halmashauri naona kabisa kwamba Halmashauri haiwezi kabisa kuwalipa. Kwa hiyo, utakuta mgogoro utaingia kati ya Halmashauri na watumishi.

Kwa hiyo, ningeomba tu kwamba hilo Serikali iliangalie kama alivyosema msemaji aliyenitangulia kwamba Halmashauri zingine kwa kweli ziko hatarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kodi za mifugo minadani. Ningependa tu kujua kwamba huu ushuru kwa sababu lazima baada ya mifugo kuuzwa lazima ushuru ulipwe, lakini ni nani atakayelipa. Ni huyu aliyeuza au aliyenunua?

Lingine ng'ombe wanaotoka minadani. Wanatoka mnada huu wanakwenda mwingine. Kabla ya hizi kodi hazijarekebishwa ng'ombe wakienda minada mitatu, kila mnada aliopitia analipa kodi. Sasa

unakuta kwamba kama mmeangalia *TV* leo asubuhi, malalamiko ya wafanyabiashara walikuwa wanalalamika kwamba wanalipa kodi mpaka mara nane kwa ng'ombe mmoja. Sasa haya marekebisho bado yanaleta utata kwamba ni nani atakayelipia. Sasa hapo tupate ufafanuzi. Kama mfanyabiashara ameshalipia ng'ombe wake akipeleka kwenye mnada husika ambao anakwenda kuuzia na ana risiti za mifugo amekwishalipia bado ule mnada unamdai tena. Hii iwekwe wazi kwamba mtu asilipishwe zaidi ya mara mbili kwa sababu itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ningependa kuzungumzia suala la mifuko ya plastiki. Kwa kweli ingewezekana hii mifuko ipigwe marufuku kabisa kwa sababu inaharibu mazingira. Hata wakati mwingine ukija hapa Bungeni inazagaa hapo nje mpaka unasema mtu wa kutoka maeneo mengine akija kuona hili Bunge na uchafu uliopo hapo nje kwa kweli ni aibu, wala sio hapa tu ni kila mahali. Ingetafutwa mifuko mingine mbadala na hii iondolewe kabisa kwa sababu imekuwa ni kero na imechafua kila mahali. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba hii mifuko ya plastiki vipigwe marufuku viwanda vinavyotengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ngozi kwa kweli ni biashara kubwa sana katika nchi nyingine. Nchi jirani ya Kenya wananunua ngozi kutoka Tanzania nyingi sana. Tatizo ni kwamba sisi hatuna viwanda. Kwa hiyo, mahitaji ya ngozi, unahitaji ngozi kama una viwanda, kama hakuna viwanda bado ngozi zitanunuliwa tu hata ukisema kwamba utaongeza kodi. Ukiongeza kodi wale wafanyabiashara wataongeza nao bei. Kwa hiyo, bado ngozi zitakwenda tu.

Kwa hiyo, utafute namna ya kuzitumia hizo ngozi zilizoko katika nchi yetu. Nadhani ni sisi ndio tuna mifugo mingi sana kuliko Kenya. Lakini Kenya ndio wanatumia nyama zaidi. Kwa hiyo, ukiziba mianya na ukipata namna ya kutumia ngozi Kenya hawatakuwa na chochote. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba hebu basi tutafute viwanda vya kutengeneza vifaa vinavyotokana na ngozi. Usiwe kwamba umeongeza wewe unatumia kwa kuongeza kodi ili zisiende nchi za nje lakini sisi wafugaji tunataka tupate market ya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ningependa sana kwa dhati kabisa kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Muswada huu Bungeni na ambao ni Muswada kwa kweli ulisifiwa tangu siku ya kwanza wakati anatangaza Bajeti ya mwaka 2003/2003/2004. Mimi nina imani sana na Waziri wa Fedha na kwa kweli ninaamini kabisa yale ambayo yamepangwa yatatekelezwa kwa ufanisi na ahadi zake ni za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia hasa kwa nia nzuri ya kuweka mambo katika kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

MHE. ELIECHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Nafikiri tuwekane sawa Waheshimiwa Wabunge, mnajua kwenye Kanuni tumekubaliana kwamba tukiingia ndani tunazima simu. Huwa tunasahau lakini Kanuni ipo nafikiri. Tujitahidi na kuhakikisha tukishaingia kwenye gari tunazima tunapokuja hapa. Zinasumbua sana simu hizi. Tunasahau *of course.*

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa kweli nashukuru sana kwa uwasilishaji mzuri wa Waziri. Yale nitakayozungumza zaidi kwa kweli nitazungumzia ya kuimarisha na pengine kuweka kumbukumbu katika rekodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Waziri kwa maelezo mazuri ya kufuta kodi. Nimshukuru sana kwa wale wananchi wa Lushoto ambao kwa njia moja au nyingine magulio hasa hao wauzaji wa mbogamboga na matunda ambao amewataja walikuwa wanamia sana na kero zilikuwa ni ndogo lakini zilikuwa zinawaumiza sana. Maana kama ulivyosema si halali mtu ameleta kuku kwenye

soko au matunda maparachichi kabla hata hayajafika hata sokoni yameshikwa kodi. Magimbi haya labda atauza labda kwa shilingi 200/= wewe unamshika shilingi 200/=, kwa hiyo, anaondoka sokoni tupu.

Mimi namshukuru sana Waziri ninajua tutapata matatizo wapi tutapata mapato lakini ndiyo kazi ya Serikali, kuondoa kero na kutafuta mbinu nyingine za kuwafurahisha wananchi wake. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie eneo moja ambalo ni muhimu pengine maelezo yatoke haraka kwenye Serikali. Ukiangalia ukurasa ule wa 43 katika Muswada na kwenye schedule ya zile kodi ambazo zinaruhusiwa kukusanywa na Halmashauri.

Mimi natoa tu tahadhari kwamba katika *schedule* hiyo kuna kodi kama *Hospital user charges* na *clean water charges for water services landed by the council.* Hizi kodi zilikuwepo, lakini zilikuwa na matumizi rasmi. Kwa mfano, huduma zilizokuwa zinatolewa hospitali, michango ya wananchi ilikuwa inakwenda kuendeleza hospitali zenyewe. Sasa tukiiweka kama mapato ya Halmashauri ni vizuri ifafanuliwe vizuri ili tusije tukaondoa hayo mapato ambayo yalikuwa yanasaidia huduma za hospitali na huduma za maji. Hili ni ushauri na naomba itekelezwe.

Lakini lingine ambalo ningeomba nichangie na nilizungumza wakati Kamati ya Fedha na Mipango ilipokuwa inajadili. Waziri aliandikiwa na Viwanda vya Madawa kujaribu kuangalia hali halisi ya kuweza kuvilinda viwanda hivi kwa kulinganisha na nchi jirani. Kenya wana viwanda 26 vya madawa, Tanzania tuna viwanda 6 vya madawa, na kwa utaratibu wa kodi zilivyo madawa yanasamehewa kodi. Sasa unaposamehe kodi bila utaratibu wa kuangalia ndani kulinda viwanda vyako ni rahisi sana kuua hivi viwanda 6 vilivyobaki. Waziri ameahidi na kwa sababu barua ile anayo ni vizuri haizingatie na kwa kweli ameahidi kwamba mwakani atajaribu kuangalia ni vipi tuweze kulinda viwanda hivi na wao kubwa walililoliomba ni kwamba zile *schedule* kule kwenye *schedule* za kulipa kodi hasa za malighafi wanazoingiza zingewekwa kwa utaratibu ambao zitakuwa *charged VAT* ili warejeshewe. Sasa naomba Waziri hilo aliangalie.

Vile vile dawa zinasamahewa kodi kama asilimia 5. Wakati dawa za kutoka Kenya zinapoingia Tanzania zinasamehewa asilimia 2 tu. Ukiangalia kwamba wenzetu wa Kenya leo hii hivi *VAT* ya kwao ni asilimia 16 ya kwetu sisi ni asilimia 20. Kwa hiyo, mzalishaji wa dawa Kenya akiingiza hapa, kwanza automatically akishalipa asilimia 2 kwa Mtanzania ofcourse atalipia *VAT*. Kwa hiyo, naliomba hili liangaliwe na kwa sababu barua imepelekwa kwa Waziri ninaamini Waziri atachukua hatua.

Pia ningependa nizungumzie neno moja ambalo Waziri jana aliahidi wakati akizungumzia Wizara ya Fedha suala la *VAT* kupunguzwa. Ni kweli Waziri ametoa maelezo mazuri na mimi nakubaliana naye. Lakini tuielewe tunavyoendelea kuahirisha katika masuala ambayo yanahusu Jumuiya ya Afrika Mashariki au Jumuiya zile ambazo tunafanya nazo biashara tutafika mahali kama mlipa mkopo. Unapolipa mkopo na ukaendelea kuucheleweshe kuulipa siku utakapokuja kuulipa itakuwa ni kazi kubwa sana.

Sasa nasema hivi kwa sababu tunavyoendelea kupunguza hivi viwango vya kodi hasa ya *VAT* wakati wenzetu wanashika asilimia 16 sisi tuko asilimia 20, siku tutakaposema tunashuka si rahisi itakuwa ni kazi ngumu sana. Sasa kwa sababu tumeingia katika ushindani na tukubali, tusikubali, mwezi Novemba, 2003 tumewaahidi wenzetu tunaweka mkataba ule wa makubaliano ya kuwa na kodi zinazofanana matokeo yake sisi tutakuwa na pengo kubwa la mapato. Kama tutajitahidi na tutaendelea kuhakikisha kwamba viwango vyetu vya kodi vinabaki vile vile viwanda vya Tanzania vyote vitakufa. Tutakuwa ni masoko ya wenzetu.

Mimi huo ndio wasi wasi wangu nilionao katika hili suala la kucheleweshe utaratibu wa kurekebisha kodi kwa kuamini kwamba tutakapofanya huko mbele tutapata unafuu. Si kweli.

Naomba Waziri ajaribu kuona na kwa sababu tumekwishaamua tutaingia katika ushindani na viwango vyetu itabidi vifanane na wenzetu mimi woga wangu ni kwamba Tanzania tutakuwa ni soko la wenzetu. Ukishaua soko la mwenzako vionjo vyake vikikubalika katika soko lako sio rahisi tena kuwarejesha watu wako hata wakiwa ni raia wako uwaambie tumieni vitu hivi msitumie vya jirani wakati wameshaelewa vionjo vya yule jirani yako.

Kwa hiyo, pengine utunge sheria kwamba sasa sitaki mtumie. Ukishafika hapo tena umekwishaua ule undugu ambao mlikuwa nao na huyo mwenzako ambaye ameingia katika ubia wa kuwa na aina moja ya kodi.

Kwa hiyo, mimi naliomba hili kwa upande wa Serikali kwamba ni kweli tutasubiri mwakani. Lakini muelewe kwamba tunasaini mkataba ule mwezi Novemba. Sasa mwakani Bajeti itakuwa ni ngumu sana kwa Waziri wa Fedha kutafuta vyanzio vya fedha kwa sababu *rates* za kodi zitakuwa sisi itabidi tulingane na wenzetu na ni vizuri tupambane nao katika soko. Vinginevyo Tanzania itakuwa ni soko la wenzetu na watu wetu watakosa ajira kwa sababu viwanda vitafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nilitaka nichangie ni yale yaliyosemwa kama maoni ya Kamati. Mimi nimefarijika sana kwa utundu wa Waziri wetu wa Fedha kutafuta vyanzio vipya na kuimarisha vile vilivyokuwepo.

Mimi ningependa sana kwa sasa hivi tujifunze kutoka kwa wenzetu kama tulivyofanya mwaka huu kuhakikisha kwamba vianzio vya kodi ambavyo vina kero vinaangaliwa. Sasa mimi naomba wenzangu wa *TRA* kwa kweli kuna wachapakazi wazuri sana. Lakini wako wachapakazi wachache wenye kuharibia heshima na sifa wafanyakazi wa *TRA*.

Mimi napenda kuupongeza uongozi mpya uliochaguliwa kuingia *TRA*. Nina imani sana nao kwa sababu alikuwemo na napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Bwana Sanare. Kwa bahati nzuri mimi nilifanya kazi na Bwana Sanare na alikuwa kiongozi wangu ni mtu mwadilifu, mchapakazi asiyechoka na kwa sababu kwa kweli amepata madhara akiwa kazini mimi naamini Serikali inamlinda na itampa haki na ninaamini ameondoka kwa sababu ya afya yake lakini hakuondoka kwa sababu ameshindwa na kazi. Ameondoka kutokana na afya yake ni mbovu na ninaamini wale ambao wamepewa madaraka kwa niaba yake kuchukua nafasi yake watamwondoa aibu kama walivyoendelea kumwondoa aibu huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kwa watumishi wachache wa *TRA* kama Waziri alivyoahidi. Kwa kweli ni jukumu letu sisi wote mfanyakazi anapoonekana ana kero atajwe mara moja bila ya kumwonea aibu na tumsaidie Waziri kwa kuwataja. Mimi nimekwishafanya hivyo mara mbili na napenda kuushukuru uongozi wa *TRA* wamewachukulia hatua kali na ushahidi ninao.

Kwa hiyo, ninaomba wote tuungane kuisaidia Serikali kuwafichua wale ambao kwa kweli tuna uhakika hawaisaidii Idara yetu na hawasaidii kuimarisha mapato ya Serikali. Ni kweli mapungufu yapo lakini yale ambayo yamezidi kiasi tusiyavumilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivi napenda kumshukuru sana Waziri kwa hotuba nzuri na naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu zaidi nitaelekeza kwenye sura ya 10 ya Muswada ambao umependekezwa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imependekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Nia hapa ni kujaribu kupunguza idadi ya kodi ambazo zinatozwa na Halmashauri za Wilaya. Kwa kweli Serikali imejitahidi kupunguza hizo kodi kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyosema katika hotuba yake kutoka kodi zaidi ya 66 na kubakiwa na kodi 6 tu hivi sasa. Mimi kwa niaba ya Halmashauri yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Kondoa Kusini, kwanza napenda niipongeze sana Serikali kwa hatua hiyo.

Pili, napenda niishukuru sana Serikali. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema hatua hizi zimechukuliwa ili kupunguza kero kwa wananchi wetu. Kwa kweli tunapongeza kwamba Serikali yetu inajali sana wananchi wake na ndiyo maana imechukua hatua ya kupunguza hizo kero kwa maana ya kupunguza hizo kodi ambazo zina kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ambayo imechukuliwa ni kubwa na itakuwa na athari kubwa sana kwa Halmashauri zetu. Mimi nimejaribu kuangalia jedwali lililopo katika kitabu chetu cha Muswada jedwali ambalo liko ukurasa wa 42 hadi 48. Nikiangalia katika kodi ambazo zimependekezwa ama ambazo zimebakizwa ziko katika makundi 6 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Halmashauri ya Wilaya Kondoa sioni kodi gani tutatoza pale hatuna. Kwa maana ni kwamba kodi zote ambazo tulikuwa tunatoza katika Halmashauri ya Kondoa hazipo zimefutwa zote.
Kwa maana hiyo na hasa hasa kodi ambayo ilikuwa inatozwa na Halmashauri ilikuwa ni kodi na maendeleo na ushuru wa mifugo.

Napenda nimwarifu Mheshimiwa Waziri kwamba vyanzo hivi viwili kodi ya maendeleo na ushuru wa mifugo ilikuwa inachangia asilimia 80 ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Inawezekana sio Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa tu ziko Halmashauri ambazo zinafanana na Wilaya ya Kondoa. Kwa hiyo, hivi sasa tunapozungumza hapa ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni kama vile imesimama kwa sababu kodi zake zote ama vyanzo vyake vyote vimesimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa kufanya hivyo, Serikali imechukua hatua kwa kuona kwamba wananchi wa Wilaya ya Kondoa wana matatizo hayo na ndiyo maana wamefuta hizo kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimefarijika sana vile vile kusoma hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha na vile vile katika Muswada huu Waziri ameahidi kwamba atafidia. Hiyo ndiyo imekuwa ni faraja yetu kwamba Serikali kuu itafidia yale mapengo yote ambayo Halmashauri za Wilaya zitakazoathirika zitafidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana. Mimi nimesimama hapa kuomba kwamba kwa kweli hatua ya kufidia ichukuliwe haraka kwa sababu mimi nimepata taarifa kutoka Wilayani kwangu na napenda nimwarifu tu Mheshimiwa Waziri kwamba Wilayani kwangu kama nilivyosema hapo awali ni kwamba shughuli zote za Halmashauri sasa hivi zimesimama kutokana na mapato hayo kutopatikana. Ni shughuli gani zimesimama sasa hivi napenda niziorodheshe hapa.

Katika Wilaya ya Kondoa ilikuwa imebajeti kutumia shilingi 756,000,000/= kwa ujumla. Lakini katika hizo shilingi 756,000,000/= mapato yanayotokana na kodi ya maendeleo na mifugo ilikadiriwa kuwa shilingi 600,000,000/= ambayo ni sawa sawa na asilimia 80 ya mapato ya Halmashauri.

Sasa kutokana na uamuzi wa Serikali kama nilivyosema tunashukuru kwa uamuzi huo lakini athari zake ni kubwa katika uendeshaji wa Halmashauri. Hivi sasa ninavyozungumza athari zifuatazo zimeanza kujitokeza. Moja ni kwamba Halmashauri imeshindwa kuchangia miradi ya wafadhili ambayo inatekelezwa katika Wilaya hiyo.

Kwa hiyo, miradi mingi ya Halmashauri ambayo ilikuwa inafadhiliwa na wafadhili hivi sasa imesimama. Kwa hiyo, tunaomba basi mchango wa Serikali Kuu uwahishwe ili miradi hii iweze kuanza kutekelezwa kwa sababu hivi sasa imesimama. Watu wanaanza kujiuliza kwamba hivi uamuzi wa Serikali ni wa busara ama si wa busara.

Jambo la pili ama athari ya pili ambayo imeanza kujitokeza katika Halmashauri na naamini katika Halmashauri nyingine vile vile linaanza kujitokeza ni kwamba baadhi ya watumishi wa Halmashauri sasa hivi hawalipwi mishahara. Kwa mfano, mshahara wa mwezi wa Julai katika Wilaya ya Kondoa haujalipwa hasa kwa wale ambao wanalipwa na vyanzo vya Halmashauri hawajalipwa mpaka sasa kwa sababu hakuna mapato. Kwa hiyo, hao watu wanahitaji msaada wa Serikali Kuu kuletewa fedha ili waweze kulipwa mishahara hasa watendaji wa vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine ambayo imeanza kujitokeza ni kwamba Halmashauri ilikuwa imejiwekea kuchangia mifuko mbalimbali. Mifuko hiyo ni pamoja na Mifuko ya Vijana, Wanawake, Mifugo na Elimu. Hiyo nayo kwa sababu vyanzo vyake vya Halmashauri vimefutwa basi nayo haichangiwi kwa sababu hakuna mapato ya namna hiyo ama kodi hiyo tena haiendelei kutozwa. Kwa hiyo, tunaomba vile vile tupate msaada ili mifuko hii nayo iweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya mwisho ambayo imeanza kujitokeza vile vile ni kwamba hivi sasa vikao vya Madiwani havifanyiki kwa sababu hakuna mapato. Sasa maamuzi hayafanyiki katika Halmashauri. Kwa hiyo tutakuwa na athari ama tutakuwa na matokeo ambayo siyo ya kuridhisha.

Kwa hiyo, tungependa Serikali ichukue hatua za haraka. Kwa kuwa katika Muswada huu umependekezwa kwamba mwaka wa fedha wa Halmashauri utaunganishwa na ule wa Serikali Kuu, tunaomba basi kila robo mwaka Serikali ama Wizara ya Fedha itoe fedha ya kuweza kujaza hayo mapengo ambayo yametokana na kufutwa kwa kodi mbalimbali katika Muswada huu. Kwa hiyo, pamoja na shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kondoa na hususan kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Kusini, lakini vile vile kilio hicho naomba mkipokee na hasa Waziri wa Fedha akipokee na akifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba jitihada zinafanyika kuweza kufanya mahesabu kati ya Wizara ya Fedha na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa, ili tuweze kupata fidia hiyo lakini naona hatua zinachukuliwa taratibu mno. Naomba hatua za haraka zichukuliwe vinginevyo Halmashauri zetu zitakufa.

Mheshimwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda niishie hapa nikushukuru tena na natamka kwamba naunga mkono Muswada huu upite mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naanza kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa kodi nyingi ambazo zilizokuwa kero kwa wananchi mjini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuzungumzia suala la *Gaming Act, 2003* (Kamari). Ukiangalia *Night Club* na *Entertainment Halls* zimeongezeka sana Tanzania. Akija mgeni anaweza kufikiria kwamba akiingia Dar es Salaan anaweza kufikiria yuko Las Vegas, Nevada kule Marekani. Tusishamilie sana mapato haya ya *Gaming Act,* tusichukulie kamari kuwa njia ya mapato. *Slot machines* zinachajiwa shilingi 16,000/= kwa mwezi ni kidogo sana inafanya Mikoa yetu mingi vijana wengi wanafanya ndio kipato chao kwenda kucheza kamari. Hii inaondoa maadili yetu ya Watanzania. Vijana wengi utawakuta wamo ndani na imekuwa kama ni *Night Club* na sehemu za kufanyia ngono vile vile. Ningeshauri Wizara iweke viwango vya hali ya juu ili visiongezeke vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ningependa kuzungumzia kuhusu mifuko ya plastiki inavyoharibu mazingira. Si mifuko ya plastiki tu, kuna *disposable water* hizi *bottles, glass disposable, syringe* na vifaa vingi na naipongeza Wizara kwa kuanzisha asilimia 15 *excise duty* ya mifuko ya plastiki inayotengenezwa nchini, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuhusu kodi wanaotozwa wafanyabiashara wenye *turnover* ya shilingi 3,000,000/= yaani shilingi 250,000/= kwa mwezi hawa ni wauza uji na maandazi, wakaanga samaki, ningeishauri Wizara ingeondoa kodi kwa wafanyabiashara hao wadogo. Ni moja ya hatua ya kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliongea kuhusu upunguzaji wa *VAT* akipunguza asilimia moja inaleta kasoro ya shilingi bilioni 70 ya Bajeti. Je, Mheshimiwa Waziri hakuzingatia faida itakayopatikana ikiwa *VAT* itakuwa asilimia 10 kasoro yaani shilingi bilioni 70 ni hata haifiki ni mapato ya mwezi mzima ya *VAT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeungana na Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwamba *VAT* ipunguzwe ili kuhakikisha kwamba nchi inakuwa na *turnover* kubwa zaidi kwa sababu kupunguzwa *VAT* italeta *turnover* katika biashara ambayo matokeo yake itafidia ile shilingi bilioni 70 aliyoitaja yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu sana, naipongeza kwanza Wizara kwa kupunguza ushuru katika gesi hii itasaidia sana katika kuhifadhi mazingira na vile vile kuna umuhimu sana wa kupunguza bei ya nishati umeme *(Electric Tariff)*. Hii itasaidia sana kwa wananchi hasa viwanda katika sekta ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo tu Muswada huu wa *Financial Bill.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua nzuri yenye manufaa kwa wananchi ya kuwaondolea kero kubwa sana. Wananchi wetu walikuwa wanahangaika wanajificha maporini kwenye mapango kwa kuogopa kodi hiyo ya maendeleo. Badala ya kutumia muda wao kushughulika na mambo ya maendeleo ya kiuchumi wanatafuta mahali pa kujificha ili wasishikwe. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi kule nyumbani kwangu ilikuwa ni kodi ya mitumbwi. Ziwa Nyasa halina samaki, wale wavuvi walikuwa wanalipia leseni ya mtumbwi sio *boat* na mapato yake kwa mwaka haifiki hata shilingi 50,000/= kwa hiyo, wanalipia leseni na wachuuzi wanaonunua visamaki havifiki hata shilingi 5,000/= walikuwa wanalipia ushuru wa biashara hizo. Baada ya Serikali kutangaza kodi zinazosumbua wananchi zifutwe na kwa niaba wa wananchi wangu wa Jimbo la Mbinga Magharibi, ninaipongeza sana Serikali na ninaishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia juu ya jedwali namba 15 kuhusu *Value Added Tax (VAT)*. Ninaungana na wenzangu kuwa kodi hii ya ongezeko la thamani, Serikali yetu ilianza kuitumia toka mwaka 1997. Wakati ilipoanza, Serikali ilikuwa ina wasiwasi kwa sababu ilikuwa ni kodi mpya na wafanyakazi walikuwa hawana ujuzi.

Kwa hiyo, ingekuwa siyo vyema kama Serikali ingeanza na kiwango cha chini, kwa wakati ule Serikali ilifanya vizuri ikaanza na kiwango cha juu. Lakini leo hii wafanyakazi wa *TRA* wame-*gain experience* ya kutosha kabisa, wana uwezo mkubwa na imethibitishwa kuwa kodi hii haina matatizo, inaweza kukusanya mapato kwa ajili ya kuendesha Serikali yetu.

Kwa hiyo, kutokana na hali tuliyofikia, ili kuweza kuipanua Kodi hii ya Ongezeko la Thamani na watu wengi walipe, wasijifiche kama Wananchi wangu walivyokuwa wanajificha miaka ya huko nyuma kwa kodi ya maendeleo. Tumefikia wakati muafaka kupunguza hiyo *Value Added Tax* na ninaishauri Serikali ifikirie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha 20% kwa kweli ni kiwango kikubwa ukilinganisha na nchi jirani kwani wote tunakwenda pamoja, tuko katika Jumuiya ya *East Africa.*

Kwa hiyo, ili tuweze kushindana vizuri, inafaa sana Serikali yetu ianze kufikiria suala hilo, ipunguze kodi ili tuwe washindani katika shughuli zetu zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka huu 2003.

Pili, nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Serikali yetu hususan Wizara ya Fedha. Pia, niipongeze Serikali kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Same Magharibi, kwa kuondoa utitiri wa kodi uliokuwa unasumbua Wananchi kwa kodi za ushuru mbalimbali wa Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitisha kodi hizi ambazo leo zimeweza kuainishwa zile ambazo ni haramu na zile ambazo ni halali, bado nafikiri baada ya Serikali kulitamka hili, baada ya bajeti

ya Serikali ya Wizara ya Fedha kutolewa, bado Halmashauri zilikuwa zinawabughudhi sana Wananchi. Mpaka leo Wananchi wanasumbuliwa sana na watozaji wa ushuru wa Halmashauri huko katika Majimbo, Vijijini na katika Kata. Wao katika Halmashauri wanadai wanasubiri wapelekewe Waraka. Sasa, sielewi Serikali za Halmashari na Serikali Kuu jinsi ambavyo zina mahusiano ya kuheshimiana na kusikilizana inakuwaje Serikali Kuu inatoa tamko, wao wanasema wanasubiri Waraka *(Circular)* au kitu kingine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa Serikali zetu zingeheshimu lile ambalo linatamkwa ndani ya Bunge na Serikali yetu na liweze kufuatwa. Vinginevyo unakuta Viongozi wetu katika Halmashauri hawaelewi ni kwa nini Serikali Kuu imefikia uamuzi wa kuondoa utitiri wa kodi, kodi ambazo zinasumbua watu wetu wengi ambao wanaishi maisha ya kimaskini, mfano akina mama wadogo na akina mama wakubwa wanaouza biashara ndogo ndogo za mchicha, samaki na kadhalika, wanabughudhiwa na kukimbizwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba baada ya siku ya leo Halmashauri zetu zifahamu kwamba Serikali imetoa agizo, liheshimiwe na lifuatwe Wananchi wasibughudhiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niishukuru Wizara ya Fedha kwa kutupatia kituo cha kulipia kodi ya *TRA* kule katika Wilaya ya Same, badala ya hali ya zamani ambapo ilibidi Wananchi katika Wilaya ya Same wasafiri umbali mrefu kutoka Same mpaka Wilayani Mwanga kulipa mapato ya Serikali. Wananchi walikuwa wanatumia fedha nyingi kati ya shilingi 10,000/= hadi shilingi 15,000/= kwa nauli, kwa ajili ya kulipa ushuru wa Serikali.

Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri ifikapo hiyo Januari, 2004 kama alivyoahidi katika hotuba yake, Wananchi wa Same waweze kulipia mapato yao pale Wilayani badala ya kupata usumbufu wa kwenda mpaka Wilayani Mwanga.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu elimu kwa walipakodi. Ninaishauri Wizara na hasa *TRA* waendeleze utaratibu waliouanzisha wa kuelimisha walipaji wa kodi. Kwa kweli wafanyabiashara wetu wengi wanaolipa kodi wana elimu ndogo sana kuhusu wajibu wao wa kulipa kodi. Lakini baada ya *TRA* kuanza kuwapa elimu ya ulipaji wa kodi, wengi wao wameanza kuzinduka na kuelewa wanachotakiwa kufanya.

Kwa hiyo, naiomba Wizara na Shirika la *TRA* waendeleze elimu kwa walipa kodi. Kuwaelimisha wajibu wao na kuwafahamisha wanatakiwa walipe kodi gani na kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ni kuhusu watozaji wa kodi katika *TRA*. Zamani ilikuwa inatokea kwamba Wananchi walikuwa hawajui kigezo cha kulipishwa kodi, akifika kwa mlipishaji wa kodi basi anasubiri kama kupata hukumu ya Mwenyezi Mungu, anauliza: "Natakiwa kulipa ngapi?" Anambiwa: "Unatakiwa kulipa shilingi 400,000/=" wanaanza ku-*negotiate.* Nafikiri suala la kulipa kodi lisiwe la ku-*negotiate,* liwe na vigezo fulani, mtu hata akiondoka nyumbani anajua, mfano natakiwa kulipa shilingi 50,000/= ama natakiwa kulipa shilingi 60,000/=. Kwa hiyo, anabeba kodi yake pamoja na posho yake ya kula na nauli. Lakini anapoondoka, anaondoka kwa hatihati na pesa nyingi ama pungufu kwa sababu hajui kodi anayotakiwa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishauri *TRA* kwa makusudi kabisa iweke vigezo vya wazi kwa walipakodi wakati wanapowaelimisha kwamba, wewe kama unafanya biashara fulani, jiandae kuja na shilingi kadhaa na akija kusiwe na habari ya ku-*negotiate* ama ya kubembelezana. Hii kodi ni ya Serikali, haina mahusiano ya kubembelezana kati ya anayetoza kodi na mlipaji. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeweza kuwapa Wananchi wetu nafasi nzuri sana ya kujiamini kulipia kodi ya nchi yao na maendeleo ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo napenda kuchangia ni kuhusu kodi ya *VAT,* ambayo wasemaji wengine wameishawishi Serikali kwamba ipunguze kidogo. Ninashauri kwamba, iwapo mazingira ya kupunguza yapo Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kupunguza kodi ya *VAT* kidogo na kupanua wigo wa kodi kwa njia zingine ili wale wanaolipa wasianze kuleta mazingira ya kukwepa kwepa. Watu wanakwepa kwa sababu 20% ni nyingi na tunafikiri kwamba kama kungekuwa na punguzo kidogo bila shaka na huo wigo ungeweza kuwa mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine yenye tatizo kwenye kodi ni kwenye *stamp duty.* Wananchi wengi hawajui elimu ya kodi ya *stamp duty* kwani nimeshahudhuria baadhi ya vikao vya *TRA* kuhusu uelimishaji wa ulipaji wa kodi, lakini elimu kuhusu *stamp duty* haiko wazi. Tunaomba hiyo elimu itolewe vizuri kwa walipaji wa kodi waweze kuifahamu. Wao wanalalamika tu kwamba kuna utitiri wa *stamp duty* na kadhalika, lakini hawaelewi. Tunaomba waelimishwe ili wajue wajibu wao wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichukue tena nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu Mkuu, Mhasibu Mkuu, Watendaji wa *TRA* na Mashirika mengine kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya mapato ya nchi hii kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho na tumewasiliana na Mheshimiwa Waziri ili tuwape muda wakajiandae, watakuja kujibu hoja baadaye jioni. Kama mlivyotangaziwa kwenye *Supplementary Order Paper,* tutakuwa na jambo moja au mawili ili kutumia muda wetu vizuri. Kwa hiyo, naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 06.11 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniita niweze kuwajibu Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ambao ni Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga na Mheshimiwa John Singo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawajibu mmoja mmoja na pia kwa ujumla wao. Nianze na Mheshimiwa Lekule Laizer, alikuwa na wasiwasi juu ya bidhaa kukamatwa kwenye vituo vya forodha na kutotunzwa vizuri. Niseme tu kwamba Shirika la Mamlaka ya Mapato wanajiandaa sasa kujenga majengo mazuri ya kuhifadhi bidhaa za namna hiyo. Itachukua muda lakini kazi hiyo imekwishaanza na hasa kwenye vituo vikubwa vya forodha. Vile vile aliuliza mifugo ipi hasa kwenye ile orodha iliyoruhusiwa itatozwa pale mnadani? Hili linafanana pia kwa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba ng'ombe wakiletwa mnadani hawatatozwa ushuru/kodi yoyote kwa kukaa tu pale mnadani, ni lazima wawe wameuzwa, lazima wawe wamepata mnunuzi, ndiyo hapo wataanza kutozwa kodi au ushuru wa mnadani. Lakini kama ng'ombe anatoka mnada fulani akaingia kwenye mnada wa pili mbele huko kwa kuingizwa tu kwenye mnada huo wa pili hatozwi chochote. Lakini akiuzwa kwenye mnada ule atalipia. Hivyo hivyo kama tulivyoeleza kwenye mazao.

Mheshimiwa Henry Shekiffu, jana alikuwa na wasiwasi sana juu ya dawa za binadamu. Hoja yake nimeichukua kwamba tuangalie uwezekano wa kulinda viwanda vyetu wakati tukichunguza mambo ya ushuru na *VAT* kwenye madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo jana na juzi kwenye Kamati nililieleza kwamba hivi sasa tunaangalia eneo zima la dawa za binadamu ili mbele ya safari labda Bajeti ijayo tuweze kuangalia kama tunaweza tukapunguza ushuru zaidi ya ilivyo hivi sasa. Lakini niseme tu kwamba kwa sasa hivi hakuna *VAT* kwenye dawa yoyote. Sasa hivi dawa yoyote haina *VAT* lakini dawa zinalipa ushuru wa asilimia 10.

Sasa hivi tunavyozungumza orodha ya dawa ambazo labda zitasamehewa kodi ya ushuru ndiyo tunaiangalia na ikiwezekana labda ushuru huo wa asilimia 10 unaweza ukafikiriwa. Lakini suala zima tunalifikiria kwa makini na nitaliwekea matangazo zaidi huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TRA* kuwa wakali mambo ya watumishi nitalieleza baadaye hili suala la watumishi wasiofaa, watumishi wasio waaminifu katika Mamlaka ya Mapato.

Vile vile Mheshimiwa Paschal Degera, alionyesha wasiwasi juu ya Halmashauri kukosa mapato hasa Halmashauri ya kwake ambayo alisema asilimia 80 ya mapato yao ya Halmashauri ya Kondoa hutegemea mifugo na hizi kodi ambazo tumezifuta. Nitalieleza baadaye kidogo hilo lakini niseme tu kwamba kama tunaeleza pengine woga huu na jana nilijaribu kueleza pengine siyo mkubwa kama ulivyo ni wasiwasi tu nitaueleza baadaye.

Pia Mheshimiwa Abdullatif Esmail, alikuwa na wasiwasi juu ya hii michezo ya kubahatisha *(Slot Machines)* hasa kwamba zinaweza zikaingiza Tanzania maadili yasiyofaa. Mimi nakubaliana naye kwamba *(Slot Machines)* na shughuli nyingi zinazofanywa mahali penye ulevi na pesa usiku zinaweza zikaleta maadili ambayo hayafanani au hayafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanywa ni kwamba kabla hujatoa leseni kwa watu wa namna hii mara nyingi huwa wanachunguzwa sana. Katika nchi nyingi wanachunguzwa kuelewa ni watu wa namna gani, tabia zao, mienendo yao. Wengine wanaweza wakawa wanatumia hizo *Slot Machines* kwa mambo mengine hata ya uhalifu kwa mfano mambo haya ya fedha haramu au mambo mengine kama ya ukahaba na kwa hiyo ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Abdullatif Esmail, kwamba tutakuwa waangalifu sana wakati tukitoa leseni kwa watu wa namna hii. Ni kweli vile vile kwamba ni vizuri kuwe na leseni chache nzuri kuliko kuwa na leseni nyingi, ilimradi tu kila mtu amekata leseni. Hili nalo tutalifikiria. Niseme tu kwamba dawa siyo kuongeza kodi hizi, kwa sababu sasa ni mwaka wa tatu tumekuwa tukichunguza biashara hii kwa Tanzania, kulinganisha na nchi za nje na naweza nikasema kwamba hapa tulipo ni kama tumefika. Hatutaki tena kufanya mabadiliko yoyote au mambo yoyote ambayo yataiyumbisha biashara hii mpaka hapo baadaye tutakapoona kwamba kweli kuna ulazima.

Kwa hiyo, tutaendelea na *rates* zilizoko isipokuwa tutakuwa waangalifu sana kuwasimamia na kuwafuatilia hao wenye leseni hizo. Ndio maana kwenye Muswada ule wa hii biashara kuna kipengele pale tuliweka Wabunge, wako Wabunge wawili nadhani wako kwenye bodi hiyo, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Salome Mbatia, ili kama wakiona kuna jambo ambalo haliendani, wanaweza wakatumia nafasi zao au wakaleta taarifa kwa Waziri wa Fedha ambaye ataweza kuchukua hatua zinazofaa.

Hili suala la mifuko ya plastiki na bidhaa nyingine za plastiki ambalo pia lilimtia wasiwasi Mheshimiwa Abdullatif Esmail, ni kwamba ukweli kama nilivyoeleza wakati wa bajeti nia ya Serikali haikuwa kufuta bidhaa zote za plastiki. Kuna ambazo ni nzuri hazinyofoki haraka na zina sifa fulani ambazo watu wa mazingira wanazikubali. Ile aina ya plastiki nyembemba ambayo niliisema kwenye Bajeti na ambayo ndiyo tunailetea ushuru wa asilimia 15 ndiyo inayosumbua na ndiyo wana mazingira wanayasema kwamba ina madhara kwa afya na kwa mazingira. Ile ndiyo tunataka watengenezaji wa bidhaa ile ama waiache ama walete teknolojia ambayo inafanana zaidi.

Kwa hiyo, chupa za maji kwa mfano kama alivyozungumzia Mheshimiwa Abdullatif Esmail, lakini hivi sasa kuna masharti pia ya kutengeneza chupa za maji, siyo kila chupa inafaa ni lazima iwe chupa ya aina hii, plastiki hii haina madhara kama hii iliyopo hapa kwenye chupa hii ya maji ya Iringa, hii inafaa.

Kuna plastiki nyingine nyembamba ambazo hazifai nazo, kwenye maji zinakatazwa. Kwa hiyo, mwaka jana nakumbuka niliwasiliana na viwanda vinavyotengeneza chupa hizi, chupa zenyewe siyo maji yenye chupa na kuwatahadharisha kwamba hivi sasa kimataifa zinatakiwa chupa za plastiki za aina fulani inayokubalika. Siyo kila aina ya chupa inaweza ikaweka maji na hilo linafuatiliwa hapa kwetu na *TBS.*

Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi tuko macho na kwa kweli hasa hasa nchi moja ambayo nimeiona ina utaratibu mzuri ni Afrika Kusini. Afrika Kusini wamekwishapiga marufuku mifuko yote ya plastiki yote badala yake wakaweka mifuko ya karatasi. Lakini hapa niliona pengine niliona pengine hakuna ulazima kwa sasa hivi tuanze na ile plastiki mbaya, baadaye tukiona jinsi mazingira yatakavyokuwa ndiyo tunaweza tukachukua aina nyingine za plastiki. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, alizungumza juu ya *VAT* nitaizungumza kwa kirefu baadaye, lakini hoja yake tunaitilia maanani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa John Singo, alizungumzia mambo mengi. Moja kubwa ninaloliona ni lile la kushukuru kwa kuwekewa Ofisi za Mamlaka ya Mapato kule Same. Jana

nilisahau kumjibu Mheshimiwa John Singo, alipokuwa anachangia juu ya Ofisi za Mamlaka ya Mapato Mikoani na Wilayani. Kati ya mabadiliko yanayokuja sasa hivi kuanzia mwaka huu kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, ni kwamba tunataka Ofisi za Wilaya za *TRA* ziwe ni *One Top Center* yaani ukienda pale shughuli zako za kodi utazimaliza kwenye ofisi moja. Siyo uwe unarandaranda. Ofisi zote za kodi ndani ya ofisi moja. Hii imekuwa na maana ya kufundisha watumishi kwa sababu ili uweze kufanya hivyo ni lazima uwe ndani ya shirika na aina ya watu wanaweza wakafanya kila aina ya kazi ya kodi. Sasa hivi ilivyo ni kwamba kuna watu waliosomea mambo ya kodi na mapato na waliosomea kodi za *VAT* tu, kuna waliosomea kodi za forodha. Kwa hiyo, mahali pamoja lazima uwe na watu hao hata kama hakuna kazi za kutosha watu watatu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna mabadiliko yatakayotokea kuanzia Januari, 2004 kwamba Ofisi za Wilaya, zitarekebishwa ili kusudi ndani ya ofisi hizo, Ofisi za Wilaya na hata Ofisi za Mikoa, ili ndani ya ofisi hizo kuweko mtu anaitwa *Total Task Men* mtu ambaye habari ya kodi imejaa kichwani kwake, iwe ni hii, iwe ni ile. Hiyo maana yake ni kufundisha watu upya. Hivi sasa tunavyozungumza tunafundisha watu upya ili kuwageuza watu kuwa *Partial Task Men* kuwa *Total Task Men. Task Men* anayejua kidogo kuwa mtoza kodi sawa sawa aliyekamilika. Hawa watakuja kwenye Wilaya zetu na Mikoa kuanzia tarehe Mosi, Januari, 2004. Kwa hiyo, Same na Wilaya zote Tanzania kutakuwa hivyo ofisi zetu zitakuwa za aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala zima la *VAT,* jana nilijaribu kulieleza lakini nirudie tena kwa sababu watu leo ni tofauti kidogo. Nilisema kwamba kwenye bajeti hii, nilikuwa nimeshawishika kuteremsha viwango vya *VAT*. Watalaamu wengi wanafikiri ni vizuri kuteremsha. Lakini nikaogopa vitu viwili.

Kwanza, tumefanya mabadiliko makubwa mno kwenye kodi mwaka huu, hasa upande wa vijijini kufuta kodi, kulipa mishahara ya watendaji wa vijiji, kulipa mishahara ya watendaji wa kata na mambo mengi yale ambayo tumeleta hapa ambayo ni Bajeti kubwa kuliko ilivyowahi kuwa hii miaka mitatu ya mwisho. Nikaogopa nikasema ni vizuri nisiende mbio mno kwa sababu kama mambo haya yasipofanikiwa yote kunaweza kukatokea balaa kwenye upande wa fedha katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili iliyonifanya nikaogopa ni kwamba ukiteremsha kwa asilimia moja tu, umepoteza shilingi bilioni 70. Kama ungetoa kwenye ishirini ukafanya 19 ni shilingi bilioni 70 umepoteza. Ukifanya 18 ni shilingi sabini mara mbili bilioni ni nyingi, kwa hiyo, nikaogopa. Lakini ili mwakani niweze kupata nguvu ya kuamua mambo yafuatayo lazima yawe yameridhisha.

Moja, matokeo ya hatua zote tunazochukua kwenye Bajeti ya mwaka huu yawe yameonyesha mwelekeo wa mafanikio. Siyo lazima yafanikiwe 100% mwelekeo wa mafanikio, hatua zote hizi kuhusiana na mafuta ya petrol, kuhusiana na mambo yote ambayo yametangazwa kwenye Bajeti yangu.

Pili, Watanzania wawe wameanza kuzoea kudai risiti kila anaponunua kitu adai risiti kwa sababu kule ndiko *VAT* ilipo. Sasa hivi kama mnavyojua bado Watanzania hawatoi risiti. Wanauza hawatoi risiti na wanaonunua mali hawatoi risiti. Ni muhimu sana kwa mnunuzi kudai na mtoaji kutoa. Katika Jiji la Dar es Salaam kumefanyika msako mwaka uliopita na mapema mwaka huu wa kufuatilia watu wa namna hii. Kumetokea mafanikio lakini bado kuna kazi ya kufanya. Nilifurahi sana jana kuna Mheshimiwa Mbunge, mmoja alikuwa anasema nadhani Morogoro kwamba wanaona wenye kuuza bidhaa sasa wana ari ya kutoa risiti ni kwa sababu sasa hivi tunawafuatilia na hawajui hasa mtu amekuja kununua kitu ni kachero ama ni mteja tu wa kawaida. Kwa hiyo, wanasema wanataka risiti, wanakupa risiti. Huo ni mwelekeo mzuri na ukiendelea hivyo mimi nitakuwa na nguvu sana za kutelemsha viwango vya *VAT*.

Jambo la tatu, lazima litokee mpango wa mamlaka ya mapato wa miaka 5 ambao nimeutangaza kwenye hotuba uwe umeonyesha ishara za mafanikio, mojawapo ukiwa ni huu Ofisi za Mikoa na Wilaya na mambo mengi niliyoeleza kwenye hotuba yangu. Mpango huo ukionyesha mafanikio nitakuwa na nguvu zaidi. Lakini pia sisi tuna historia ya kuteresha ushuru.

Mimi nafikiri sifa mojawapo za bajeti za toka mwaka 2001 mpaka sasa hivi ni kufuta kodi, tumefuta kodi nyingi na kurekebisha ushuru na ada nyingi. Lakini hatuoni kama hizi zimeteremsha bei za

bidhaa. Mara nyingi sana nafuu nyingi tunazozitoa hazimfikii mlaji kwa maana kwamba ni sasa hivi nimeona kwa mara ya kwanza, wanaotangaza kwenye magazeti wiki hii kwamba baada ya Serikali kupunguza ushuru kwenye *gas* na wao wanapunguza bei, hilo limenifurahisha sana. Ni mara ya kwanza nimeona tena kwa kutangaza kwenye magazeti. Sasa ningependa kuona hivyo mara nyingi na nyingi na nyingi. Kwa sababu wakifanya hivi basi kuna mazingira mazuri ya watu kununua vitu zaidi na kulipa ushuru wa *VAT. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni yale niliyoyaeleza jana kwamba katika Afrika Mashariki kwa sababu anaelekea viwango vyao vya wenzetu katika Afrika Mashariki viko chini ya sisi Tanzania. Hatuna namna lazima tutateremsha huu ushuru. Mimi kinachonisumbua ni *timing,* je, Januari, je, Julai, je, lini? Hilo naomba mniachie, watalaam tunaliangalia kwa makini na natumaini kwamba itafika siku tutaliamua, lakini hatuwezi kukawia kama walivyosema baadhi ya Wabunge zaidi lazima tutaamua mapema iwezekanavyo.

Kuhusu fidia Serikali za Mitaa. Mimi nimemsikiliza Mheshimiwa Paschal Degera, hasa kwa makini. Lakini nirudie niliyosema kwamba zaidi ya asilimia 90 ya mishahara inayolipwa vijijini ni fedha kutoka Serikali Kuu, zaidi ya asilimia 90 ya mishahara ya huko kwenye Halmashauri zetu ni fedha kutoka Serikali Kuu kama Elimu, Maji, Afya, Barabara, *HIV Aids* ni fedha za moja kwa moja kutoka Serikali Kuu.

Kwa hiyo, mimi sina wasiwasi, yaani sitaki watu wanadhani kwamba sasa itakuwaje. Hivi ninavyozungumza mafungu haya yote yameshakwisha mwezi huu wa saba. Tutaendelea kutoa kwa sababu fedha hizo tunazo kwa sababu ni fedha tulikuwa nazo toka mwanzo hazikutokana na kodi za walipa kodi zile ambazo tumefuta hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo mimi niliite dogo kwa asilimia chini ya 10 ambayo ndiyo ilikuwa inakusanywa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli zao nyingine mbalimbali. Kinachoendelea sasa hivi nini? Kwamba kunafanyika ukaguzi Halmashauri kwa Halmashauri kujua hawa hata pengo lao ni nini maana pengo siyo la kodi zote tulizofuta ni ya zile kodi tulizofuta ambazo kwenye Halmashauri fulani zilikuwa zikilipwa hii ndiyo pengo. Kwa hiyo, hivi sasa tunavyozungumza Halmashauri kwa Halmashauri, Wizara ya Fedha na Wizara ya TAMISEMI tunapitia ili kubaini pengo Halmashauri kwa Halmashauri.

La pili, linaloendelea ni kwamba kama kuna Halmashauri ambazo zilipata Hati Safi ya Hesabu zao *(Clean Certificates)* za ukaguzi kama zilivyothibitishwa na Kamati ya *Local Government* ya Bunge, wale tutawalipa mara moja kwa sababu hesabu zao zimethibishwa. Wale tutawalipa hilo pengo mara moja. Kwa hiyo, tunaomba Halmashauri zile ambazo zinafikiri kwamba mkaguzi amekwishazipiga *tick,* zijitokezea nasi tutazilipa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu, kuna Halmashauri ambazo zina mikataba na mashirika ya nje pengine ni Serikali, Wafadhili wa aina moja au nyingine na katika mkataba huo labda kulikuweko kipengele kwamba Halmashauri, yenyewe ilipe fedha kiasi fulani ili mkataba uweze kuendelea. Kama kuna Halmashauri za namna hiyo, ambazo sasa zimekwamishwa na uamuzi huu zijitokeze na sisi tutawalipia hiyo sehemu ya kwao ambayo ingewezesha mkataba kuendelea kutekelezwa. Tutawalipa sasa hivi wakishatuletea tu barua na uthibitisho wa mkataba tutawalipa sasa hivi wakishatuletea barua na uthibitisho wa mkataba tutawalipia mara moja.

Kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba ikifika mwisho wa mwezi Agosti, hesabu hizi zitakuwa zimekamilika, hali ya kila Halmashauri itakuwa imejulikana na malipo ya fidia kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri yanaweza yakafanywa kila Halmashauri na hali yake itakavyokuwa imejitokeza.

Kwa hiyo, ningependa Waheshimiwa Wabunge, mkirudi majimboni kwenu muwahimize wakurugenzi wenu ili waweze kuharakisha kazi hii ili tuweze kurejea kwenye hali ya kawaida upesi iwezekanavyo. Isipokuwa kwa yale malipo ya Watendaji wa Vijiji na *WEO,* Serikali itaanza kuwalipa mapema mwakani, siyo sasa hivi. Ningependa kutoa ushauri kuwa mabadiliko haya ya kodi na ushuru yaliyotokea ni makubwa na maana ni kwamba Halmashauri sasa ni lazima zibadilike. Kuna kitu kinachoitwa *Local Government Reform.* Mimi nasema sasa *reform* hiyo lazima iwe *restructuring* kwa sababu kama kuna Halmashauri iliyokuwa ikikaa hapa ikatuma mgambo huko kwenda

kukamata kodi na hivi na fedha zinaingia, nafikiri Halmashauri hiyo, haiwezi kufanya kazi sawa sawa kwenye huu utaratibu mpya. Halmashauri katika utaratibu huu mpya maana ni kwamba Halmashauri sasa ndizo zitakazokuwa washauri wakuu kwa vijiji, kwa sababu vijiji vitaendelea kupanga mambo yao, vijiji vitaendelea kuchangisha fedha kwa ajili ya maendeleo, vijiji vitaendelea kufanya mambo ya kwao, ngazi ya kijiji au ngazi ya kata. mshauri mkuu na atakayesaidia ubunifu kwenye tija ni Halmashauri. Kwa hiyo, Halmashauri haziwezi kukaa tena hivi kama Mangimeza lazima ziende kwa watu, Halmashauri lazima zitazame huko, haziwezi kutazama hivi, lazima zitazame huko na ziende. Halmashauri ambayo haitazami na kwenda huko haifai, wala haiko kazini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hili tunalijua kwenye zile Wilaya zina *TASAF* na zile Wilaya ambazo zinajenga shule kwa msingi wa MMEM ni lazima *DC* na Halmashauri waende kule wakakague. Hivi sasa wao watakuwa wakaguzi kuona je, vijiji vinatekelezaje, je, waliokabidhiwa mradi wa *TASAF* au MMEM wanatekelezaje, je, *value for money,* je, kitu gani hiki, wao watapita wakiuliza je, nyingi na kusahihisha ile Wachina wanasema *on the spot guidence.* Hilo neno Wachina walikuwa wanatumia, Halmashauri sasa zitakuwa kazi kubwa ni kukagua na kurekebisha papo kwa papo, *on the spot advise.* Hili ni neno moja walituachia Wakomunisti Wachina neno zuri.

Kwa hiyo, mimi napendekeza na nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu twende kwenye Halmashauri tuwaambia waende kwenye *field* watoke ofisini. Hela hiyo ya kutoka ofisini wakifanyia *coordination* iko kwa sababu kuanzia sasa fedha za Mkuu wa Wilaya anampelekea moja kwa moja. Kwa hiyo, hawezi tena kusema mgao haujafika, *RAS* amesimamisha fedha, wana hela wanapeleka moja kwa moja. Kwa hiyo, wakichanganya za Mkuu wa Wilaya na fedha za Halmashauri waingie kwenye gari moja waende kukagua na kusimamia huko. *(Makofi)*

Lingine nataka kusema nilirudie sana ili watu walielewe juu ya kupunguza kodi na ushuru mbalimbali hakukuwa maana basi watu wajikalie, hapana kumekuwa na maana ya kusema watu sasa wagharimie miradi yao hapo walipo kwa sababu kati ya mambo watu wakaona hizi kodi ni kero ni kwa sababu walikuwa hawaoni matokeo ya fedha walizotoa kama kodi, uhusiano wa kutoa na kuona. Je, madarasa yapo ndiyo, zahanati zipo tulizoambiwa tutajenga ndiyo, mtaro wa maji uko ndiyo, kalvati ipo ndiyo, hiki kingine ndiyo, wakiona hivyo na wenyewe wakiona hivyo na wataendelea kutoa. Kwa hiyo, hawa watu watakuwa wanachangia vitu vya hapo hapo walipo na ndiyo tunataka wafanye, siyo hiyo wakalalamikie mtu aliye kule Wilayani hapana, changieni mradi wenu wa hapo hapo mlipo. Kwa hiyo, mimi naona mkichangia hivyo na wakawekeana masharti vile vile itakuwa ni aina nyingine ya kulazimishana kulipa fedha.

Lakini kwa maendeleo yao hapo hapo na wanaweza kuyaona hapo hapo na kazi ya Halmashauri sasa ni kusaidia *process* hiyo ya hapo hapo walipo, kuchangiana fedha, kusimamia fedha, kuzikagua na mwisho kusukuma maendeleo ya watu yaende kwa kasi zaidi. Hii ndiyo mimi naiona nafasi ya Halmashauri mpya, siyo hizi za kukaa pale kama Mangimeza mnasubiri kodi ije mnatuma hata Mgambo. *No way! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waheshimiwa Wabunge, watakaporudi kwenye Majimbo yao watapata matatizo kidogo. Kuna watu wale waliokuwa wanafaidika na utaratibu wa zamani, hawapendi mambo haya. Hawa ndio wameanza kutembea wanasema ooh, Serikali ilikurupuka. Serikali yenye watu wenye akili, inaweza ikakurupuka?! Hasa ni nani aliikurupusha? Serikali imejileta yenyewe ikafanya yenyewe. Kwa hiyo, hakuna kukurupuka. Jambo hili tumelifanyia utafiti miaka miwili. Jambo hili Waziri wa TAMISEMI kuanzia Januari, 2003 aliliwekea msimamo mpaka wa kuondoa vizuizi barabarani, lakini kuna watu jeuri hawataki kubadilika. Hawataki kumwonea huruma huyu anayelalamika. Wanataka kuendelea na ule Utukufu na Umungu mtu. Kwa hiyo, mpaka wameunda na Askari wa kwenda kukusanya mapato. Nasema wale Mgambo nawasikitikia, watafute mashamba walime. *(Kicheko/Makofi)*

Kama walidhani waliajiriwa kufanya kazi ya Uaskari wa kupambana na wananchi wenzao, nawasikitikia. Sasa watafute mashamba walime kama wengine. Wale wakurugenzi waliodhani kwamba, kazi yao kubwa ndio hiyo ya kutuma Askari, wawaletee kodi nyingine zinazoonekana na nyingine hazionekani na wenyewe waanze kutafuta kazi nyingine kwa sababu muda wao nao ni mfupi.

Wakurugenzi watakaozembea jambo hili kulichangamkia na kuliwekea mambo sawasawa haraka haraka kwa kusingizia eti hela ya Mramba haijafika, nitawashughulikia kikamilifu. Kikamilifu!! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari hii ni lazima ifanikiwe. Habari hii hairuhusiwi kushindwa. Haiwezi kuruhusiwa! Waheshimiwa huko, kama kuna mtu mzembe mzembe hivi aliyelegea ambaye huko Vijijini anaendelea kutoa visingizio mleteni hapa sisi tumshughulikie. Kwa sababu yeye analipwa na Serikali Kuu, hawezi kukaa pale akijisingizia kama bibi kizee, tutamshughulikia aondoke mapema. Haiwezekani! Kwa hiyo, kule tukienda, tunakwenda kifua mbele na ile orodha na kumwambia Mkurugenzi sasa unabadilika unakwenda huko. Mimi nimeshangaa sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni *TRA*. *TRA* imezungumzwa vizuri na kwa namna fulani vibaya. Mimi ningesema tu kwamba, kwa muda mrefu tumejua kwamba kuna watu wachache ambao wameharibu sifa ya Mamlaka ya Mapato na sisi tunawafahamu na wengine tunawajua. Ningependa niseme kwamba, mwezi wa Sita Mamlaka ya Mapato imeanzisha Kikao ndani ya *TRA* kinachoitwa ni Kikao cha Maadili Bora ndani ya *TRA (Ethics Committee)*. Kila Mkoa una hiyo *Ethics Committee* na Makao Makuu kuna *Ethics Committee* ya kusikiliza rufani kutoka Mkoani na kadhalika. Baada ya Makao Makuu kushughulikia malalamiko, maana hizi ni *Ethics Committee* za malalamiko, kama Makao Makuu ikiona kuna hoja *(there is a case to answer)* inapeleka kwenye *Anticorruption Bureau* wakachunguze sasa kwa undani ili kuthibitisha tuhuma za rushwa na mambo kama hayo. Kama wakiona hapana ni jambo wanaloliweza liko katika taratibu zao, wanaamua pale pale Makao Makuu. Kwa hiyo, hivi vikao vimeanza kufanya kazi. Sasa hivi ninavyozungumza wapo watu watatu wamepelekwa kwenye Tume ya Rushwa ili wakachunguzwe kwa undani zaidi. Makaratasi yote na ushahidi wote unapelekwa kule na wale wengine wanachukuliwa hatua za mara moja.

Kuna mfano hapa, Mheshimiwa Naibu Spika wetu amekuwa na tatizo hilo. Toka mwezi wa Nne, makaratasi yamepelekwa kule yashughulikiwe, hata Makao Makuu yashughulikiwe, lakini kuna mtu mmoja ameamua kuyakalia tu, toka mwezi wa Nne. Wiki hii ndio tumekuja kugundua baada ya kumshika koo kabisa akatoa makaratasi kwenye kabati akasema yako hapa. Sasa uliza kitu gani kilitokea? Hakuna maelezo. Yule leo tunavyozungumza tumekwishamchukulia hatua za kinidhamu. Tumegundua jana, leo tunavyozungumza hatua za kinidhamu zimechukuliwa. Hakuna cha msalie Mtume kwenye mambo haya, hakuna! Ningependa wote wanisikie, tumekwishaelewana na Makao Makuu ya Mamlaka, hakuna ndugu wala mjomba, wala shemeji, wala *classmate* wala nani. Pale kuna kazi na utendaji mzuri wa kazi, ndio hoja kubwa na uaminifu na uadilifu.

Kwa hiyo, narudia na niliomba tena jana, Waheshimiwa Wabunge, naomba wananchi waniandikie mimi mwenyewe majina ya watu wanaojulikana kwamba ni wala rushwa popote walipo ndani ya Mamlaka ya Mapato. Waniandikie mimi Waziri mwenyewe kwa jina au kwa cheo, waniambie, hapa kwangu kuna mtu huyu amekula hivi, anakula na fulani, tarehe fulani walikwenda wapi, walifanya hivi, walifanya hivi na ni kiasi gani na mali zake ziko wapi. Kati ya watu tunaochunguza, tumepeleka *PCB* wamchunguze hao niliosema. Mmoja ana mali isiyoeleweka sawasawa ilitoka wapi. Mali hii kwa karani huyu inawezekana? Hebu mchunguzeni aeleze, maana tumemshuku. *(Makofi)*

Kwa hiyo na Waheshimiwa Wabunge nawaomba, tayari jana nimepata majina mawili. Jana nilisema naomba, tayari majina mawili nimeshapata, jana hiyo hiyo. Nawashukuru sana wako hapa, maana mambo haya kwa kawaida hatutoi siri nani kasema. Hatusemi. Lakini kuna Wabunge hapa tayari wameshanipa orodha. Ongezeni hiyo orodha sasa. Ongezeni! Mimi mwenyewe ili kuonyesha *seriousness*, tufagie uchafu. Hii inaitwa *loss luggage*. Tufagie hii ili tubaki na watu sawasawa. Kuna watu wengi ni sawa sawa na masanduku yaliyopotea kwenye *Railway Station,* hao hatuwahitaji. *(Kicheko/Makofi)*

La pili ambalo tunafanya, kuna Idara ambazo tunaanza kuziona zina watu waliochoka sana. Ni watu waliochoka hata ungewafundisha hawawezi kuingiza tena mapya. Kuanzia sasa, tumeelewana na Mamlaka, wanakwenda Vyuo vya Elimu ya Juu. Vyuo Vikuu vyetu, Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa mfano *Arusha Institute of Accountancy,* Dar es Salaam, wote hao na *NBAA* na wengine wote hao, wanatafuta watu wenye alama 'A' na 'B'. wanasema tuna nafasi 20, tunataka kuzijaza na watu wa namna hii. Alama ya A au B. Wale wanafunzi wanawekwa pale, anatafutwa *consultant*, sio wao tena, mtu mwingine wa nje anawahoji wale. Tunataka kutoa hapa watano wakafanye kazi ya Forodha, wawili kazi ya kukadiria mapato, wengine kazi ya *VAT and so on and so forth.* Tuchukue *top note* kwa sababu kazi ya kodi ya

kuleta mapato kwenye nchi ni kazi ya watu ambao bongo zao zinachemka saa 24. Huwezi kwenda kuchukua watu legelege tu, tena waliiba *Certificate* ndio wakaenda huko. Haiwezekani! Tunataka kuchukua *"A+". (Kicheko/Makofi)*

Tena kati ya watu tunaowachunguza kuna mmoja walituambia huyu mtu fulani hapo kwenu cheti chake ameiba. Eeh, kati ya watu walioingia kwenye hii Kamati ya Maadili. Kuna watu wanachunguza vyeti. Watu wametuletea habari, yule tunamfahamu tulisoma naye, cheti chake sio hicho. Tayari tunaye mbaroni. Tunataka kuchukua Watanzania *top note* na kwa sababu tunalipa mishahara mizuri, tunataka hiyo mishahara mizuri walipwe watu hao ndio baadaye wataliendesha hili Shirika. Kila Shirika lazima liwe na aina ya watu ambao baadaye wataliendesha. Lakini wahojiwe kwa utaratibu mzuri na alama zao ni nzuri na kiasi iwezekanavyo, hawa Viongozi wa *TRA* wenyewe wasihoji watu, watafute watu wa nje wawahoji wawaletee alama na wao wachukue. Kwa njia hiyo tutaondoa ile ya kusema upendeleo, ooh, nini na mambo yoyote yale.

Kwa hiyo, hilo ni badiliko lingine kubwa sana ambalo nimekwishaelekeza litekelezwe katika *TRA* na hasa Idara ya Forodha. Wenzangu walioko kwenye Mamlaka hii waelewe kwamba, siku zao zinaanza kuhesabiwa. *Their days are numbered* kwa sababu hawa wametusumbua sana. Ndio ukienda kule *Airport*, ukienda kwenye *long room* ni watu hawa ndio wanatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kukueleza kwamba, hivi sasa tunavyozungumza tunataka kutumia teknolojia ndio maana tunahitaji watu waliosoma kwa viwango vya juu waweze kuelewa hii teknolojia. Hivi tunavyozungumza, pale kwenye Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, ndege inapoingia na watu wanapekuliwa, kuna mtu mwenye *computer* anaona kila anayepekuliwa, kila kinachochukuliwa na kusikia kila wanalozungumza, akiwa Makao Makuu. Sawasawa na inavyofanyika kwenye *Super Market* kubwa Ulaya, wale watu ambao wanaelewa. Kuna mtu anakaa pale anaona kila kitu kinachoendelea na mtambo huo sisi tunao. Ndio maana ukienda pale *Dar es Salaam Airport,* wale watu waliokuwa wanazunguka, Maofisa wangu wa Forodha wamekwishaambaa hawapo tena. Kwa sababu tunawaona, tunawasikia na tunaona wanachofanya. Wamekwishaambaa. *(Kicheko)*

Hivi tunavyozungumza tunahamia *Long Room*. Kama mnavyojua kuna washabiki wengi na watu wengi wanazunguka pale *Long Room*. Pale *Long Room* nawaambia, mkinipa mwezi mwingine mmoja watu wale watakuwa wameambaa. Hakuna! Ili mteja azungumze na mtumishi na sisi tunamsimamia tukiwa kule Makao Makuu kwenye *Command Post*. Kwa hiyo, haya mambo tunayolalamikia hapa, mimi nawahakikishieni tu mje mniambie nilisema uwongo, labda hiyo ndio tutashindana. Lakini haya ninayozungumza yako. *(Kicheko/Makofi)*

Halafu tunaingiza mtambo wa kupiga picha kwenye makontena kule ndani. *Container* limekuja hili, kule ndani picha inapigwa kama wanavyofanya kwenye sanduku lako pale *Airport*, tunaona kila kitu kilichoko mle ndani. Sasa hivi unajua kwenye makontena yale wanatafuta watu wafupi wanaingia kule ndani wanachokonoa. Hii ni ajira moja nzuri kwa watu wafupi. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini muda si mrefu, hakuna mfupi atakayepata kazi hiyo wala mrefu. Tunatumia mitambo tu kuangalia kule ndani kwa picha kujua kuna nini. Kwa hiyo, nazungumzia habari za *modernization* ya *customs function,* tunai-*modernize*. Nina hakika kabisa kodi sasa itaanza kumiminika maana hakuna majadiliano, hakuna mazungumzo. Sisi kwa kuwa tutakuwa tunamwona mtu kwenye picha wakizungumza pale kinyume cha taratibu, maana unaambiwa jinsi ya kumshughulikia mteja. Tunaanza hata kukushuku tu. Mbona tumeona umekaa muda mrefu na yule mtu kulikuwa na nini mnazungumza pale? Kwa nini muda ule ulikuwa mrefu zaidi? *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Haijawahi kutokea! *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Kwa hiyo, tutakuwa tunafanya kazi kwa mtandao na *computer* na kwa sababu hiyo tutapunguza ucheleweshaji mkubwa uliokuwa unalalamikiwa hapa, kitu kinachukua muda mrefu, kinachukua miezi, huu upuuzi wote utakwisha. Ni mambo ambayo kwa kweli tumerithi. Ni mambo ya kizamani na tunatumia teknolojia kuyafutilia mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba, jana niliposikia Waheshimiwa Wabunge fulani wakiisifia Serikali hii ya Awamu ya Tatu, kwa kazi nzuri ya kutengeneza lile daraja la Rufiji, nilifurahi sana. Mimi mwenyewe nilifurahi sana kwa sababu watu wamepata daraja. Lakini zaidi nilifurahi, kwa sababu nafikiri hamkujua nilivyokuwa nataabika na lile daraja. Ukichelewa kupeleka malipo kule Kuwait, ukichelewa siku moja tu, ile adhabu ni fedha nyingi. Ni adhabu ya pesa, halafu wanakusimamisha. Kwa hiyo, kila siku sala ya asubuhi ilikuwa hela ya daraja iko sawasawa? Hela ya daraja imekwenda? Daraja, daraja, wimbo! Kwa hiyo, hii ni kazi moja nzito ambayo imenitoka na mimi nimefurahi. Sasa kilichobaki, tujenge uchumi. Daraja ni la kujenga uchumi, sio la kufurahi tu tuna daraja. Tujenge uchumi sasa ili kusudi uchumi huo ulipie lile daraja. Lazima uchumi utakaoibuka ulipie gharama za hilo daraja. Hii ndio rai yangu. Kufurahi ni sawa, lakini kufurahi bila uchumi wenyewe kufurahi, sasa tunafurahia nini? *(Kicheko/Makofi)*

Juzi nilipita nikasikia mtu anasema ooh, sisi tumefurahi. Ananiambia mtu mmoja. Mheshimiwa Waziri wetu mzuri tumefurahi umetupunguzia kodi. Nikamwuliza, shamba lako limeongezeka mara ngapi kutokana na kupunguziwa kodi? Akasema aaha, hapana angalau nimeanza kufikiria kuoa mke wa pili. *(Kicheko)*

Sasa hilo sio kusudi bwana! Kama ulitaka kuongeza nguvu kazi sawasawa, mimi sina matatizo, lakini ongeza uchumi. Kama mke wa pili atakusaidia kuongeza uchumi sawasawa, lakini sio uzidi kulala chali saa sita ya mchana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie tu kwa kusema kwamba, kwa kweli Muswada huu nimeuleta ili tuendelee kuboresha njia zetu za kisheria za kufanya kazi tupate nguvu ya kutekeleza zile hoja ambazo zimetokana na Bajeti. Nataka kuwahakikishia kama kawaida kwamba, kazi hii ambayo imekwishaanza, sasa itaanza kwa kasi inayotakiwa na kwa nguvu inayotakiwa, kwa mujibu wa sheria ambayo Waheshimiwa Wabunge watakuwa wamepitisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria Ulisomwa Bungeni Mara ya Pili)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003
(The Finance Bill, 2003)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada una vifungu vingi sana. Sasa tunachoweza kufanya hapa, tupitie zile sehemu ambazo nadhani ziko 18. Nafikiri tupitie sehemu tu, tunachangia eneo lolote lile.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 32

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye Ibara ya 32 (a) ukurasa wa 40, tunapendekeza hiyo Ibara ya 1(A) kubwa ambayo inasema, *"tax rate on income of an individual"* halafu inaanza kutoa *business turnover* halafu *column* ya pili *tax payable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza yote hiyo iondolewe na badala yake tuweke maneno mapya ambayo yanafafanua vizuri viwango vya *turnover* ambavyo mlipa kodi atapaswa alipie. Nilikuwa nimeipatia meza nakala ya marekebisho haya, ili sasa yaingie kwenye *Hansard* napendekeza tuseme hivi: "*By deleting paragraph one (a) appearing under head B and substituting for it the following: Business turnover where the gross turnover is less than three million shillings per annum, tax payable Shillings twenty thousand where the gross turnover is Shillings three million and less than seven million per annum. Tax payable Shillings 50 thousand Shillings where the gross turnover is Shillings seven million and less than Shillings 14 million per annum. Tax payable Shillings 165 thousand where the gross turnover is Shillings 14 million and less than twenty million per annum. Shillings three hundred and eighty five thousand*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nimemaliza hapo. Niseme tu, kwenye eneo hilo hilo kwenye *printing* yalikuwa yamerukwa maneno ambayo ni ya msingi kidogo yanahusu Ibara ya 58(b) *roman*...

MWENYEKITI: Mheshimiwa *AG* hatujafika kwenye kifungu hicho. Labda tukifika baadaye.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Hapana. Iko pale pale, walikuwa wamekiruka katika *printing*. Tumegundua jioni hii.

MWENYEKITI: Haya. Endelea na maelezo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Waheshimiwa Wabunge, ambao walikuwa na hiyo karatasi, Muswada kama ulivyochapishwa mwanzoni, kwenye eneo hili la Ibara ya 32, kabla ya pale sasa kulikuwa na Ibara moja ambayo tulikuwa tunasema na yenyewe ibadilishwe. Ni ya msingi sana kwa sababu inahusu misamaha ambayo inatolewa kwa Taasisi za Kidini na pale walikuwa wameandika magari ambayo yatapewa msamaha huo kwa kusema yasiyozidi *CC 3000.* Lakini ili twende sawasawa na jinsi sheria inavyosema, tunapendekeza kwa idhini ya Kamati hii, eneo hili sasa lisomeke kama ifuatavyo:-

Naomba maneno haya ndio yaingie kwenye Hansard: *"In the case of religious organization for the advancement of religion, if the relief is on motor vehicles described in tariff heading number 87.03 and*

HS codes 8702.20.10 and 8702.90.20 under the first schedule of the custom tariff act 1976, such vehicles shall note exceed 3000 CC." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hizo *amendments* tupatiwe kama *schedule of amendments*. Nakala zikapigwe *photocopy*, sisi tumepitisha hii, sasa tuone haya maandiko. Ilitakiwa itolewe mapema hii, nilikuwa natafuta kifungu cha kanuni bahati mbaya aliwahi katikati. Ahsante nashukuru.

MWENYEKITI: Nafikiri itafanyika. Naomba Wabunge wapate hizo *schedule of amendments*. Ibara hiyo imekwishaafikiwa. Kwa hiyo, tunaendelea.

Ibara ya 33
Ibara ya 34

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 35

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulizie kuhusu ibara ya 35 ya hiyo *part 10.* Hii imependekeza kuunganisha mwaka wa Serikali za Mitaa na ule wa Serikali Kuu. Sasa naomba nipate maelezo, haya mapendekezo yameanza kutekelezwa lini; ni Julai, hii ya mwaka huu au yanaanza lini? Naomba maelezo.

MWENYEKITI: Hiyo ni ibara ya 35, Mheshimiwa Waziri, maelezo. Kama hujaelewa anaweza kujieleza tena, ibara ya 35

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa. Marekebisho haya yanaanza mwaka huu. Nilivyoelewa *harmonization* ya miaka hii ilikuwa ianze mwaka huu na ikifika mwakani itakuwa imeshaingia *full scale.* Mwaka huu ni wa maandalizi.

MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nipo katika sehemu ya kumi ibara ya 36, ambayo inapendekeza kuongeza *schedule,* shabaha yake ikiwa ni kupunguza kodi. Kama nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri, alisema na mimi nakubaliana naye kwamba, kila mara Serikali inapopunguza kodi lakini haiwafikirii walengwa, Wafanyabiashara wanaendelea kutoza bei ya juu. Sasa lakini Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, yeye anashangaa na ataendelea kushangaa. Sasa mimi ninavyomfahamu Mheshimiwa Mramba, ambaye nimefanya naye kazi mahali pengi na ushupavu wake atakubaliana na mimi kwamba, Serikali haiwezi kuendelea kushangaa bali iunde mkakati wa kuwashughulikia hawa kama vile alivyokuwa ameeleza katika maeneo mengine? *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Nakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge na ningemwomba tuwasiliane ili aendelee kunipa maarifa na uzoefu wake ili kazi hii ifanyike vizuri zaidi.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67

(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 68

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoangalia ibara ya 68 (ii), Kingereza kinanipa matatizo na nikasema nitasoma kuona utata uko wapi. *Where the Regulations are to be made,* hayo ni marekebisho yake. *Where the Regulations are to be made inversion to which consultation are required in accordance with Sub-Section One. Such a consultation shall be unified even for being writing to have been made by the Minister other than the Minister and that concerned to their progression having produced as such.*

Sasa, *having made by the Minister other than the Minister.* Siamini kama ni Kingereza kinaweza kutusaidia kwenye mambo ya kodi. Hakiwezi kutusaidia, maana ni lazima tuwe *clear* kabisa, mlipa kodi ajue anafanya nini na kama yuko vegi vegi inaleta hofu, pia atakayetafsiri hakupata chochote. Ndiyo wasi wasi wangu. *We must be very clear* hapo haipo *clear.* Nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nia ni nini, maana Waziri amerudia mara mbili? Huyo Waziri ni yupi, ama ana maana ya kwamba najaribu kutoa tafsiri, *where other Regulations to be made prevention to which consultation are required according with Sub-Section One, such a consultation shall be unified in writing to have been made by a person other than a Minister,* pengine hai- *make sense* kwangu. Sasa kama inajirudiarudia hivi, tunataka *carriage* ijirudie pia kwenye ibara ya 70 tunakokwenda. Ningependa kupata mawazo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa tatizo la Mheshimiwa Mkono. Kusema kweli mchana sikujua kwamba, ni yeye alikuwa ameniandikia. Kwa sababu sikuwa nimeona hiyo note imetokea upande gani. Lakini ukweli ni kwamba, kwenye hizi Sheria, kifungu hicho hicho ambacho Mheshimiwa Mkono amekisoma, kinafanana na huyo mtoto wake wa pili katika sehemu ambayo hatujafika. Kwa hiyo, ninapojibu sasa hapa nitakuwa najibu kwa yote mawili.

Ni kweli kwa sababu Mheshimiwa Mbunge au mwananchi ambaye hana hizi Sheria mbili hawezi akaelewa haya maneno yana maana gani. Sehemu ya kwanza ya Waziri anayetajwa kwa mujibu wa Sheria zinazosimamia Tawala za Mikoa kwa upande wa Halmashauri za Miji na Jiji na upande wa Halmashauri za Wilaya, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amekasimiwa na Bunge mamlaka ya kuweza kutengeneza *By-Laws.* Ndiyo anatajwa *other than the Minister*.

Sasa huyu ametajwa, Waziri ni nani katika Sheria hizo mbili? *Act No. 7* na *Act No. 8* za 1982. Huyo ni Waziri wa TAMISEMI ndiye anasimamia majukumu hayo.

Lakini Sheria hiyo inamwambia: "Unapotengeneza *Bylaws* hizi Kanuni ndogo ndogo zinazosimamiwa na Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji, kuna maeneo fulani lazima kama unasema unataka kutengeneza *Bylaws* mathalan kuhusiana na magogo yatakayokatwa na kutozwa ushuru kutoka katika Hifadhi za Serikali au maeneo ambayo yako katika himaya ya Halmashauri, unapaswa ushauriane na Waziri anayesimamia misitu."

Sasa pendekezo hapa Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, tunataka tuone hao Mawaziri wahusika, Waziri wa Serikali za Mitaa, anayeshughulikia Serikali za Mitaa na yule anayeangalia misitu kwamba kweli wameshauriana na zile *By-Laws* sasa zinapoandaliwa ziseme wazi kabisa kwamba, *By-Laws* hizi nimezi-*approve* mimi kama Waziri wa TAMISEMI, baada ya mashauriano na Waziri mhusika.

Hii ndiyo inayotafutwa hapa kwamba, pawepo kweli na uthibitisho kwamba mashauriano kama yanavyotakiwa na Sheria kweli yamefanyika.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 69
Ibara ya 70

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)
(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2003
(The Finance Bill, 2003)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2003 *(The Finance Act, 2003),* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujawaita Mawaziri wanaohusika, haya Maazimio yanatakiwa Wabunge kutoa mawazo yao. Sasa inawezekana tulichelewa kupata *Order Paper* ya jioni, kama kuna watu wanataka kuchangia, basi walete sasa hivi nina wachangiaji wawili tu hapa, wasije wakasema hawakuelewa.

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kuomba na Kupata Msaada unaohitajika katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai
(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance in Criminal Matters)
Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Masuala ya Sheria
(The SADC Protocol on Legal Affairs)

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Utaratibu wa Kurejesha Wakosaji au Watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition)*

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawalan chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, ambaye amefanya kazi kubwa za kuzichambua Itifaki tatu za Jumuiya ya Maendeleo ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika, zinazohusu:-

- Masuala ya Sheria *(The SADC Protocol on Legal Affairs).*

- Kupeana misaada katika uendeshaji wa Mashauri ya Jinai *(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance in Criminal Matters).*

- Kuhusu utaratibu wa kurejesheana Wakosaji au Watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition).*

Nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika hauna haja ya kusisitizwa. Ni silaha kubwa kwa maendeleo yetu ya kiuchumi na kijamii katika mazingira ya leo ya utandawazi. *SADC* ilianzishwa tarehe 17 Agosti, 1992 pale viongozi wa Kusini mwa Afrika, walipopitisha Azimio huko Windhoek, Namibia, pamoja na kusaini Mkataba wa Jumuiya hii. Ibara ya 21 ya Mkataba iliainisha maeneo mbalimbali ya ushirikiano na ibara ya 22 iliruhusu kufikiwa kwa Itifaki mbalimbali.

Kuainisha maeneo mengine ya ushirikiano. Tangu kuanza kwake *SADC* imekuwa ikipanuka kwa namna ya kuongezeka idadi ya wanachama na majukumu inayoyatekeleza. Kutokana na kukua au kupanuka huko kwa *SADC,* mambo mengi yamejitokeza ikiwa ni pamoja na:-

Asasi zake nyingi kuhitaji mwongozo na ushauri wa kisheria wakati wote. Hivyo, kuhitaji chombo cha kutoa ushauri huo. Itifaki kuhusu masuala ya Sheria imelenga kuanzisha rasmi chombo cha kutoa ushauri huo.

Pili, fursa nyingi za raia wa nchi hizi kuingia katika nchi nyingine. Wapo wenye kutumia vibaya fursa hiyo, wao huitumia fursa hiyo kujificha au kuficha mali zinazohusika na uhalifu uliofanywa katika nchi hizo nyingine. Hali hii imesababisha kuhitajika utaratibu wa nchi za *SADC* kupeana msaada katika

mashauri mbalimbali ya jinai na pia kurejesheana watuhumiwa na mali ili jumuiya isitumiwe kama maficho ya wahalifu.

Itifaki za *SADC Protocol Mutual Assistance in Criminal Matters* na *SADC Protocol on Extradition* zimelenga kusudio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona umuhimu wa kuwepo Itifaki hizo, tarehe 7 Octoba, 2000 na tarehe 3 Octoba, 2002 Viongozi Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika katika mikutano yao waliweka saini Itifaki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki kuhusu masuala ya Sheria inaanzisha Kamati ya Mawaziri yenye kujumuisha Mawaziri wa Sheria na Wanasheria Wakuu wa nchi za *SADC* kama chombo cha kuwashauri Viongozi Wakuu wa nchi katika masuala ya Sheria na pia kama mhimili wa kufikiwa malengo ya Sekta ya Sheria katika nchi za *SADC* ambayo ni:-

(a) Sekta ya Sheria kutoa msaada wa kisheria kwa Jumuiya ya *SADC.*

(b) Sekta ya Sheria kutoa msaada wa kisheria kwa Sekta zingine za *SADC.*

(c) Kuzisaidia nchi zilizoridhia Itifaki ili kujenga uwezo wa kitaalam wa kisheria.

(d) Kuwezesha utekelezaji wa ushirikiano *(Mutual Assistance).*

Nyingine ni kuandaa malengo na mikakati ya pamoja. Kuendeleza na kuimarisha utaratibu wa kushughulikia mashauri ya jinai na madai na la mwisho, kuanzisha na kuendeleza utaratibu wa kubadilishana habari na tafiti za kisheria.

Itifaki kuhusu kupeana misaada katika uendeshaji wa mashauri ya jinai, umelenga kuziwezesha nchi wanachama wa *SADC* kuimarisha kiwango cha kusaidiana katika mambo mbalimbali. Kila nchi mwanachama inatakiwa kutoa msaada wa kisheria utakaohitajika na nchi nyingine mwanachama. Hivyo, nchi mwanachama ziko huru kuomba na kupata msaada unaohitajika katika upelelezi wa makosa ya jinai kama uhujumu uchumi, rushwa, ukwepaji kodi, *money laundering,* ushuru na forodha na kadhalika. Uendeshaji wa kesi za jinai, kutoka katika Mahakama ama mamlaka nyingine yenye uwezo huo, kuhoji mashahidi, upekuzi na kuwasilisha hati.

Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa na Itifaki hii ni pamoja na yafuatayo:-

Itifaki imetaja mazingira ambayo nchi inayoombwa *(Requested State)* inaweza kukataa kutekeleza maombi ya nchi inayoomba *(Requesting State).* Ombi laweza kukataliwa lote au sehemu yake. Mazingira hayo ni pamoja na kitendo kinachohusika kuwa siyo kosa la jinai katika nchi inayoombwa. Pili, makosa husika kuwa ni yenye mwelekeo wa kisiasa. Tatu, kama mhusika ameonekana hana hatia na kuachiwa katika nchi inayoombwa na pale ambapo utekelezaji wa ombi unaweza kukiuka Katiba, Itifaki imeelezea nini kinatakiwa kuonyeshwa au kuainishwa katika maombi ya nchi inayoomba, kwenda nchi inayoombwa. Hayo ni pamoja na kuelezea msaada unaoombwa, sababu za maombi na aina ya upelelezi, uendeshaji wa ushauri unaoendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Itifaki utaratibu wa kurejesheana wakosaji au watuhumiwa, ni vema tukumbuke kuwa hadi sasa tunayo Sheria Na. 15 ya mwaka 1965 kuhusu suala zima la kurejesheana wakosaji au watuhumiwa na nchi ambazo tunayo makubaliano ya aina hiyo. Itifaki husika haiingilii Sheria hiyo, bali itawezesha kuimarisha utekelezaji wa sheria hiyo na sheria za aina hiyo katika nchi nyingine.

Itifaki hii imelenga kuweka makubaliano yaliyotarajiwa katika sheria yetu kwa nchi zote za *SADC.* Kwa mujibu wa Sheria yetu, kurejesheana huko kutazingatia masharti mbalimbali kama yalivyoainishwa katika makubaliano husika. Kwa upande wa Itifaki hii imeainisha mambo ya kuzingatiwa kuwa ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kila nchi mwanachama inatakiwa kutoa msaada, kurejesha wakosaji, watuhumiwa watakaohitajika na nchi nyingine mwanachama kwa kuzingatia Sheria zake husika.

(b) Itifaki imeainisha makosa ambayo yatahusika kuwezesha mtu kurejeshwa, haya ni makosa ambayo katika nchi husika mtu akipatikana na hatia ataweza kuadhibiwa kwa adhabu ya kifungo cha aghalabu mwaka mmoja.

(c) Itifaki imeainisha mazingira ambayo yakijitokeza nchi inayoombwa lazima ikatae kumrejesha mhusika nayo ni:-

(i) Pale ambapo maombi ni kwa sababu za kisiasa;

(ii) Pale msingi au chimbuko la mashtaka kuhusika, umejikita katika ukabila, udini, rangi ya mtu, Taifa la mtu, eneo mtu atokako. Mawazo ya kisiasa, jinsia au nafasi ya mtu;

(iii) Kama tayari ipo hukumu iliyokwisha kuamuliwa;

(iv) Kama mhusika alishapewa msamaha kwa kushtakiwa au kuadhibiwa kwa kosa husika ama kwa msamaha au kupita muda;

(v) Kama mhusika ataweza kupewa adhabu ya kuteswa, kudhalilishwa au siyo ya utu; na

(vi) Kama katika nchi inayoomba, mhusika amepewa adhabu bila ya kuwepo na bila kuwa na taarifa ya kutakiwa na pia hatapata fursa ya suala husika kusikilizwa upya naye akiwepo.

(d) Itifaki inaainisha mazingira ambayo nchi itakuwa na hiari ya kukataa kumrejesha mkosaji au mtuhumiwa nayo ni:-

(i) Pale mtuhumiwa anapokuwa raia wa nchi inayoombwa, nchi hiyo yaweza yenyewe kuchukua hatua kama mashtaka husika yapo Mahakamani katika nchi iliyoombwa;

(ii) Pale kosa husika linapokuwa na adhabu ya kifo, inabidi kupatikane uhakikisho kuwa iwapo adhabu hiyo itatolewa haitatekelezwa;

(iii) Pale ambapo kosa husika halikutendeka katika nchi inayoomba au inayoombwa na Sheria za nchi iliyoombwa hazilifanyi kosa lililotendeka katika mazingira hayo kuwa kosa la jinai; na

(iv) Pale nchi inayoombwa itaona kuwa kumrejesha mhusika inakiuka misingi ya utu kama vile umri au afya ya mhusika.

(e) Itifaki inaainisha njia za mawasiliano katika maombi ya aina hii, inataka iwe kwa maandishi na kwa kupitia njia za Kibalozi, mawasiliano baina ya Wizara ya Sheria au Mamlaka nyingine, inataka makabrasha yote husika yawe katika lugha inayotumika au inayokubaliwa na nchi inayoombwa.

(f) Itifaki inaainisha mazingira ya nchi kuomba amri ya mtu kukamatwa. Nchi iliyoombwa itaamua maombi ya aina hiyo kwa mujibu wa Sheria zake.

(g) Itifaki inaainisha mambo ya kuzingatia pale nchi inapopata maombi kutoka nchi zaidi ya moja ya mtu kurejeshwa katika kila moja ya nchi hizo.

(h) Itifaki inaainisha wazi kuwa mali zilizo katika nchi iliyoombwa zinazohusika na utendaji wa mkosaji aliyerejeshwa na zinazoweza kuhitajika katika kielelezo nazo zitarejeshwa katika nchi husika.

(i) Itifaki inaweka wazi kuwa nchi yoyote husika yaweza kupendekeza marekebisho ya Itifaki kwa utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki zote tatu zina Ibara zinazoelekeza nchi wanachama kuridhia kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya kila nchi. Nchini Tanzania, Ibara ya 65(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imelipa Bunge Mamlaka ya kujadili na kuridhia Mikataba ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa na nchi.

Baada ya maelezo hayo, napenda kuliomba Bunge hili Tukufu lijadili, kuzichambua na kisha liazimie kuridhia Itifaki zote tatu za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizoko Kusini mwa Afrika kuhusu masuala ya Sheria *(The SADC Protocol on Legal Affairs),* kuomba kupata msaada katika uendeshaji wa mashauri ya jinai *(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance in Criminal Matters)* na utaratibu wa kurejesheana wakosaji au watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition),* kwa kupitisha Maazimio matatu yafuatayo: Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kuomba na Kupata Msaada unaohitajika katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai *(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance in Criminal Matters),* Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Masuala ya Sheria *(The SADC Protocol on Legal Affairs)* na Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Utaratibu wa Kurejesha Wakosaji au Watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. RAYNALD A. MROPE - (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Maazimio ya kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* kuhusu utaratibu wa kurejesheana wakosaji au watuhumiwa, masuala ya Sheria na kupata msaada unaohitajika katika uendeshaji wa mashauri ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Maazimio ya Kuridhia Itifaki yaliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Harith Bakar Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Maazimio hayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizomo Kusini mwa Afrika kuhusu utaratibu wa kurejesha wakosaji au watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition)*.

Pili, Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizoko Kusini mwa Afrika kuhusu Masuala ya Sheria *(The SADC Protocol on Legal Affairs).*

Tatu, Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizoko Kusini mwa Afrika kuhusu Kuomba na Kupata Msaada unaohitajika katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai *(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance in Criminal Matters).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Maazimio haya yana maudhui yanayofanana, Kamati ilijadili kwa pamoja na hivyo maoni pia yatawasilishwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuchambua Maazimio haya kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Kigunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Rosemary H. K. Nyerere, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Mwanne I.

Mchemba, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalifan na Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mjumbe ambaye anasoma taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inahudumiwa na Makatibu ambao ni Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Makatibu hao kwa kuihudumia Kamati vizuri na napenda nimshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka M. Mussa, kwa kuiongoza Ofisi yake vizuri. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa kuwasilisha Maazimio haya mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba, umuhimu wa Itifaki hizi unatokana na ukweli kwamba, kutokana na kukua na kupanuka kwa *SADC* mambo mengi yamejitokeza ikiwa ni pamoja na kusababisha asasi nyingi za *SADC* kuhitaji mwongozo na ushauri wa Kisheria wakati wote na hivyo kuhitajika chombo cha kutoa ushauri huo. Pia baadhi ya raia wa nchi hizi hutumia vibaya fursa ya kuingia katika nchi nyingine kwa kujificha au kuficha mali zinazohusika na uhalifu katika nchi nyingine na hivyo kuhitajika utaratibu wa nchi za *SADC* kupeana msaada katika mashauri mbalimbali ya jinai na pia kurejesheana watuhumiwa na mali ili Jumuiya ya *SADC* isitumiwe kama maficho ya uhalifu na wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imeridhika na sababu zilizotolewa ili kuonyesha umuhimu kwa Tanzania kuridhia Itifaki hizi na ninaliomba Bunge lako Tukufu liyakubali na kuridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Pamoja na kukubali Itifaki hizi ziridhiwe na Bunge lako Tukufu, kwa kuzingatia umuhimu wake, Kamati inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe katika utekelezaji:-

(i) Serikali na Taasisi husika ziwe makini katika kushughulikia maombi ya kurejeshwa kwa watuhumiwa ama wakosaji hususan yale yanayotolewa kwa njia ya Posta kwani wahalifu wa Kimataifa wanaweza kutumia njia hii kuwaonea watu wengine kwa manufaa yao.

(ii) Haki ya mtuhumiwa kukubali *(consent)* kurejeshwa katika nchi inayoomba arejeshwe izingatiwe kabla uamuzi huo haujafanyika.

(iii) Utekelezaji wa Itifaki hizi ufanyike kwa makini ili kuepusha watu kuonewa kwa sababu mbalimbali zikiwemo sababu za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni haya, napenda kurudia kusema kuwa, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala haina pingamizi lolote na Itifaki hizi na ninaliomba Bunge lako Tukufu, liyajadili hatimaye kuyaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Itifaki hizi na ninaunga mkono hoja hii moja kwa moja. *(Makofi)*

MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Tanzania kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, kuhusu Masuala ya Sheria pamoja na Utaratibu wa Kurejesha Wakosaji au Watuhumiwa, pamoja na Upatikanaji wa Msaada katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Kambi ya Upinzani haina sababu yoyote ya kupinga kuridhiwa kwa Itifaki hizi. Lakini kama ambavyo tumewahi kuelezea huko nyuma na kutoa maoni yetu kuhusu Itifaki na Mikataba tunayoiridhia ni kwamba, tunakuja kukamilisha zoezi ambalo linakuwa limekwishafanywa na wakubwa kwa kumwaga wino tayari. Kwa hiyo, Bunge letu hapa ni kuja kupiga mihuri *(Rubber Stamping),* hata kama kuna kasoro ambazo zinabainika wazi ndani ya Itifaki zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba tuige mfano wa wenzetu ambao inaonekana kwenye Itifaki hizi bado hawajasaini. Tuna uhakika nchi hizi si kwamba, hazijasaini tu kwa sababu hazikupelekewa karatasi hizo kusaini au hazikushiriki kwenye vikao hivyo. Tunaamini zinafanya *research* ya kutosha ili kuhakikisha kwamba, wakija kusaini wanakuwa wamepata maoni, ridhaa na baraka kutoka kwa wananchi toka katika nchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutambua kwamba, nchi zenyewe zinazoridhia Itifaki hizi zinatofautiana kwa namna moja ama nyingine katika kuthamini, kukubali na kusimamia kwa dhati Utawala wa Sheria ndani ya nchi zao, kukubali Itifaki hizi ukiacha kando malengo halisi ya kushawishi misaada ya wafadhili, kuvutia wawekezaji kuja kuchota raslimali zetu, kuongezea na kutanua wigo wa kutambua na kukipa nafasi kile kitu kinachoitwa utandawazi, bado Itifaki hizi zinahitaji kuangaliwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inasemekana hivi sasa kuna kitu kinachoitwa *The Ruling Party's Club* na mambo yanayozungumzwa na kupangwa na wahusika si rahisi kuyaelewa isipokuwa wao kwa wao. Kuna wasiwasi kwa kutumia Itifaki kama hizi, baadhi ya watu wakanyimwa haki zao za Kisheria za Kimataifa mfano mtu kupata hifadhi za ukimbizi wa kisiasa kama ilivyotokea wakati wa sakata la Mwakenya pamoja na kundi la Makigii na wenzake mwaka 1983. Maadam inazungumzwa kabisa katika Itifaki hizi kwamba, nchi zenyewe husika ndizo zinaweza zikatafsiri makosa yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba, mfumo wa Sheria za nchi hizi haufanani, kutekelezeka kwa Itifaki hii huenda kukawa kuna wasiwasi au isitimize malengo yaliyokusudiwa. Ukiangalia Mikataba yenyewe au Itifaki zenyewe, baadhi ya nchi zilizosaini bado zina mtafaruku wa ndani mfano nchi za *Congo DRC,* wamesaini Mkataba wa kubadilishana watuhumiwa lakini hawajasaini Mkataba wa *Legal Affairs.* Hii inatupa wasiwasi kwamba, wamekuwa wepesi kusaini Mkataba wa kurudishiana watuhumiwa ili iwe rahisi kuwashughulikia Wakongo wanaoipinga Serikali iliyoko madarakani lakini wanaona kigugumizi kusaini Mkataba wa Itifaki za Kisheria ili wasijifunge na kuumbuka mbele ya Mataifa yanayoheshimu Utawala wa Sheria. Hata hivyo, tunapongeza uanzishwaji wa kuwepo Itifaki ya Kuomba na Kupata Msaada unaohitajika katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai. Tunapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia upanuliwe wigo kwa kutumia Kanuni za Itifaki hii kwa kuruhusu Mawakili toka nchi moja kwenda kusimamia na kuendesha kesi nchi nyingine, iwapo ushauri huu wa Kisheria utaweza kuhitajika hasa kwa watuhumiwa wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujafika huko, ni vema pia tukaanzia kwenye maeneo yetu sisi wenyewe ili kujenga msingi ulio mzuri wa kutekeleza Itifaki yenyewe. Mfano hivi sasa si Mawakili wote wanaoruhusiwa kusimamia kesi zinazofunguliwa kwa upande wa Zanzibar, endapo wanatokea upande wa Tanzania Bara na vivyo hivyo kwa upande mwingine. Mfano mzuri kuna baadhi ya Mawakili waliopo hapa hapa ambao wamewahi kuonja joto hiyo ya jiwe. Ni vizuri mambo kama hayo yaliyomo ndani ya uwezo wetu sisi wenyewe tukayarekebisha ili tuweze kutoa mwanya wa kufanya makubwa kama haya ya *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inaonekana siku zote Tanzania tunakuwa wepesi wa kuingia kichwa kichwa ndani ya Mikataba na Itifaki kuliko wenzetu. Je, tunafanya utafiti wa kutosha kutambua athari na faida za muda mfupi na muda mrefu au tunafanya mambo ki-*fashion? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri kuwa, iwapo Bunge linaweza likaletewa Mikataba ya kuridhia Itifaki, tena Mikataba yenyewe au Itifaki yenyewe ambayo

imesainiwa na wakubwa wa nchi, ni kitu gani kinashindikana katika kuleta Mikataba mingine ambayo Serikali ina saini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Nashukuru sana. *(Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hakuna Mheshimiwa Mbunge yeyote, aliyeomba kuchangia katika hoja zote tatu. Kwa hiyo, namwita mtoa hoja, ili ajumuishe hoja yake, wamechangia Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ningependa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Raynald Mrope, kwa jinsi alivyoweza kuwasilisha maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nimshukuru kwa pongezi ambazo amezitoa hapa kwa jinsi tulivyolishughulikia suala hili na nimshukuru pia kwa kuweza kuunga mkono hoja zote tatu, ikiwa ni yeye pamoja na Kamati nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ambayo ameyazungumzia ni ya msingi na sisi tumeyapokea, tutayafanyia kazi na huko siku za usoni haya yote ambayo wameyazungumzia yatatusaidia katika utekelezaji wa shughuli zetu. Kwa hiyo, tunapenda kusema tumepokea ushauri huo katika mambo mbalimbali ambayo ameyagusia hasa hili suala la kumtaka anayeshutumiwa kupatikana kwa njia ya Posta ama kwa njia ambazo zinaweza kuleta athari za aina fulani fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumelichukua hili shauri na Mikataba hii siyo inatufunga moja kwa moja, upo uwezekano mkubwa kabisa wa kupeleka maoni yetu kupitia Katibu wa *SADC* na kuweza kuwafikia Wakuu wa nchi na kufanya *amendments* za masuala haya. Kwa hiyo, hatuingii katika masuala haya kwa kweli kichwa kichwa, utafiti umefanywa na zipo taratibu ambazo zimewekwa ikiwa kama hatukuridhika na mambo fulani fulani basi marekebisho ya *Protocol* hizi yanaweza yakafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala zuri ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kama ilivyo kwa upande wa *East African Community,* tunazo *Protocols* za namna hiyo na kabla hatujaweza kuzikubali ama kuziridhia, tunazileta katika Vikao vya Bunge lakini *Protocol* hizi kweli zimekwishatiwa saini na Wakuu wetu wa nchi. Kwa hiyo, hiyo *point* tunaichukua na tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa nikumbushie kwamba, nia kwa kweli ya *Protocol* hizi ni kutekeleza Maazimio ambayo yamo katika ile *Treaty* yenyewe, *The Declaration and Treaty of Southern Africa Development Community,* ambayo ilitiwa sahihi tarehe 17 Agosti, 1992 kama nilivyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa ama malengo makubwa ni kuleta mshikamano wa nchi zetu na kubwa zaidi ni kutufikisha mahali ambapo tutakuwa tuna *regional integration* katika *SADC.* Kwa hiyo, haya yote kwa kweli ambayo tunajaribu kuyafanya ni kwa nia ya kutekeleza *Treaty* ile ili kujaribu kuboresha maisha ya wananchi wetu kuona kwamba, kuna *Social Justice*, kuna Utawala Bora na pia kuna Demokrasia. Kwa hiyo, nia ya *Protocol* hizi ni nzuri kama zilivyo kwa upande wa *East African Community.*

Sasa napenda nimalizie kwa mara nyingine kusema kwamba, nashukuru kwa mawazo mazuri ambayo ameyatoa na yale ambayo tunaona kwamba, yanahitaji kufanyiwa kazi katika *The Legal Sector* ya hiyo *Committee* hata kupelekwa wa Wakuu wa nchi zetu, basi tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kuomba na Kupata Msaada unaohitajika katika Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai yaani
(The SADC Protocol on Mutual Legal Assistance

in Criminal Matters)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Masuala ya Sheria
liliridhiwa na Bunge)
Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Masuala ya Sheria
(The SADC Protocol on Legal Affairs)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Masuala ya Sheria
liliridhiwa na Bunge)

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Utaratibu wa Kurejesha Wakosaji au Watuhumiwa *(The SADC Protocol on Extradition)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Utaratibu wa Kurejesha Wakosaji
wa Watuhumiwa liliridhiwa na Bunge)

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Misitu
(The SADC Protocol on Forestry)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kuwasilisha Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia Mkataba wa Ushirikiano katika Sekta ya Misitu kwa Nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne S. Makinda, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo, walioweza kuupitia Mkataba na kuchangia ili kuuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, ambayo inathamini uhifadhi endelevu wa raslimali za misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, ambayo ina azma ya kushirikiana katika kuendeleza, kuhifadhi na kusimamia misitu katika misingi endelevu, kukuza biashara ya mazao ya misitu ili kuchangia katika kuondoa umaskini na kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uanachama wetu, Sekta ya Misitu imenufaika na misaada mbalimbali iliyotolewa na wahisani kwa nchi wanachama wa Jumuiya hii. Miradi ambayo imetekelezwa au itatekelezwa kutokana na misaada hiyo ni kwanza, kuimarisha Vyuo vya Misitu kwa Tanzania na vyuo hivyo ni Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi na Chuo cha Misitu Olmotonyi Arusha. Pili, kuimarisha mtandao wa Vituo vya Mbegu na kwa Tanzania ni Wakala wa Mbegu za Miti Morogoro. Tatu, utafiti na uhamasishaji wa kilimo misitu kama HASHI Shinyanga na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tumbi, Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu ulisainiwa na Marais wa nchi 10 za *SADC* tarehe 3 Oktoba, 2002 huko Luanda nchini Angola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu unalenga katika mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Ushirikiano wa nchi katika usimamizi, umiliki na utumiaji wa raslimali za misitu na kuhimiza jamii ioteshe miti na kuihifadhi misitu;

(ii) Kuandaa Sera za Misitu, programu na mipango kwa kutumia vigezo na viashiria vya usimamizi endelevu wa misitu;

(iii) Kufanya tathmini za mara kwa mara za raslimali za misitu;

(iv) Kuanzisha na kuendesha Kituo cha Takwimu au *Data*;

(v) Kuhakikisha kwamba Sheria zinaboreshwa na kutekelezwa ili kuhimiza usimamizi endelevu wa misitu na kulinda ikolojia na misitu yenye umuhimu wa kudumisha utamaduni, dini na *species* zilizo katika hatari ya kutoweka;

(vi) Kuunda Sera zitakazohimiza ushirikishwaji wanawake katika usimamizi endelevu wa misitu;

(vii) Kuwa na programu za pamoja na Mikataba inayotekeleza usimamizi wa pamoja wa misitu inayovuka mipaka ya nchi;

(viii) Kuchukua hatua za Kisheria na kiutawala ili kudhibiti athari hasa za kiasili na zile zitokanazo na shughuli za binadamu hususan kwa misitu inayovuka mipaka;

(ix) Kutambua elimu ya jadi waliyonayo wananchi na haki zao ili wanufaike na matumizi ya elimu hiyo;

(x) Kulinda raslimali ya misitu na kuhakikisha matumizi yake yanapata ridhaa na kuweka masharti ya mgawanyo sawa wa manufaa yatokanayo na raslimali hiyo;

(xi) Kuendeleza viwanda, biashara, uwekezaji na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi na jamii;

(xii) Kuhimiza elimu, mafunzo na ufahamu kwa umma kuhusu misitu na shughuli zinazohusiana na misitu;

(xiii) Kuendeleza utafiti wa misitu na kubadilishana taarifa za matokeo ya utafiti; na

(xiv) Kupashana na kubadilishana *data* na taarifa zinazohusu usimamizi wa misitu na utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zitakuwepo gharama za utekelezaji ambazo zitajumuishwa katika Bajeti ya kila mwaka ya Wizara kutokana na ukweli kwamba, utekelezaji wa Mkataba huu ni sehemu ya kazi za kila siku za Wizara. Vile vile, miradi katika Itifaki hii inaweza kutekelezwa kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya wahisani wa Kimataifa na ushirikiano kati ya nchi marafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji wa Mkataba huu utaimarisha masuala ya udhibiti wa shughuli za misitu ndani na nje ya nchi na hivyo kutekeleza Sheria ya Misitu kikamilifu. Aidha, Tanzania itapata manufaa yafuatayo:-

- Kuboresha usimamizi wa matumizi endelevu ya miti na misitu.
- Kulinda mazingira na kuboresha njia za upatikanaji wa manufaa yatokanayo na raslimali ya misitu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

- Kukuza biashara ya mazao ya misitu ndani na nje ya nchi kwa lengo la kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu kama ulivyoainishwa kwenye Ibara ya 26 ya Mkataba ambayo inahitaji nchi wanachama kuridhia Mkataba huo kwa mujibu wa Katiba za nchi zao, naliomba Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili, liazimie kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuridhia Mkataba wa Ushirikiano katika Sekta ya Misitu kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The SADC Protocol on Forestry).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio lenyewe linasomeka kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*;

NA KWA KUWA lengo kuu la Itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano miongoni mwa nchi katika kuhifadhi na kusimamia raslimali za misitu bila kupoteza uhuru na maslahi ya msingi ya nchi;

NA KWA KUWA madhumuni ya Itifaki hii ni kuwezesha nchi wanachama kushirikiana katika kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza misitu hasa ile ambayo umuhimu na manufaa yake yanavuka mipaka ya nchi wanachama moja au zaidi;

NA KWA KUWA Tanzania ikijiunga na Itifaki hii itafaidika kwa kushirikiana pamoja na nchi wanachama katika uhifadhi endelevu na usimamizi wa raslimali za misitu. Aidha, kuridhia Itifaki hii ni hatua mojawapo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002;

HIVYO BASI, baada ya kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii na kwamba nchi yetu itanufaika kutokana na Itifaki ya Ushirikiano katika Sekta ya Misitu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaombwa katika Mkutano wake wa kumi na mbili na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa liazimie kuridhia Itifaki ya *SADC* ya ushirikiano katika Sekta ya Misitu kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika kwa jina lingine "*The SADC Protocol on Forestry".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. WILLIAM J. KUSILA (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Ushirikiano katika Sekta ya Misitu kwa nchi za *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Ushirikiano katika sekta ya misitu kwa nchi zilizo kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, pamoja na Marais wengine wa Jumuiya ya *SADC,* kwa kuikubali na kuweka saini katika Itifaki hii ambayo ni muhimu sana kwa nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kujiunga na nchi nyingine ambazo ni wanachama wa *SADC* katika kuwa na Itifaki kama hii kwani ulimwengu wa sasa ni wa ushirikiano hususan katika kukabiliana na masuala ya utunzaji bora wa aina zote za misitu kwa lengo la kuwa na matumizi endelevu ya hifadhi ya mazingira. Bahati nzuri Tanzania tayari tunayo Sheria ya Misitu na Nyuki ya mwaka 2002. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kujiandaa kikamilifu katika kutekeleza

yaliyomo katika Itifaki hii. Maeneo yote muhimu ya Itifaki hii ambayo yametajwa inabidi yafahamike kwa wadau mbalimbali.

Aidha, kufanya hivyo, nchi yetu na wananchi wake kwa ujumla, wanaweza kunufaika na kufaidika kutokana na Itifaki hii. Pia kwa kutekeleza Itifaki hii, nchi yetu itaweza kukuza biashara ya mazao ya misitu ndani na nje ya nchi kwa lengo ya kuboresha maisha ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu mzuri wa jinsi ya kutoa elimu kwa wadau na kuwawezesha kimtaji ili waweze kushiriki vizuri. Mara nyingine sisi Watanzania huwa tunakuwa watazamaji katika mambo hata yale ambayo tunapaswa kushiriki kikamilifu kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Itifaki hii inahusu masuala ya utunzaji misitu ambayo ni muhimu sana kwa jamii nzima ya Kitanzania. Hivyo, Kamati inashauri kuwa katika siku za usoni wadau mbalimbali kwa kuanzia ngazi za Vijiji, Wilaya, Mikoa na Taifa, zikiwemo Halmashauri za Wilaya, *NGOs* na watu binafsi, washirikishwe katika utekelezaji wa Itifaki hii ya Sekta ya Misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Misitu na Nyuki ambazo tumeshazitunga, Serikali iangalie uwezekano wa kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuzisoma na kuzielewa. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii iangalie namna ya kuwa na Mfuko Maalum wa kusaidia wafanyabiashara wa bidhaa za misitu kama vile mbao, kamba, nta na asali kwa lengo la kuuza nje ya nchi kwa ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali ihakikishe kuwa miradi itakayotokana na misaada ya Itifaki hii inafaidika kwa kiwango cha juu na baadhi ya miradi hiyo ni kama Vyuo vyetu vya Misitu kama vile Chuo cha Misitu Olmontonyi Arusha, mtandao wa vituo vya mbegu za miti na utafiti na uhamasishaji wa kilimo cha misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea na dhana ya kuhifadhi misitu, matumizi mbadala ya nishati yaendelezwe yakiwemo matumizi ya umeme na gesi. Vyanzo hivi ni vya ghali sana kwa wananchi. Serikali iwe makini kuona namna ya kupunguza gharama zake ili wananchi wengi waweze kutumia vyanzo hivi badala ya matumizi makubwa ya mkaa hivi sasa mijini na vijijini. Pamoja na uharibifu wa misitu, muda mwingi hutumika kutayarisha nishati hii ya kuni na mkaa, muda ambao ungetumika kwa uzalishaji au kuongeza kipato. Serikali ione uhusiano uliopo kati ya umaskini na uharibifu wa mazingira ambao ni watoto mapacha kama alivyosema Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu, Bwana Solomon Odunga, pamoja na wataalam wake kwa ushirikiano wao mzuri ambao ulifanya kazi hii kuwa nyepesi wakati wa kupitia na kujadili Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuijadili Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, Kamati inapendekeza Azimio la Itifaki hii lijadiliwe na Bunge lako Tukufu na kisha kuliridhia kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni kuhusu Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Misitu, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 43(b)(c), Toleo la 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natanguliza shukrani na pongezi kwa kuwasilisha Mkataba huu wa ushirikiano katika Sekta ya Misitu kwa nchi za *SADC*. Mkataba umeainisha kwa undani na umewafikiria wadau wote wa ndani ya nchi mathalani akina mama na pia umetoa uchambuzi wa utafiti wa kina ambao ulishafanywa na wataalam mbalimbali kwa kuwa akina mama ndio wahusika wakuu katika

familia hivyo, kutambuliwa kwao ni hatua kubwa ya kuhakikisha kwamba, mradi huu una uwezo wa kuwa na waangalizi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba umetambua na kuthamini uzoefu na maoni ya wanajamii waishio katika maeneo yanayotarajiwa kuwa na miradi ya misitu. Kwa mantiki hii, hata wananchi wanakuwa na moyo wa kujitolea inapobidi kwani wananchi kuwa sehemu ya mradi huo na sio mradi wa kuwa mali ya Serikali. Jukumu kubwa la Serikali ni kuwapa uelewa wananchi kuhusiana na umuhimu na manufaa ya Mkataba huu. Mfano, wananchi wakishirikishwa na kujua umuhimu wa misitu inayowazunguka wataweza kuihifadhi na kuitunza kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waeleweshwe umuhimu wa kupanda miti, hivyo basi utaratibu wa kata mti panda mti ubadilishwe na kuwa panda miti kata mti na hii iambatane na upatikanaji wa teknolojia rahisi ya kupikia badala ya kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha kuondoa ukiritimba wa biashara katika mazao ya misitu baina ya nchi wanachama, Mkataba umeainisha vizuri ila wasiwasi unakuja kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi ya Upinzani baada ya kuzingatia haya yote, haina matatizo ya kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kuwa wakati Mheshimiwa Waziri, anasoma Itifaki hii alitaja Chuo cha Mbegu cha Morogoro na mimi ni mdau wa Chuo kile, sitangazi *interest* yangu, mimi ni mdau tu.

Katika maelekezo ambayo pengine yatasomwa kwenye *Hansard* ya Msemaji wa Upande wa Upinzani katika kurasa mbalimbali ambazo wakuu wa nchi waliambiwa wasaini pale, katika ukurasa wa 14, *Legal Affairs,* Botswana na Kongo hawakusaini. Katika *instruction* tarehe 3 Oktoba, 2002 Mozambique na Zambia hawakusaini, katika *first day* tarehe 3 Oktoba, 2002, Bostwana, Mozambique, Namibia, Zimbabwe hawakusaini. Sasa sio Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhoji hawa, ni Mabunge yao yatahoji kwa nini hawakusaini, sisi kwa sababu Rais wetu amesaini, kwa hiyo, tunaridhia si kazi yetu kuhoji nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia ile Kanuni ya Bunge nilidhani Mikataba yote inapita kwenye Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje. Kwa bahati nzuri kwenye kila kipengele cha Kamati katika upande wa majukumu Ibara ndogo ya pili, kipengele kidogo cha II katika kila kurasa za Kamati hizo, isipokuwa tu bila kuathiri ukweli wa Kamati yenyewe, Kamati kwa mfano ya Uongozi, Kamati Teule na Kamati ya Kanuni nyingine ambazo zinahusika na mambo hayo, zote zimepewa mamlaka hayo katika kuridhia Mkataba ambao unakuja kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ni kwamba, kuungana na wakuu wa nchi zilizokuwa zimeketi katika Mikataba hiyo ni suala muhimu lakini mapungufu yaliyojitokeza katika sekta ambayo inahusika katika nchi mbalimbali ni jukumu la nchi hizo kusimamia majukumu hayo kwa kutekeleza sheria zao na kuimarisha sekta ambazo zimetajwa katika Mkataba wenyewe, hilo ni jukumu la nchi zinazohusika. Kwa hiyo, nchi zichemke katika kusimamia Mikataba yote, sheria kama zilikuwa hazikidhi basi ziendelee kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, tulipitisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa hapa unaohusu mambo ya ardhi oevu na mambo ya Mikataba ya misitu na tulishauri kwamba, kuwepo na nishati mbadala. Lakini badala ya kuleta nishati mbadala naona kuna utiriri wa majiko mbadala, kuna majiko ya mkaa ambayo yanatumia mkaa kidogo. Sasa ile siyo *solution* ya kulinda mazingira. Kwa kweli wana mazingira duniani tunaomba wagundue nishati mbadala kama wale wananchi wa Kiloka ambao waligundua tofali moja kwa kutumia *one by three by four* kwa kutumia majani na udongo kidogo na aina fulani ya kemikali kutengeneza tofali ambalo linaweza kuivisha kitu wakati huo. Kwa hiyo, teknolojia ile ndio inafaa katika kuondoa *frustration otherwise* Tanzania katika miaka ijayo itakuwa haina misitu itakuwa na vichaka na mapori badala ya kuzungumzia misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana wananchi wenzetu wa kule Tabora, Kigoma, lakini wakimbizi ndio wanaharibu mazingira. Kwa hiyo, Itifaki hii itazuia uharibifu wa mazingira wanapokuja tu wanawapatia nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kwanza nimshukuru Mheshimiwa William Kusila kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kwa taarifa ya uchambuzi waliofanya katika Itifaki hii. Pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, pamoja na Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, maoni na uchambuzi wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, wamefanya uchambuzi wa kina na kama ilivyo wajibu wa Bunge Tukufu, kwa mujibu wa Katiba, moja ya kazi kubwa ya Bunge ni kuishauri Serikali na kwa kweli katika maoni yaliyotolewa umepatikana ushauri mzuri sana wa nini tunatakiwa kama wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika tunaporidhia Itifaki hii ni mambo gani tuyazingatie katika kuitekeleza Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ambapo wataalam wake wako hapa, nina hakika wamechukua *notes* za haya yaliyotokana na ushauri wa Kamati na bila shaka yatafanyiwa kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine tu niruhusu niseme lile la msingi kwa sababu kwa kawaida Itifaki ni utaratibu wa utekelezaji wa jambo mlilokubaliana na tumeambiwa Wakuu wa nchi katika *SADC* walishakubaliana Mikataba ya msingi. Lakini hii Itifaki inayohusu eneo la misitu ukitaka kupata hasa ni nini kinacholengwa hapa ukienda katika ile *paragraph* ya kwanza kabisa, Wakuu wa nchi wanaposema wanakumbuka na kuzingatia. Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nisome kwa lugha ya Kingereza mistari mitatu au minne inasema: *"Recalling that the objectives of the Southern African Development Community (SADC) include achieving development and economic growth, poverty alleviation with alternate objective of its eradication and achieving sustainable utilization of natural resources and effective protection of the environment"*. Hili ni lengo na nina hakika Kamati imetukumbusha kwamba, tuyazingatie haya kwa mfano anapozungumzia juu ya nishati mbadala, majiko sanifu ingawa Mheshimiwa Semindu Pawa, anasema vema tuseme majiko sanifu lakini pia tutafute nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tunapokumbuka kwamba, *SADC* ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa na tunao Mkataba wa Kimataifa unaohusiana na bioanuwai. Tunapozungumzia misitu tuna kitu tunasahau katika bioanuwai maana misitu pengine tunaichukulia kama miti na misitu yenyewe lakini unapozungumzia bioanuwai unasema: *"A recognizing the intrinsic value of forests and their vital role in the functioning of the ecological systems* na maneno muhimu ni haya *and maintenance of all forms of life* na sisi binadamu pia ni *form of life"*. Kwa hiyo, haya ndio yanasisitizwa kwamba, tunapofanya ushirikiano katika nchi za *SADC* tuzingatie kwamba, hili linahusu hata uhai wetu sisi wenyewe binadamu. Nilitaka nitoe tu kwa uchache haya ambayo ni ya msingi katika ushauri tulioupata na tutauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme moja kuhusu baadhi ya nchi kuonekana kwamba, hawajasaini katika *document* tuliyonayo. Katika utaratibu wa Mikataba hii ya Kimataifa mkikubaliana kuwa na Mkataba au Itifaki kama hivi, wale Wakuu wa nchi au Wawakilishi wa nchi waliohudhuria mkutano wanaweka saini katika makubaliano yale siku ile ile. Lakini Mkataba ule au Itifaki ile inatoa muda wa wengine kuweka saini zao. Kwa hiyo, kama kwa tarehe hii inayoonekana sio kwamba nchi zote, unaona kuna baadhi ya nchi hazikusaini si kwa sababu haziafiki yale maudhui ya Itifaki yaliyomo, ni utaratibu wa Mikataba ya Kimataifa, mnaweza kusaini siku ile ile au siku za baadaye, huwa unatolewa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru tena Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kuunga mkono kwa sababu hili ni jambo la msingi, ni kama *sustenance* ya *forms of life* hata Kambi ya Upinzani sote ni binadamu tulio hai. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa *observation* hii muhimu na niseme tu kwamba, ushauri wote uliotolewa tutauzingatia na kuufanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Misitu liliridhiwa na Bunge)

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Utamaduni, Habari na Michezo
(The SADC Protocol on Culture, Information and Sports)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, lipitishe Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* kuhusu utamaduni, habari na michezo. Azimio hili lilipata ridhaa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kikao chake cha tarehe 24 Julai, 2003 kilichofanyika hapa Dodoma.

Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati hiyo, pamoja na Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, kwa ushirikiano na maoni yao mazuri ambayo yatazingatiwa wakati wa utekelezaji wa Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi 14 ambazo ni Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).* Ushirikiano katika masuala ya utamaduni, habari na michezo ni muhimu sana katika kuwahusisha wananchi wa kawaida wa nchi zinazoshirikiana katika maendeleo. Itifaki ya ushirikiano katika maeneo hayo ilisainiwa na Wakuu wa nchi na Serikali katika mkutano uliofanyika tarehe 14 Agosti, 2001 huko Blantyre Malawi. Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliweka saini kwa niaba ya nchi yetu. Tangu kuanzishwa kwa *SADC,* mambo kadhaa yamefanyika katika maeneo ya utamaduni, habari na michezo kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzisha Tunzo ya Uandishi wa Habari *(Media Award)* ya *SADC;*

(ii) Kuchapisha kila robo mwaka kijarida cha *SADC* cha masuala ya utamaduni, habari na michezo kiitwacho *Southern African Culture Information and Sport News (SACIS News);*

(iii) Kuanzisha Shirika la Utangazaji la *SADC* liitwalo *SABA* ambalo hukusanya vipindi vya redio kutoka nchi wanachama na kuvisambaza;

(iv) Kuanzisha matamasha ya utamaduni katika nchi za *SADC;*

(v) Kuchukua hatua za awali za kuanza kuunda Mfuko wa Utamaduni wa *SADC;* na

(vi) Kuchukua hatua za awali za kuanza kuwa na Tuzo ya Utamaduni ya *SADC* itakayojulikana kama *Hall of Fame.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii imeandaliwa kwa kutambua kuwa ushirikiano katika utamaduni, habari na michezo unasisitizwa na Mashirika ya Kimataifa yanayohusika na fani hizi. Utamaduni wa michezo ni fani ambazo zina nafasi kubwa katika kuimarisha uhusiano na mshikamano miongoni mwa Mataifa mbalimbali. Michezo inasaidia sana katika kuimarisha jamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa ikiwa ni pamoja na kuwajengea watu hali ya kujiamini. Sekta ya Habari na Mawasiliano husaidia katika kuimarisha Jumuiya za Kimataifa kama hii yetu. Aidha, Itifaki hii itasaidia katika kupanua wigo wa ushiriki wa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ina jumla ya sura tano, sura ya kwanza inatoa tafsiri ya istilahi zinazotumiwa na misingi mikuu ya ushirikiano wenyewe ambayo ni:-

(i) Kutekeleza sera na mipango kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa *SADC* kifungu cha nne;

(ii) Kushirikiana katika matumizi ya raslimali za miundombinu na utaalam;

(iii) Kujenga utambulisho wa nchi za *SADC* bila kuathiri tofauti za utamaduni kati ya nchi na nchi; na

(iv) Kuwezesha wadau mbalimbali na wananchi kwa jumla kupata habari muhimu na kushiriki katika shughuli za utamaduni na michezo bila vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya pili, inaainisha na kufafanua vipengele vya ushirikiano ambavyo ni:-

(i) Uainishaji wa sera za utamaduni, habari na michezo za nchi wanachama;

(ii) Mafunzo na utafiti;

(iii) Ushirikiano katika matumizi ya miundombinu na utaalam;

(iv) Kubadilishana habari;

(v) Ushirikiano wa wadau mbalimbali;

(vi) Masuala ya haki na usawa wa jinsia katika utamaduni, habari na michezo; na

(vii) Ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika shughuli za utamaduni, habari na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya tatu, inafafanua kwa undani zaidi aina za ushirikiano katika utamaduni, habari na michezo. Sura ya nne, inaainisha utaratibu katika ushirikiano kwa kuanzisha Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Itifaki na aidha inaweka utaratibu wa kugharamia shughuli za ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya tano, inaweka utaratibu wa mambo mbalimbali ikiwemo uhuishaji wa Itifaki, kutatua migogoro inayohusu tafsiri, kuweka saini, kuridhiwa na tarehe ya kuanza kutumiwa kwa Itifaki ambayo ni siku 30 baada ya kuridhiwa na angalau theluthi mbili ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii itakuwa na manufaa yafuatayo kwa nchi yetu:-

(a) Kubadilishana utaalam na uzoefu na wenzetu katika nyanja za utamaduni, habari na michezo;

(b) Wasanii, wanahabari na wanamichezo mbalimbali wa nchi yetu watahamasika na kuinua viwango vyao kutokana na kushiriki katika matamasha ya utamaduni, mashindano ya michezo, pamoja na utaratibu wa kutoa tuzo kwa wale wote wanaofanya vizuri zaidi katika nyanja hizi;

(c) Watanzania wataimarisha taaluma zao kutokana na kushiriki katika programu za mafunzo za *SADC;*

(d) Asasi zetu za mafunzo zitakazoteuliwa kuhudumia nchi wanachama zitakuwa na fursa zaidi ya kuendelezwa kwa michango ya *SADC;*

(e) Nchi yetu itaweza kupunguza utegemezi wa vipindi vya redio na *television* kutoka nje ya Bara la Afrika kutokana na utaratibu wa kubadilishana vipindi miongoni mwa nchi wanachama;

(f) Nchi yetu itafaidika na ufadhili kutoka Mfuko wa Utamaduni wa *SADC* pindi utakapokuwa umeanzishwa; na

(g) Tutanufaika kutokana na utaalam na uzoefu wa nchi wanachama katika kushughulikia masuala ya jinsia na ulemavu katika utamaduni, habari na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kugharamia na kuchangia programu mbalimbali zitatengwa katika Bajeti za Wizara zinazosimamia masuala ya utamaduni, michezo na habari, pamoja na asasi nyinginezo zitakazohusika na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge hili Tukufu, lipitishe Azimio lenyewe kama lilivyoambatanishwa katika orodha ya shughuli za Bunge za leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu utamaduni, habari na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 100(2)(2), Kamati ya Huduma za Jamii, ilipata muda wa kutosha kufikiria Azimio hili aidha, Kamati ilipitia vifungu vyote vya Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata maelezo na ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kuhusu itifaki ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* inayoanzisha ushirikiano katika nyanja za utamaduni, habari na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Itifaki hii inahusu Wizara tatu nazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala ya Habari, Wizara ya Elimu na Utamaduni, masuala ya utamaduni na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa masuala ya michezo. Hivyo, Waziri wa Elimu na Utamaduni akisaidiana na wataalam toka Wizara yake, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, walitoa maelezo na ufafanuzi kuhusu Itifaki hii.

Kutokana na maelezo na ufafanuzi uliotolewa, Kamati yangu iliridhika na kukubali kuwa Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika inayohusu utamaduni, habari na michezo, iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu, hivyo, Kamati yangu inaunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, Kamati ilitoa mapendekezo na maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kujiunga na Itifaki ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* inayoanzisha ushirikiano katika utamaduni, habari na michezo. Tarehe 14 Agosti, 2001 ndiyo siku ambayo Viongozi Wakuu wa Nchi za *SADC,* akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliweka sahihi Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile inaipongeza Serikali kwa kuleta Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* inayohusu utamaduni, habari na michezo bila kuchelewa sana kama ilivyokuwa katika Mikataba mingine ili ipate nguvu ya Kisheria na utekelezaji wake uweze kuanza na hatimaye nchi yetu inufaike na Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikiano katika utamaduni, Kamati inakubaliana na ushirikiano katika utamaduni. Kamati inakubaliana na ushirikiano unaoanzishwa na Itifaki hii katika masuala ya utamaduni hasa kubadilishana utaalam, ujuzi na uzoefu katika nyanja za utamaduni ikiwa ni

pamoja na kuandaa tamasha mbalimbali za pamoja na kuweza kulinda utamaduni wa nchi hizi kwa ajili ya vizazi vijavyo *(Cultural Heritage).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaunga mkono malengo ya Itifaki ya kuainisha nchi wanachama kuanzisha vituo vya utamaduni kibiashara, ambavyo pamoja na kulinda na kuendeleza utamaduni wa nchi pia vinatakiwa vitumike kuongeza mapato ya nchi.

Hivyo, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa nchi yetu tayari ina Chuo cha Utamaduni cha Bagamoyo, ambacho kimeteuliwa kuwa Chuo cha Ubora wa Hali ya Juu *(Centre of Excellency)* kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali iboreshe na ikitangaze Chuo hiki ili kiweze kukidhi matakwa na mahitaji ya nchi za *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile imeridhika kuwa Itifaki hii inaweka misingi ya kuanzisha vituo vya kuendeleza vipaji *(Centres of Talents Development)* katika fani mbalimbali za utamaduni, habari na michezo ikiwa ni pamoja na kutafiti na kuendeleza lugha za asili za nchi wanachama wa *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudi za kuimarisha Taasisi ya Lugha za Kigeni *(ETROTANA),* iliyopo Zanzibar, ambayo imepata hadhi ya Kimataifa *(Centre of Excellency)* kwa ajili ya kutafiti na kuendeleza lugha za asili ili iweze kutumika kwa manufaa ya wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaafiki kuanzishwa kwa ushirikiano wa michezo miongoni mwa nchi za *SADC*. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuwa pamoja na uanzishaji wa vituo vya kuendeleza vipaji *(Centres of Talents Development)* katika fani mbalimbali za michezo, ni muhimu sana Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo itekeleze jukumu lake la kusimamia maendeleo ya michezo nchini kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Michezo.

Kamati vile vile inashauri kuwa chini ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* Taifa letu linatakiwa kuimarisha maeneo yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha umma kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo vya mwili na kujenga hali ya ushindani miongoni mwa jamii.

(b) Kuhakikisha kuwa Wizara inaendesha mafunzo ya uongozi, ualimu, uamuzi na utawala wa michezo yote.

(c) Kuhakikisha kuwa Serikali inasimamia utekelezaji wa Itifaki hiyo ya Ushirikiano katika kufanya tafiti mbalimbali za Sheria na kanuni za michezo na kuzirekebisha kulingana na mabadiliko katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania imeendelea kushiriki katika michezo na nchi za *SADC* hata kabla ya Itifaki hii kusainiwa, Kamati inaona kuwa utekelezaji wa Itifaki hii utaongeza kiwango cha ushirikiano katika nchi hizi kwa ajili ya mikutano, semina, makongamano, mashindano ya Kimataifa na kuinua ubora wa michezo na mbinu za kisasa katika medani za michezo kwa viwango vya Kimataifa.

Aidha, ushirikiano wa michezo katika nchi za *SADC* utajenga uwezo wa nchi hizi kushiriki katika michezo na mashindano ya Bara la Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri Serikali kuwa kwa kutumia utaalam, uzoefu na ufundi utakaopatikana kwenye Itifaki hii katika michezo mbalimbali, Serikali ifanye jitihada za makusudi

za kuunda na kuimarisha timu za Taifa za kudumu katika michezo mbalimbali ili timu zetu ziweze kuwa za ushindani badala ya utaratibu wa sasa wa kuziunda kwa dharura muda mfupi kabla ya mashindano na hatimaye timu hizo mara nyingi hufanya vibaya katika michezo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue hatua hizo pamoja na kutenga Bajeti kwa ajili ya timu za Taifa, kutafuta, kutambua, kukusanya na kuendeleza vijana na watoto wenye vipaji vya michezo katika vituo maalum na hatimaye kuunda timu bora zenye kutoa ushindani katika michezo ya ndani na michezo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Serikali ianzishe utaratibu wa kuandaa timu za Taifa kwa kuendeleza wenye vipaji vya michezo pia ihusishe watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali kwani Itifaki hii inatambua umuhimu wa kuwaendeleza na kuwashirikisha kikamilifu katika michezo ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono Itifaki ya *SADC* kwa kuanzisha ushirikiano wa kubadilishana habari miongoni mwa nchi za Kusini mwa Afrika. Vile vile Kamati inaunga mkono kuanzishwa Mfuko wa kuendeleza utafiti katika utamaduni, habari na michezo katika nchi za *SADC* ambao vyanzo vyake vya fedha ni michango toka nchi wanachama za *SADC*, wafadhili na wahisani kutoka nje ya nchi hizo.

Kamati inashauri kuwa ili nchi yetu iweze kunufaika vizuri na Itifaki hii, Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuandaa na kuboresha mazingira yanayotakiwa kwa kutoa michango ya uanachama kila mwaka, kuandaa wasanii, wanamichezo na wanahabari wenye sifa na wenye uwezo wa kutumia miundombinu ya kisasa ya mawasiliano na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Itifaki hii inaanzisha utaratibu wa kubadilishana utaalam katika kutoa habari ikiwa ni pamoja na kubadilishana vipindi vya redio na televisheni, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue tahadhari zote za kuhakikisha kuwa habari na burudani zitakazotolewa kwa umma zinazingatia maadili mema ya Watanzania na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na dhana ya kuanzisha tuzo ya Uandishi wa Habari ya Nchi za *SADC,* kwa nia ya kuhamasisha na kutambua kazi nzuri itakayofanywa katika kuelimisha jamii. Hatua hii itawezesha wanahabari wetu kujizatiti na kutumia taaluma zao katika kukusanya, kuandaa na kusambaza habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inaikubali hoja ya kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji la Nchi za *SADC,* likiwa ni chombo cha kusambaza na kubadilishana habari miongoni mwa nchi wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona muda umekwisha, ili kutoa haki kwa maoni ya upande wa Upinzani kwa dakika zile hautoshi. Kwa hiyo, kesho upande wa Upinzani utatoa maoni yake halafu wachangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Mutungirehi, wa pili ni Mheshimiwa Mgaywa na wa tatu ni Mheshimiwa Dr. Lamwai. Tunamalizia kwa hao tu.

Suala la pili, kuna tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, linasema kuna Waheshimiwa Wabunge wengi, wamekuwa wakitaka kushiriki kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa *ALAT* unaofanyika Ukumbi wa Chimwaga Dodoma. Kuna baadhi wangependa kwenda kule na kwamba masuala yanayojadiliwa yametokana na uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi mbalimbali. Sasa

wanaotaka kwenda wanaweza kwenda kesho, lakini saa tisa. Bunge linaendelea na mambo yake kama kawaida. Ila wakati wako saa tisa unaweza kwenda kule.

Baada ya matangazo haya, Waheshimiwa Wabunge, naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 01.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 6 Agosti, 2003 Saa Tatu Asubuhi)